

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA ISHIRINI

Kikao cha Saba - Tarehe 15 Juni,2010

(Mkutano ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI:

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU BUNGE:

Randama za Makadirio ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 45

Upatikanaji wa Namba na Hati kwa Vijiji vilivyokwishapimwa

MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA aliuliza:-

Kwa kuwa, Vijiji vya Maleza, Kata ya Mbagala na Ndanga Kata ya Mbuyuni, vilivyoko kwenye Jimbo la Songwe vilikwishapimwa na kuandikishwa kwa muda mrefu sasa lakini havijapatiwa Namba na Hati zao:-

- (a) Je, ni lini vijiji hivyo vitapatiwa Namba na Hati?
- (b) Kama kazi ya kuvipatia namba vijiji hivyo itaendelea kuchukua muda mrefu. Je, isingekuwa vyema vijiji hivyo vikaingizwa kwenye utaratibu wa kupatiwa ruzuku?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Guido Gorogolio Sigonda, Mbunge wa Songwe, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Kijiji cha Maleza kilicho katika Kata ya Mbagala kiliandikishwa baada ya kutimiza vigezo vyote. Hata hivyo, kijiji hicho hakikupatiwa Hati ya kuandikishwa vijiji rasmi wakati huo kutokana na kuwepo kwa maombi mengine yaliyokuwa yanachambuliwa ili uandikishaji wa vijiji vyote vitakavyokuwa vimetimiza vigezo viweze kupatiwa Namba na Hati za kuandikishwa kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Tangazo la Serikali Na. 205 la tarehe 26/6/2009 ilitangaza vijiji vipya kwa ajili ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliofanyika Oktoba 25, 2009. Katika Tangazo lile la Serikali Na. 205 ambalo linatambua Ndanga kama Kitongoji ndani ya Kijiji cha Mbuyuni, Kata ya Mbuyuni, ilidhihirika kwamba kuna baadhi ya vijiji vingine vilisahaulika wakati wa kuchapisha Tangazo hilo. Serikali iliamua kupitia upya Tangazo hilo la Serikali kuboresha kasoro zilizojitokeza ili Hati stahiki ambayo ndiyo inakuwa na namba kwa vijiji vyote vipya ziweze kutolewa kwa wakati mmoja kwa lengo la kuondoa mikanganyiko inayoweza kujitokeza.

Kazi hiyo sasa imekamilika na Tangazo Na. 17.9 la tarehe 14 Mei, 2010 liko kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuchapishwa. Baada ya tangazo kutoka utaratibu wa kutoa Hati utafanyika.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vijiji ambavyo havijapewa Hati kupewa ruzuku, namshauri Mheshimiwa Mbunge awasiliane na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ili kijiji hicho kiweze kuwekwa kwenye orodha ya Vijiji vinavyopata ruzuku. Kigezo kikubwa cha kijiji kupata ruzuku ya uendeshaji ni kusajiliwa na kuchagua uongozi wa Serikali ya Kijiji.

MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA: Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Naibu Waziri kwa jibu lake ambalo lina matumaini. Lakini kwa sababu swala hili ni la muda mrefu sana. Je, hiyo Hati kuchapishwa na yenyewe itachukua muda mrefu kama ilivyokuwa?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, najua swali hili linagusa pia na Wabunge wengine wengi ambao wamekuwa wakiulizia jambo hili. Nataka nimthibitishie sasa kwamba baada ya hili zoezi kukamilika na baada ya kwamba sasa tangazo kukamilika na baada ya kuwa sasa tangazo litatoka na tutawatangazia pia na Wakurugenzi kwamba uchaguzi mdogo uweze kufanyika, nina hakika kabisa kwamba Hati hizo hazitachelewa kama ilivyokuwa kwa sababu tutakuwa tumemaliza tatizo la msingi (*Makofi*)

MHE. MOHAMMED R. ABDALLAH: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Hivi kweli inakubalika kwamba Kijiji kimepimwa na kina Hati na hatimaye kuuziwa Mwekezaji na Serikali kutotoa maamuzi ya haraka, kwamba haiwezekani Mwekezaji kuwekeza katika kijiji hicho kwa sababu hicho Kijiji tayari kina Hati na ni ya Serikali ya Kijiji. Suala hili limetokea kwenye Kijiji cha Mivukoni, Pangani.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, ukiziangalia sheria zote mbili za Vijiji na zile za Ardhi, uamuzi wa kutoa ardhi kwa ajili ya mtu mwingine yeyote yule unafanywa na Kijiji chenyewe kupitia Serikali yake na kupitia Mkutano Mkuu wa Kijiji. *That is the bottom line*, hakuna mtu mwingine yeyote pale anaweza kupitisha maneno bila kupata ridhaa ya wanakijiji wake kwa maana ya Mkutano Mkuu wa Kijiji. Kwa hiyo kama kuna jambo lolote ambalo limefanyika nje ya hapo, *then* hili jambo ni la kufuatilia na kujua kwamba ilikuwaje ikawa hivyo kwa sababu Kijiji lazima kitamke pale na uongozi wa Halmashauri pamoja na uongozi wa Wilaya ni lazima ujue kwamba kuna jambo la namna hii ambalo limetokea pale. (*Makofi*)

MHE. JOHN S. MALECELA: Mheshimiwa Naibu Spika nashukuru sana kwa kuniruhusu kuuliza swali la nyongeza.

Wakati wa kugawa Wilaya ya Dodoma Vijijini ilitokea Wilaya mbili, Wilaya ya Bahi na Wilaya ya Chamwino. Katika upande wa Wilaya ya Chamwino kuna tarafa ambayo mpaka sasa, huu ni mwaka nadhani ni wa tatu bado haijatangazwa kwenye gazeti ili itambulike kama ni tarafa. Mwanzo nilishughulika na aliyekuwa Waziri wa TAMISEMI ambaye sasa ni Waziri Mkuu baada ya hapo nimeshughulika na Mawaziri wote wanaohusika mpaka sasa na kila wakati naambiwa itafanywa.

Je, Naibu Waziri anaweza kulihakikishia Bunge hili na Wananchi wa Mtera kwamba suala hilo la kuandikisha Tarafa hiyo katika Gazeti la Serikali ili itambulike rasmi ijulikane?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, uamuzi wa mwisho wa kusema kwamba hii inakuwa ni Tarafa au si Tarafa unafanywa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na jambo ambalo analizungumzia Mzee Malecela hata mimi mwenyewe amewahi kuniona na mimi mwemyewe nilikuwa na ziara ya Mkoa wa Dodoma. Kwa hiyo nilikwenda mpaka Mtera na amelizungumzia jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimthibitisha kwamba tumezungumza na Mheshimiwa Waziri Mkuu na kwamba kuna watu wengine pia ambao wametaka kuanzisha Tarafa. Nataka nithibitisha hapa kwamba Tarafa anayoizungumzia Mzee Malecela ambayo tatizo lake lilikuwa ni jina tu kwamba tumehama pale, lilikuwa katika mapendekezo ambayo yamepelekwa kwa Mheshimiwa Rais kwa ajili ya kuweza kufanya uamuzi wa mwisho ili iweze kuwa Tarafa kama anavyosema Mzee Malecela.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nithibitisha kwamba katika mchakato hili jambo lilipita (*Makofi*)

Muundo wa Serikali za Mitaa-Jiji la Dar es Salaam

MHE. CHARLES N. KEENJA aliuliza:-

Kwa kuwa, mwezi Mei, 2008 Ofisi ya Waziri Mkuu iliunda Kamati ya Mmari kutathmini Muundo wa Serikali za Mitaa katika Jiji la Dar es Salaam na kupendekeza njia za kuboresha muundo huo ili utekeleze kwa ufanisi majukumu yaliyokusudiwa; na kwa kuwa, Kamati ilipewa muda wa mwezi mmoja kukamilisha tathmini hiyo na kuwasilisha taarifa yake lakini zaidi ya mwaka mmoja umepita tangu Kamati iundwe:-

- (a) Je, ni mambo gani makubwa na muhimu yaliyopendekezwa na Kamati hiyo?
- (b) Kwa kuwa, umepita muda wa zaidi ya mwaka mmoja tangu Kamati hiyo ilipoundwa. Je, ni mambo gani ambayo yameshatekelezwa na yapi yamezingatiwa katika Bajeti ya mwaka 2009/2010?
- (c) Je, ni sababu zipi zilisababisha kuchelewa kwa utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati na ni lini taarifa yao itasambazwa kwa Wabunge na kuwekwa wazi kwa wakazi wa Dar es Salaam?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Charles Ndelianarua Keenja Mbunge wa Ubungo lenye sehemu a, b na c kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua ya kupitia Muundo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa Mkoa wa Dar es Salaam, ilitokana na matatizo ya uendeshaji yaliyopo katika mamlaka hizo, Matatizo hayo ni pamoja na:-

- (a) Udhaifu katika uratibu wa shughuli za Mamlaka za Serikali za Mitaa.
- (b) Malalamiko mengi kuhusu utoaji huduma usioridhisha.
- (c) Kuingiliana kwa majukumu kati ya Mamlaka hizo na ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Kamati iliyoongozwa na Ndugu Deotrephe Mmari, ambaye alikuwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kukamilisha kazi yake, iliwasilisha taarifa serikalini ambayo ilikuwa na mapendekezo yanayohusu Muundo,

Utawala, Sheria zinazotawala Jiji kwa sasa, Majukumu, ongezeko kubwa la idadi ya watu na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupitia na kuchambua mapendekezo ya Kamati Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI ilitambua umuhimu wa matokeo, mapendekezo na ushauri wa Kamati kujadiliwa na kutolewa maoni na wadau husika.

Hivyo taarifa hiyo zilisambazwa katika Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Manispaa za Kinondoni, Ilala, Temeke na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam kama wadau muhimu ili waweze kuijadili taarifa hiyo. Baada ya uchambuzi na kujumuisha maoni ya wadau yanayotokana na taarifa hiyo, mapendekezo yalipelekwa kwa Waziri Mkuu kwa maamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na maelezo hayo naomba kuchukua nafasi hii kuishukuru Kamati ya Ndugu Mmari, kwa kazi nzuri waliyoifanya ambayo itasaidia katika kutoa mwelekeo wa huduma katika Halmashauri za Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshauri Mheshimiwa Mbunge awe na subira wakati Serikali inaendelea kuifanyia kazi taarifa ya Kamati. (*Makofi*)

MHE. CHARLES N. KEENJA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Kwanza nimhakikishie kwamba sina tatizo na subira.

Mheshimiwa Naibu Spika, imechukua muda mrefu tangu matatizo haya yawepo na yana gharama kubwa sana.

- (a) Je, katika kipindi hiki kilichobaki kabla ya Uchaguzi Mkuu ni hatua gani ambazo Ofisi ya Waziri Mkuu itachukua na ninauliza swali hili nikitambua kwamba swali hili nilimwuuliza Waziri Mkuu?
- (b) Ni kwa nini basi mambo yale ambayo hayahitaji marekebisho ya sheria yasishughulikiwe sasa kiutawala pengine ili kuhakikisha kwamba matatizo haya yanaanza kupunguzwa kabla ya kipindi kijacho cha Bunge?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza hapa kazi iliyofanywa na ile Tume ya Ndugu Mmari ni kazi nzuri sana, ninazo *volumes* pale ni kazi kubwa kidogo. Lakini nataka nithibitisha hapa kwa kusema kwamba Waziri Mkuu ameshaipokea ripoti ile na ina masuala mengine ambayo ndani yake inahitaji pia kupata maoni ya wale wadau wanaohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kusema kwamba hatua ambayo imechukuliwa kwa maana ya kujibu swali lililoulizwa hapa, ni hiyo ya kuhakikisha kwamba Waziri Mkuu amepokea taarifa ile na mimi nilipokuwa natafuta majibu ya swali hili

nilimshirikisha pia Waziri Mkuu akaniambia pia katika hili imebidi kumhusisha pia Mkuu wa Nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kusema hapa kwamba haya yote kwa pamoja ndiyo yanayosubiriwa hapa kwa maana ni jambo linagusa Dar es Salaam, kuuza Dar es Salaam, *Politics* na *Economics* za Nchi hii zinakuwa *determined* na Dar es Salaam. Ukisema unachomoka tu hapa ukasema kwamba utafanya hivi ni tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, anasema yapo yale mambo ambayo hayahitaji Sheria ambayo yanatakiwa kufanyiwa kazi. Mara kwa mara tunakutana na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam na tunakutana na Manispaa hizi na Waheshimiwa mnauliza maswali hapa mara kwa mara, mitaro wakati mwingine inaonekana haifanyi kazi, watu wanatupa takataka ovyo kule, haya hayahitaji kumngoja Waziri Mkuu wala kumngoja Mheshimiwa Rais kwa sababu ni mambo ambayo yapo katika utaratibu mzima wa utendaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nataka nikuthibitishie hapa na Bunge lako lote kwamba kazi hii inafanyika na mimi nataka niseme kwamba kazi inayofanywa ofisi ya Waziri Mkuu kwa maoni yangu ni kazi nzuri na ninahakika kwamba itaendelea kufanyika, ninyi mtusaidie sasa kupitisha bajeti yake, ikishapita hapa tukafanye kazi tumalize. (*Makofi/Kicheko*)

MHE. BENSON M. MPESYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi, naomba niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi hapa ni kwamba inaonekana kwamba hatuna Muundo Maalum unaoweza kusema Jiji linaundwa na Manispaa au manispaa ngapi zitengeneze Jiji. Ndiyo maana unaona Dar es Salaam kuna Manispaa lakini katika Majiji kama Tanga na Mbeya hakuna vitu kama hivyo. (*Makofi*)

Serikali inaweza kutueleza hapa ili kuwe na Jiji inatakiwa liwe na muundo gani? Maana yake kila jambo lipo tofauti sana, ni muundo upi unaopendekezwa na Serikali?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, Hakuna muundo maalum hapa ambao unaweza ukasema sasa huu ni *static* ukikaa hivi unabaki huo huo, muundo huu ni mchakato, akina Deotrephe Mmari mle ndani wanakuja na mawazo kuhusu namna ya kuli-*manage* Jiji la Dar es Salaam.

Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mpesya kwamba hata yale Majiji mengine ambayo anayatamka hapa kwa mfano Jiji la Mwanza, Jiji la Mbeya, Jiji la Tanga nayo tunayatazama katika mchakato huu kuangalia kwamba ni namna gani nzuri ambayo inaweza ikatusaidia katika ku-*manage* Majiji haya ili huduma nzuri iweze kutolewa kwa watu wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo hatuna muundo maalum ambao unaweza ukatoka leo na kesho unaona kwamba haukufai ukauacha, kwa kweli hakuna muundo maalum kama anavyosema yeye mwenyewe nakubaliana naye.

Na. 47

Serikali Kuajiri kwa Mikataba Mifupi

MHE. MUSSA A. ZUNGU aliuliza:-

Katika mfumo wa sasa ajira ya kudumu na pensheni kunawafanya watumishi kutowajibika vizuri na baadhi yao kukosa tija kwenye maeneo ya kazi na hivyo kukosekana ajira wahitimu wengi toka Vyuo vya Juu:-

Je, Serikali sasa ipo tayari kuajiri kwa mkataba wa muda mfupi na hivyo kufungua milango ya ajira kwa wahitimu wanaomaliza elimu ya vyuo wanaokosa ajira?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS MENENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge wa Jimbo la Ilala, napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ajira Serikalini hutawaliwa na masharti mbalimbali ambayo ni masharti ya kudumu na malipo ya uzeeni, masharti ya kawaida (*Operational Service*) na yale ya mkataba wa muda maalum. Ajira chini ya masharti haya hutegemea aina ya kazi, sifa weledi uzoefu na kuwepo kwa nafasi ya ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na masharti haya, msingi mkubwa wa ajira Serikalini ni ule wa masharti ya kudumu ambayo lengo lake kubwa ni kuufanya Utumishi wa Umma kuwa endelevu, kwa kuwa na watalaamu wanaoweza kurithishwa madaraka na kumudu majukumu ya kutekeleza kazi mbalimbali za Serikali kwa nyakati tofauti na kwa kulingana na mahitaji ya Serikali.

Hata hivyo, inapotokea kuwa kuna umuhimu wa kuajiri watumishi kwa mikataba ya muda maalum, Serikali hufanya hivyo ili kutekeleza kazi zinazojitokeza ambazo zinahitaji utaalum maalum. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge wa Jimbo la Ilala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wakati huu Serikali haina nia ya kuajiri wahitimu wa vyuo vikuu kwa masharti ya mkataba kujaza nafasi zinazohitaji ajira ya masharti ya kudumu kwa sababu utaratibu huo hautaiwezesha Serikali kuwa na watumishi wenye

sifa, uzoefu na weledi unaotakiwa kutekeleza majukumu yake na kuweza kurithishana madaraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ieleweke kwamba ajira ya mkataba si suluhisho la tatizo la ajira kwa watalaam wa vyuo vikuu kwa vile ajira ya mkataba ni ya kipindi maalum na baada ya kipindi hicho mhusika hatakuwa na kazi. Suluhisho la kudumu la tatizo la ajira ni kubuni na kutekeleza sera za uwekezaji na kuweka mazingira mazuri yatakatayovutia uwekezaji katika sekta ya kilimo, viwanda na utoaji wa huduma. Pamoja na hatua hizi ni muhimu kwa wahitimu wa vyuo vikuu kubadilika kifika ili waweze kujijiri wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la ufanisi na uwajibikaji kwa baadhi ya watumishi ni changamoto inayoikabili jamii yetu na linaendelea kushughulikiwa na Serikali kwa kuhimiza usimamizi na uwajibikaji katika taasisi zetu.

MHE. MUSSA AZZAN ZUNGU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Waziri kwamba yako maeneo ambayo watumishi lazima wawe wanaajiriwa kwa muda mrefu mathalani walimu, waganga na wauguzi.

Mimi nimetoa ushauri na kwa majibu ya Waziri alivyosema Serikali haina nia ina maana ushauri huu wameukataa kitu ambacho wangekwenda kukifanyia kazi. Yako maeneo ya watalaam wa fedha, uchumi, mipango na manunuzi ambao utendaji wao ni mbovu na matokea yake huhamishwa eneo moja mpaka eneo lingine kutokana na utendaji mbovu.

Je, Serikali inasema nini kuhusu watalaam kama hawa au Je, Serikali inasema nini au ni nini inafikiria kwa maeneo mengine kama haya ili iweze kuwapa ajira na ili waweze kuwa na ufanuzi mzuri na uwajibikaji na kuheshimu wananchi ambao kwa sasa hivi hawawatendei haki?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwamba Serikali sasa hivi haina utaratibu wa kuajiri watumishi kwa muda maalum au kwa mikataba na kama alivyosema yeye mwenyewe mtumishi mbovu hata ukimwajiri kwa mkataba haina maana kwamba utaweza kuboresha utendaji wake. Kimsingi kinachotakiwa wale watumishi wabovu wachukuliwe hatua ikiwezekana waondolewe katika utumishi wa umma ili waweze kuingizwa watumishi wengine ambao watafanya kazi kwa ufanisi. (*Makofi*)

MHE. ALOYCE B. KIMARO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali imekiri mara kwa mara pamoja na Waziri kwamba wako wafanyakazi hewa. Lakini hatujasikia hatua zinazochukuliwa kwa wale waliowaajiri ama wanaotumia hizi fedha za wafanyakazi hewa. Je, Serikali inaweza kutoa jibu hapa Bungeni kwamba wamechukuliwa hatua gani na ni watu gani hao?

NAIBU SPIKA: Jamani hamfuati swali la msingi. Huyu alitaka ubadilishwe mfumo wa ajira kuliko huu wa kuendelea uwe na *contract system*, sasa mambo ya wafanyakazi hewa. Haya Mheshimiwa Waziri jibu kwa sababu unawafahamu sana hawa wafanyakazi hewa.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge amesema kwamba hajasikia hatua zozote tunazozichukua kushughulikia watumishi hewa. Ni kweli tumefanya uhakiki katika sekta ya Afya, tumefanya uhakiki katika sekta ya Elimu na tumekuta watumishi hewa na tulikabidhi katika vyombo vya sheria ili kuweza kufanya uchunguzi kujua ni akina nani hasa ambao wamehusika katika kusababisha fedha za Serikali kupotea. Napenda nimhakikishie kwamba muda si mrefu atazisikia hatua ambazo tutazichukua.

MHE. DR. ANTHONY M. DIALLO: Mheshimiwa Naibu Spika, katika awamu ya tatu Serikali ilikopa zaidi ya bilioni 100 za Kitanzania kutoka *World Bank* kwa ajili ya *Civil Service Reform*. Katika mapendekezo makubwa ya *Civil Service Reform* ilikuwa kwamba ajira ziwe zinatolewa kwa mikataba. Sasa inavyoonekana ni kwamba hilo deni pamoja na nia ambayo ilikuwepo hapo awali sasa hivi imeachwa. Je, Serikali inaweza kutuambia nini kwamba hizo fedha zilizokopwa kwa ajili ya kufanya hiyo shughuli zilipotea bure?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali ya Awamu ya Tatu na hata ya nne imepata fedha kutoka Benki ya Dunia na wafadhili mbalimbali katika kushughulikia masuala ya mabadiliko katika utumishi wa umma. Lakini hizo hazikuwa na madhumuni ya kubadilisha utumishi wa umma kuwa wa mkataba badala yake ilikuwa ni kuboresha mifumo, sera, sheria na kuhimiza uwajibikaji wa watumishi ili waweze kuwatendea haki wananchi na kutoa huduma bora, suala ambalo ndilo ambalo linaendelea katika utumishi wa umma.

Na. 48

Maslahi ya Watumishi wa Serikali

MHE. GEORGE M. LUBELEJE (K.n.y. MHE. JOB Y. NDUGAI) aliuliza:-

Mara kadhaa, wafanyakazi wa Umma hapa nchini wametishia kugoma kwa madai ya mishahara midogo sana. Pia posho na marupurupu yao ikilinganishwa na kiasi cha kodi kubwa wanayokatwa:-

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mbunge wa Kongwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikiongeza mishahara ya watumishi kila mwaka kwa kadri ya ukuaji wa uchumi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita yaani 2005/2006 hadi 2009/2010, kima cha chini cha mishahara kimeongezeka kwa asilimia 61 kutoka shilingi 65000 hadi shilingi 104,410 kwa mwezi. Wastani wa mishahara umeongezeka kwa asilimia 108.22 kutoka shilingi 152,848 hadi shilingi 318,261 kwa mwezi. Aidha, Bajeti ya mishahara ya watumishi imeongezeka kwa asilimia 160.29 kutoka shilingi bilioni 681,900 mwaka 2005/2006 hadi shilingi trilioni 1,77,891 mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuongeza mishahara kwa kiwango hiki Serikali pia imekuwa ikirekebisha kiwango cha chini cha kodi ya mapato ili kumpa unafuu wa kodi mtumishi ambapo katika kipindi cha mwaka 2005/2006 hadi 2009/2010 kima cha chini cha kulipa kodi ya mapato kilirekebishwa kutoka shilingi 65,000 hadi shilingi 104,410 kwa mwezi.

Aidha, kiwango cha chini cha kodi ya mapato kimeshuka kwa asilimia 18 mwaka 2005/2006 hadi asilimia 14 mwaka 2010/2011 hivyo kuongeza kipato halisi cha wafanyakazi.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa majadiliano kati ya *TUCTA* na Serikali yalikuwa yanaendelea. Nataka kujua. Je, majadiliano hayo yamemalizika na kama yamemalizika, ni nini makubaliano kati ya Serikali na *TUCTA*?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali ilikuwa na majadiliano ya pamoja na vyama vya wafanyakazi ambapo majadiliano yetu yalikalimika tarehe 8 Mei, 2010 na katika makubaliano hayo kwanza tulikubaliana kumteua *regulator* na iwe imekamilika kabla ya mwezi wa Septemba.

Pia, tulikubaliana kupunguza kiwango cha ukataji kodi kwa kima cha chini cha mishahara kutoka asilimia 15 hadi 14 na pia tulikubaliana kiasi cha kima cha chini cha mishahara.

NAIBU SPIKA: Anasema walichokubaliana kima cha mishahara maana atasema kwenye hotuba yake.

MHE. LUCAS L. SELELII: Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwa mambo ambayo wafanyakazi wanalalamikia ikiongozwa na *TUCTA* ni pamoja na mishahara, kodi na hasa mafao ya uzeeni ukizingatia ule mfuko wa *PPF* hapa Waziri anasemaje?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma si ameongea?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Naibu Spika, katika majadiliano yetu mojawapo lilikuwa ni suala la kupishana kwa mafao yaliyotolewa na mifuko mbalimbali ndiyo maana tukakubaliana kumchagua *regulator* kwa maana kwamba Serikali imeanzisha chombo ambacho kitakuwa kinahakikisha kwamba mifuko hiyo inatoa mafao yanayolingana.

Kwa hiyo, kwa kumteua *regulator* pamoja na majadiliano mengine ambayo yanaendelea napenda nimhakikishie kwamba suala hili na lenyewe litakuwa limeisha.

MHE. ISMAIL JUSSA LADHU: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa malalamiko ya wafanyakazi hayahusu tu madai ya kutaka tu kuongezewa mishahara na posho bali pia wanazungumzia tofauti kubwa sana baina ya mishahara na posho zao na ile ya viongozi wa kisiasa, Serikali haifikirii kwamba kuna haja ya kupunguza mishahara na marupurupu ya viongozi wa kisiasa kama Mawaziri na Wabunge ilikaribiane kama ilivyofanyika katika Uingereza hivi karibuni? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Jussa uanze kupunguza wa kwako kwa kweli. (*Kicheko*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ismail anapendekeza kwamba tupunguze mishahara ya viongozi wa kisiasa ili tuongeze mishahara ya watumishi wa umma. Napenda kumweleza kwamba watumishi wa umma wanakaribia 400,000. Wabunge ni kama 320.

Pia wale wanaolipwa kima chini ni wengi zaidi kuliko hata wale wanaolipwa mishahara ya juu kwa hiyo, hata tukichukua mishahara yote ya Wabunge tukisema tuongezee kwa watumishi wa umma haiwezi kuongezeka hata asilimia 1. Kwa hiyo, si suluhisho kwa mishahara ya watumishi wa umma kwa kupunguza mishahara ya viongozi wa kisiasa. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Lakini ukweli ni kwamba kila watu wana masharti yao. Ndiyo ukweli wenyewe.

Na. 49

Ubovu wa Barabara Nchini

MHE. SAID AMOUR ARFI aliuliza:-

Kwa kuwa barabara nyingi katika miji yetu zipo katika hali mbaya sana ukiwemo Mji wa Mpanda na kwa kuwa fedha zinazotolewa na Mfuko wa Barabara hazitoshelezi na kwa kuwa, Halmashauri nyingi hazina vyanzo vizuri vya mapato:-

(a)Je, Serikali iko tayari kusaidia kwa kutoa fedha za ziada kufidia pengo lililopo kati ya mahitaji halisi ya fedha inayotolewa na Mfuko wa Barabara?

(b)Je, Serikali iko tayari kutenga fedha maalum kwa ajili ya ujenzi wa mifereji ya maji ya mvua mjini ili barabara hizo zidumu na kupunguza matengenezo ya mara kwa mara?

NAIBU SPIKA: Jamani haya basi hawajapunguza mishahara yenu, mnyamaze tuendelee na kazi. (*Kicheko*)

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Arfi, Mbunge wa Mpanda kati, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali kupitia Wizara yangu imekuwa ikisaidia ujenzi wa barabara za miji mbalimbali pale Bajeti inaporuhusu. Kutokana na ufinyu wa Bajeti ya Serikali, hakuna fedha za ziada zilizotengwa kufidia pengo hilo.

Hata hivyo, kutokana na ukweli kuwa fedha za mfuko wa barabara zimeongezeka kutokana na ukweli kuwa fedha za Mfuko wa Barabara zimeongezeka kutoka shilingi bilioni 101.2 mwaka 2006/2007 hadi kufikia shilingi bilioni 288.2 mwaka huu wa fedha 2009/2010, Halmashauri na Manispaa zimeongezewa mgao karibu mara mbili ya mgao wa zamani.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, ili kusaidia Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda katika kuboresha barabara za mji, Wizara yangu katika mwaka wa fedha 2009/2010 ilitenga jumla ya shilingi milioni 180 kwa ajili ya kujenga barabara za mji wa Mpanda kwa kiwango cha lami, hii ikia ni pamoja na ujenzi wa mifereji.

Aidha, Wizara yangu inaendelea kutenga fedha kulingana na uwezo wa Serikali.

MHE. SAID AMOUR ARFI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali kwa niaba ya wananchi na wakazi wa Mji wa Mpanda napenda kuishukuru sana Serikali kwa jitihada za kuboresha barabara za Mji wa Mpanda.

Lakini ukweli unabakia palepale kwamba fedha inayopatikana kupitia Mfuko wa Barabara haitoshelezi kutokana na mahitaji halisi ya halmashauri zetu.

Je, sasa Serikali inaweza kutusaidia Halmashauri ya Mji wa Mpanda ili tuweze kuimarisha mifereji katika maeneo ya mji wa zamani na makanyagio kama ombi maalum?

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Arfi, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumetambua changamoto iliyo katika mji wa Mpanda na ndiyo maana Serikali ilitenga pesa jumla ya shilingi bilioni 1,547,000,000/= kwa ajili ya kujenga barabara saba (7) katika Mji wa Mpanda ambao ujenzi wake ulianza Januari, 2009 na umekamilika mwezi Aprili, 2010.

Pia mwaka huu wa fedha tulitenga shilingi milioni 180 kwa ajili ya ujenzi wa mifereji. Nafahamu bado kuna changamoto ya ujenzi wa mifereji katika Mji wa Mpanda, tutaendelea kujitahidi kuwaunga mkono Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda ili tuweze kuboresha ujenzi wa mifereji katika mji huo.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Sambamba na swali la msingi pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, pia katika Halmashauri ya Wilaya ya Iramba kuna barabara inayounganisha kutoka Kiomboi kwenda Misigiri ambayo hutengewa Bajeti ya kilomita tano(5) kila mwaka.

Barabara hiyo sasa imechukua miaka mitatu bado hazijakamilika na zimebaki kama kilomita 10 hivi. Sasa wakati wanatengeneza nyingine zinaharibika na nyingine hazijamalizwa.

Je, Waziri ataungana na mimi kwamba mwaka huu atenge fedha za kumaliza barabara ile? Ahsante!

NAIBU SPIKA: Mbona siyo swali la nyongeza la msingi? Swali la msingi ni barabara ya kule sasa ukiuliza maalum Waziri hawezi kukujibu sahihi. Lakini Waziri ujibu hilo swali kama unazo hela za kusambaza, haya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu.

WAZIRI WA MAENDELEO MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ridhaa yako naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mlata, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi la Mheshimiwa Mbunge tumelisikia na tatalizingatia katika mchakato wa Bajeti hii ya mwaka 2010/2011 na ikishindikana tutaangalia katika Bajeti zinazofuata. (*Makofi*)

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Serikali ya awamu ya nne haina aibu kwa barabara ya uhuru ya Dar es Salaam, barabara yenye historia kubwa katika nchi hii

kuiacha kuwa na mashimo na mahandaki katikati ya Jiji la Dar es Salaam na kuyaacha magari na wananchi wakihangaika?

NAIBU SPIKA : Jamani Waheshimiwa Wabunge sasa mnaenda *off line*, kwa sababu hiki ni kitu kipya kabisa mtegemee Waziri ajibu? Lakini kwa sababu yeye anajua barabara zake ajibu tu anavyoona.

WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu sana umuhimu wa barabara hii ya uhuru katika Jiji la Dar es Salaam na tumeshaanza kuifanyia kazi na katika mwaka ujao wa fedha tumeitengea pesa kwa ajili ya kuiweka barabara hiyo katika hali nzuri.

Na. 50

Hitaji La Lami Katika Barabara ya Soni-Bumbuli-Dindira

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO aliuliza:-

Barabara ya Soni-Bumbuli-Dinda ni moja kati ya barabara zilizoingizwa katika mpango wa matengenezo ya kudumu kupitia Mkandarasi kwani wakati wa mvua nyingi hususan Aprili na Mei maeneo yenye milima mikali na kona kali ya vijiji vya Dule na Mbelei hupitika kwa tabuu sana.

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka lami kiasi cha mita 400 kila eneo ili kupunguza wasiwasi na adha wanayopata wasafiri katika maeneo hayo?
- (b) Je, Serikali kwa niaba ya wananchi wa maeneo hayo inaweza kutoa shukurani za dhati kwa *Father Selestin* wa Kanisa Katoliki Sakarani- Mbelei kwa kutoa trekta lake mara kwa mara kuvuta magari yanayokwama katika maeneo hayo?

WAZIRI WA MIUNDOMBINU alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hezekia Shellukindo, Mbunge wa Jimbo la Bumbuli, lenye sehemu (a) na (b) kama ifutavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Soni-Bumbuli hadi Dindira ni miongoni mwa barabara zilizo katika mradi wa majaribio wa “*Performance Based Management and Maintenance of Roads (PMMR)*”. Chini ya mpango huu Mkandarasi anawajibika kukarabati na kuitunza barabara kwa kipindi cha miaka mitano (5).

Pendekezo la Mheshimiwa Mbunge la kuweka lami katika baadhi ya sehemu ili kuifanya ipitike bila wasi wasi ni zuri na lingeweza kutekelezwa iwapo uwezo wa Serikali kifedha utaporuhusu.

Kwa sasa Wizara yangu inapenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa Mkandarasi ambaye yupo eneo la mradi ataelekezwa kurekebisha maeneo hayo korofi kwa kiwango cha changarawe ili iweze kupitika majira yote ya mwaka. Pamoja na hayo

Serikali itaangalia uwezekano wa kutenga fedha katika mwaka wa fedha 2011/2012 kwa ajili ya kuweka lami au zege ili kuimarisha maeneo korofi yaliyopo kwenye barabara hiyo.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Serikali napenda kumpongeza *Father Selestin* wa Kanisa Katoliki Skarini- Mbelei, kwa moyo wa kizalendo ambao ameonyesha kwa moyo wa kizalendo ambapo ameonyesha kwa kutoa trekta lake kusaidia kuvuta magari yanayokwama katika baadhi ya maeneo ya barabara hiyo.

Ningependa kutumia fursa hii kutoa wito kwa wananchi wengine pia kuiga mfano huo mzuri wa *Father Selestin* kwa kuwa na moyo wa kujitolea kuwasaidia wenzao wapatapo matatizo.

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri nina maswali madogo mawili ya nyongeza. Kwa kuwa eneo hilo lenye kona na miteremko mikali limefanyiwa ukarabati kidogo,

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Laizer unapita kati ya anae sema na mimi. (*Makofi*)

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Je, Waziri ataweza kumwelekeza Mkandarasi kwamba asiweke changarawe kwenye barabara hiyo sehemu ya kupita tairi tu ingekuwa eneo lote lisambazwe liwekwe lami au iweke changarawe kwa sasa hivi kama alivyoshauri Mheshimiwa Waziri?

Pili, katika barabara hiyo, Waziri atakubaliana na mimi kwamba kuna eneo la kilomita kama nane (8) hivi changarawe zilizowekwa zilikuwa zina vumbi kwa hiyo, kuna matope mengi ya kilomita kama 8 kutoka sehemu ya Dule kwenda sehemu ya Luhangala.

Je, atamwelekeza airekebishe maanake ipo katika wakati wa matengenezo yaliyokubaliwa?

WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza ni kuhusu kumwelekeza Mkandarasi ili aweze kuweka changarawe zaidi kuliko kuweka tu kwenye maeneo yale ambayo matairi yanapita. Wazo hilo tumelipokea nitawaelekeza wataalam ili waweze kulifuatilia kwa karibu Mkandarasi huyu afanye kazi ambayo ni bora zaidi kuliko ambavyo ana fanya hivi sasa.

Kwa upande wa kipande kile cha Dule mpaka Luhangala, kilomita nane (8) ambalo changarawe yake sio nzuri ni vumbi, pia tutalizingatia na kuweza kumwelekeza Mkandarasi ipasavyo kama vile ambavyo Mheshimiwa Mbunge amependekeza.

MHE. DR. SAMSON F. MPANDA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona. Matatizo yaliyoko Bumbuli yako sawa sawa na yale yalioko Jimboni kwangu Kilwa Kaskazini, katika barabara ya Ndundu - Somanga hasa upande wa Malendego kwenda Muhoro pale Wakandarasi wanafanya vya ajabu kabisa. Wanatoza au

wanawaambia watu walipie mafuta kwa ajili ya kuvuta gari. Je, adha hii itaisha lini?

WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nasikitika sana kwa shida ambayo wananchi wameipata katika harakati za ujenzi wa barabara hiyo kutoka Ndundu hadi Somanga. Habari njema ni kwamba kipindi hiki sasa cha mvua ambacho kilileta adha kubwa sana kwa wananchi kwenye barabara hiyo kipindi cha matengenezo, kipindi hiki sasa kimeisha. Sasa tunaingia sasa mwezi wa sita ambao ni mwezi mvua zimekatika, zimemalizika nitamwelekeza Mkandarasi ahakikishe kwamba barabara ya Mchepuo ile ameitengeneza vizuri na kwa vile hakuna mvua bila shaka sasa hivi kutakuwa hakuna kukwama tena.

MHE. LUCY T. MAYENGA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa sheria iliyopo hivi sasa hairuhusu Halmashauri zetu kukopa. Je, Serikali kwa kuwa kuna matatizo mengi ya miundombinu mibovu katika ngazi ya Halmashauri na ngazi ya Mkoa. Serikali haioni kwamba kuna umuhimu sasa wa kujenga uwezo kwenye Halmashauri ili hatimaye kuziruhusu kukopa kwa kutumia *Infrastructure Bonds*, (Hati Fungani) za miundombinu ili walau kuweza kupata uwezo wa kukopa ambao unatumia muda mrefu kati ya miaka kumi na tano hadi ishirini kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu hii?

WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua changamoto zilizopo za ujenzi wa miundombinu ya barabara katika Halmashauri zetu kwa nchi nzima, Serikali sasa hivi ipo katika mkakati wa kuasisi mfuko wa miundombinu kupitia *Infrastructure Bonds* na wakati huo huo kutafuta njia ambazo zitaongeza fedha katika mfuko wa barabara. Taratibu hizi na mchakato huu utasimamiwa kwa ukamilifu ili kuhakikisha kwamba tunakuwa na pesa nyingi zaidi kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya barabara nchini mwetu, wazo la Mheshimiwa Lucy Mahenga tutalizingatia, tutaangalia namna jinsi tutaweza kulitekeleza.

Na. 51

Mipango ya Uendelezaji Kanda za Maendeleo ya Kaskazini

MHE. MBARUK K. MWANDORO aliuliza:-

Kwa kuwa, mipango ya uendelezaji wa kanda ya maendeleo ya Kaskazini (*Northern Development Corridor*) ikiwemo Bandari mpya ya Tanga, Reli ya Tanga-Musoma na uwekezaji mkubwa katika viwanda, kilimo na kwa kuwa muda mrefu umepita bila kuwepo dalili za mipango halisi ya utekelezaji na badala yake kuwepo dalili za kuvunja Reli ya Tanga-Arusha na Ruvu- Mnyuzi na hivyo kuanza kukatisha tama wananchi.

- (a) Je, Serikali imefikia wapi katika azma yake ya kujenga Bandari ya Mwambani, Tanga pamoja na Reli ya Tanga hadi Musoma?

- (b) Je, Serikali imefikia hatua gani katika azma ya uwekezaji mkubwa katika sekta za viwanda, vikiwemo vya EPZ, kilimo na madini pamoja na mradi wa magadi soda?
- (c) Je, Serikali inasema nini kuhusu au kuimarisha reli ya Tanga-Arusha pamoja na kiungo cha Ruvu-Mnyuzi?

WAZIRI WA MIUNDOMBINU alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbaruk Kassim Mwandoro, Mbunge wa Mkinga, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo.

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, azma ya Serikali ya kujenga Bandari ya Mwambani, Tanga pamoja na Reli ya kutoka Tanga hadi Musoma, bado ipo na mpango wa ujenzi wake ni moja ya miradi iliyomo kwenye mpango kabambe wa Reli ya Afrika Mashariki (*East Africa Railways Master Plan*). Pamoja na mpango wa uwekezaji wa sekta ya uchukuzi wa Wizara wa Miundombinu.

Aidha, mpango huo kwa sasa unahusisha ujenzi wa Reli kutoka Bandari ya Mwambani, Tanga hadi kwenda Bandari mpya ya Kampala nchini Uganda ambayo imependekezwa kujengwa.

Hivi sasa, Serikali inatafuta wawekezaji ambao watakuwa tayari kushirikiana katika kufanya upembuzi yakinifu pamoja na usanifu wa mradi na hatimaye ujenzi wake. Serikali za Tanzania na Uganda zitashirikiana katika mchakato wa ujenzi wa Reli hiyo ya kuanzia Tanga-Musoma.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza azma ya Serikali ya uwekezaji mkubwa katika sekta za viwanda, vikiwemo vya EPZ, kilimo na madini pamoja na mradi wa magadi soda, Serikali kupitia Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa kushirikiana na uongozi wa Mkoa wa Tanga imebainisha eneo la EPZ lenye jumla ya hekta 1,363 katika kitongoji cha Neema, Kata ya Tangasisi katika Manispaa ya Tanga.

Eneo hili lipo karibu sana na eneo litakalojengwa Bandari mpya ya Mwambani. Upimaji wa awali umekamilika na zoezi la uthamini wa mali ipo katika hatua za mwisho. Baada ya zoezi hilo la uthamini, Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi wataanza uendelezaji wa Miundombinu katika eneo hilo na hatimaye kuhamasisha wawekezaji.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Reli ya Tanga-Arusha haitavunjwa bali itaimarishwa chini ya mradi wa Reli na Bandari kutoka Tanga-Arusha-Musoma hadi Kampala nchini Uganda kama ilivyoelezwa katika jibu la sehemu (a) la swali hili. (*Makofi*)

MHE. MBARUK MWANDORO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri ambayo yameleta shahuku kubwa kwa wananchi

hasa kwa kuzingatia maendeleo yalipo sasa hivi na kutazamia kuanzishwa kwa soko la pamoja la Afrika Mashariki.

Kwa kuwa masuala haya yamekuwa ya muda mrefu sana, Mheshimiwa Waziri anaweza kueleza ni lini hasa huo usanifu na uchambuzi yakinifu utafanyika ili shughuli hizi zifanyike zilizokwama kwa muda mrefu?

WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli mchakato huu umechukua muda lakini kwa sababu nchi mbili zinahusika taratibu mbalimbali zimefuatwa na mwaka huu 2010, Serikali mbili hizi za Uganda na Tanzania zimefanyika majadiliano kwa ajili ya kuharakisha mchakato wa ujenzi, uimarishaji wa Reli ya Tanga-Moshi-Arusha na ujenzi mpya wa kutoka Arusha–Musoma.

Tunatarajia kwamba kwa juhudi mpya hizi za Serikali mbili bila shaka kazi hii itaenda kwa haraka zaidi. Nasikitika sitoweza kusema tarehe gani tutaanza kufanya usanifu katika Reli hii lakini mara tu tutakapofahamu ratibu kamili tutalijulisha Bunge lako Tukufu.

Na. 52

Bei Nzuri Kwa Zao La Pareto

MHE. MARTHA J. UMBULLA aliuliza:-

Kwa kuwa zao la pareto ni moja ya mazao ya biashara yanayoweza kuongeza pato la Taifa na kwa kuwa zao hilo hustawi sana Mkoani Manyara hususan Jimbo la Babati Vijijini na kwa kuwa Serikali ilikiri kuhamasisha kilimo cha mazao ya biashara ili kuongeza pato la Taifa.

Je, kwa nini Serikali isiweke bei nzuri kwa zao la pareto ili wakulima wengi wahamasike kupanua kilimo cha zao hilo?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, kama ifuatavyo.

Nakubaliana na ukweli kwamba pareto ni mojawapo ya mazao ya biashara na linaloweza kuongeza pato la Taifa kama yalivyo mazao mengine. Kutokana na sababu hiyo, Serikali kupitia Bodi ya Pareto imekuwa ikihamasisha uzalishaji wa zao hilo. Uhamasishaji huo unafanyika katika mikoa ya Mbeya, Iringa, Arusha, Manyara na Kilimanjaro, linakolimwa zao hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Serikali kuhakikisha kuwa bei ya pareto inawavutia wakulima wengi kulima zao hilo, mkutano wa wadau uliofanyika tarehe 2 Julai, 2009 jijini Mbeya ambapo wakulima na wanunuzi wa pareto walishiriki, wadau

hao walikubaliana kuongeza bei ya pareto kutoka shilingi 700 kwa kilo msimu 2008/2009 hadi shilingi 1,000 kwa kilo msimu 2009/2010 kwa pareto daraja la chini na yenye sumu ya wastani wa asilimia 1.3. Aidha, bei ya daraja la kwanza yenye sumu ya wasatani wa asilimia 1.7 iliongezeka kutoka shilingi 1,500 kwa kilo msimu 2008/2009 hadi shilingi 1,700 msimu 2009/2010. Kutokana na mabadiliko hayo ya bei, tathmini iliyofanyika na Bodi ya Pareto ilionyesha kuwa hadi tarehe 31 Machi, 2010 zaidi ya asilimia 80 ya wakulima wa pareto walilipwa wastani wa shilingi 1,200 kwa kilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali (Kupitia Bodi ya Pareto) imepanga kuitisha kikao kingine cha wadau wa zao la pareto ambapo pamoja na mambo mengine, suala la bei ya pareto litajadiliwa.

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa zao la pareto linatumika kutengeneza dawa ya kuulia wadudu kama vile mbu na wadudu wengine warukao na kwa kuwa katika maduka mengi hapa Tanzania yamesheheni makopo ya kuulia wadudu kutoka nchi za nje na nchi jirani. Je sambamba na uboreshaji wa kilimo cha zao hilo, pamoja na kuweka bei nzuri, ni kwa nini Serikali pia isianzisha kiwanda cha kutengeneza madawa ya kuulia wadudu kwa kutumia pareto ili kilimo hicho kiweze kuwa na tija zaidi?

(b) Kwa kuwa wakulima wengi hasa Mkoani Manyara wameitikia kilimo cha pareto na azma ya Serikali ya Kilimo Kwanza na kwa ajili hiyo kuna matarajio makubwa ya kuvuna mazao mengi katika msimu huu. Je, sambamba na azma hiyo, Serikali imejiandaa vipi kuhakikisha kwamba *spirit* hiyo ya Kilimo Kwanza kwa wakulima wadogo inaenda sambamba na kuhifadhi mazao ili azma ya Serikali ya Kilimo Kwanza iwe endelevu?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Ni kweli kabisa kuna biashara nyingi ya madawa ya kuuliawadudu ambayo yanatoka nje ya nchi lakini pia ni ukweli kwamba Mheshimiwa Umbulla aelewe kwamba Serikali haifanyi biashara. Kwa hiyo, tunachokifanya kusema kweli ni kushauri na kuhamasisha wafanya biashara waweze kuanzisha viwanda vya kuulia wadudu na kutumia pareto yetu ambayo tunaizalisha hapa nchini nchini.

Katika Kilimo Kwanza tunahamasisha vipi uhifadhi. Niseme tu kwamba kwanza Serikali inatoa ruzuku ya pembejeo mbalimbali ili tuweze kuongeza uzalishaji wa chakula ili tuweze kupata chakula kingi kwa ajili ya matumizi ya humu ndani ya nchi pamoja na kuuza nje ya nchi. Lakini suala la uhifadhi linaanzia kwenye kaya. Kwa hiyo, kila kaya inatakiwa ihakikishe kwamba chakula kile kinahifadhiwa ili tuweze kupata chakula cha kutosha mpaka tuingie kwenye msimu mwingine. Lakini niseme kwamba sisi kama Serikali chakula ambacho tunakinunua kusema kweli ni chakula ambacho tunakinunua kwa kiasi kidogo sana, *limit* yetu ni tani 150 kwa mwaka kwa ajili ya kutusaidia kwa dharura kwa miezi miwili, mitatu wakati wa matatizo. Kwa hiyo, suala

la uhifadhi kusema kweli inaanza kwenye ngazi ya kaya, kila kaya ihakikishe kwamba inahifadhi chakula.

NAIBU SPIKA: Kutokana na muda tunaendelea na swali linalofuata, nina dakika tano tu.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Naibu Spika, nitajibu kwa haraka ili kwenda na muda wako. Kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Martha Umbulla na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Namna moja ya kuhimiza kilimo kwanza na utekelezaji wake ni kuanzisha viwanda vingi ambavyo vitasindika mazao ya kilimo ikiwemo pareto. Kwa hivyo, sisi tutawahamasisha wafanyabiashara, lakini ningependa kuwahimiza wakulima wa Mkoa wa Manyara, Mkoa wa Iringa hata Mkoa wa Kilimanjaro kupanda pareto zaidi ili waweze kuvutia wawekezaji katika kuanzisha viwanda vya kusindika pareto.

Na. 53

Wakulima Kujua Gharama za Kuzalisha Mazao yao

MHE. DKT. CHRISANT M. MZINDAKAYA aliuliza:-

Je, kwa nini Serikali imeshindwa kusaidia kuwa na mfumo unaowasaidia wakulima kujua gharama ya uzalishaji wa mazao yao ili bei wanayouzia mazao hayo iwe na tija?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Chrisant Majiyatanga Mzindakaya, Mbunge wa Kwela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Kilimo inao mfumo wa kuwasaidia wakulima kujua gharama za uzalishaji wa mazao kwa kutumia teknolojia mbalimbali zinazoshauriwa na watafiti kutumika.

Mtiririko wa mfumo huu huanzia kwenye vituo na kanda za utafiti wa kilimo, ambapo teknolojia zinazozalishwa hupendekezwa kutumika na wadau ikiwa ni pamoja na kuainisha gharama zake.

Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika inacho kitengo unganishi cha habari ugani na utafiti wa kilimo kwenye kila kanda ya utafiti. Kitengo hicho kina wataalamu wakuu wa utafiti, habari na ugani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi kubwa ya kitengo hicho ni kuhakikisha kuwa, teknolojia zinawafikia wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na taarifa kuhusu gharama za teknolojia mbalimbali zinazotolewa na watafiti kwa ajili ya kutumika na wakulima. Kiungo muhimu sana kwenye mfumo huu ni Afisa Kilimo na Mifugo wa Wilaya ambaye

hupeleka taarifa hizo kwenye ngazi ya Kata na kuhakikisha kuwa zinafika kwa wakulima vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ngazi ya kijiji, wakulima hufundishwa na wataalamu wa ugani kuhusu utumiaji wa teknolojia mbalimbali kwa mfumo wa mashamba darasa na vikundi. Mafunzo hayo hujumuisha taarifa kuhusu gharama za uzalishaji. Kwa mfano, katika mwaka 2009/2010 wakulima wa mahindi katika Nyanda za Juu Kusini, waliofuata kilimo bora cha mbegu za kisasa na kutumia mbolea za viwandani kikamilifu, walipata faida ya wastani wa Sh. 1,034,200 kwa hekta na wale waliotumia mbegu bora lakini wakaweka mbolea nusu ya kiwango walichoshauriwa walipata faida ya Sh. 201,500 na wakulima ambao hawakupanda mbegu bora na hawakutumia mbolea ya viwandani walipata hasara ya Sh. 43,550. Mifano kama hii kwa mazao mengine ipo mingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kukiri kuwa, pamoja na kuwepo mfumo wa taarifa za gharama za uzalishaji, ipo changamoto ya taarifa hizo kutokuwafikia wakulima wote kutokana na idadi ndogo ya Maofisa Ugani ambapo hadi sasa wapo wagani 4,437 tu, ikilinganishwa na mahitaji ya Maofisa Ugani 15,082.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu inakabiliana na changamoto hii kwa kuwafunza wagani wapya. Kwa mfano, mwaka huu, ifikapo Novemba 2010, tunatarajia wagani 2,743 watahitimu katika Vyuo vyetu tayari kwa ajira. Mkakati huu wa kuwapata wagani wapya, utaendelea mpaka kufikia lengo la kupata mgani mmoja kwa kila Kata kwa kuanzia na baadaye mmoja kwa kila kijiji.

MHE. DKT. CHRISANT M. MZINDAKAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri amesema kwamba, wakulima wa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, walipata faida ya shilingi 1,034,200. Nataka atuambie hawa wakulima ni wangapi?

Swali la pili, kwa kuwa sasa hivi kuna teknolojia na upelekaji wa taarifa kwa wananchi ni rahisi kuliko zamani; sasa hawaoni kwamba wangeanzisha utaratibu wa kutangaza angalau kwa wastani bei na gharama za mkulima ili wakulima nao waweze kufanya kazi kwa kujua gharama zao za kilimo?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tunavyofanya *research* tunafanya *sampling*. Kwa hiyo, siyo rahisi kuelezea *population* au wingi wa watu ambao walipata faida ya shilingi elfu moja.

La pili, kuhusiana na suala la gharama, nimesema tuna vitengo unganishi kwenye Kanda zetu ambavyo vinatoa gharama kwa kuanzia kwenye *inputs*, yaani wanavyoanza kulima mpaka wanavyotumia mbegu pamoja na mbolea, kupalilia na kuvuna. Kazi hii wanaifanya wataalamu wetu wanapeleka kwenye Wilaya, Wilaya nao wanapeleka kwenye Vijiji. Kama nilivyosema kwamba, Maofisa Ugani wetu ni wachache. Suala la bei kama ilivyo, sisi Serikali hatupangi bei; bei inatokana na nguvu ya soko. Kwa hiyo, inategemea tu kwamba, wamevuna kiasi gani kama mavuno ni kidogo basi bei nayo itapanda. *Supply* ni ndogo basi *price* inapanda na pia suala la bei linatokana na wapi

anakouzia. Kama atavuna Sumbawanga lakini akauzia Mbeya ni *obvious* kwamba, suala la usafiri nalo litakuwa limeongeza bei; kwa hiyo, ni rahisi Serikali kupanga bei.

Na. 54

Mradi wa Kupeleka Umeme Vijijini Kupitia MCC

MHE. JAMES P. MUSALIKA (K.n.y. MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA)
aliuliza:-

Mradi wa MCC wa kupeleka umeme kwenye Vijiji vya Karumwa, Ikangala, Nyarubele, Nyijundu, Nyaruguguna na Nyangh'wale ulitakiwa kuanza mwezi Machi, 2010 lakini hadi sasa haujaanza licha ya tathmini ya mazao na mali za wananchi kwenye njia ya kupisha umeme huo:-

Je, Serikali inawaambia nini wananchi wa maeneo hayo na kwamba ni lini mradi huo utanza kutekelezwa?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa James Philipo Musalika, Mbunge wa Nyangh'wale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Vijiji vya Buselesele, Katoro, Rwamugasa, Nyarugusu, Bukoli, Msalala, Bukondo na Nyangh'wale ndiyo Vijiji vya Wilaya ya Geita, ambavyo vitapatiwa umeme chini ya ufadhili wa MCC. Naomba nitumie nafasi hii kusahihisha kwamba, tathmini ya mali na mazao haijakamilika, ambacho kimefanyika ni tathmini ya awali (*preliminary*) ya mali za wananchi. Tathmini ya kina (*detailed evaluation*), ili kubaini thamani ya mali za wananchi kwa wakati huu itafanywa na *Africare* kuanzia hivi karibuni kwa mikoa yote sita. Kama tulivyoeleza hapa Bungeni Julai 2009, Mradi huo utahitaji ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kVA 33, yenye urefu wa kilomita 16 kutoka kwenye kituo cha kupoza umeme kilichopo Bulyanhulu. Jumla ya *transforma* mbili zenye ukubwa wa kVA 200 zitawekwa na wateja kama 200 wanatarajiwa kunufaika na maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mradi huo umekwishanza, ambapo taratibu za manunuzi za utangazaji wa zabuni ili kumpata mkandarasi mjenzi zimeanza. Zabuni ilitangazwa tarehe 15 Machi, 2010 na zitafunguliwa tarehe 9 Julai, 2010. Ni matarajio ya Serikali kwamba, kufikia mwisho wa mwezi Agosti, 2010, mkandarasi atakayekamilisha hii kazi atakuwa amepatikana na kusaini mkataba tayari kwa kuanza ujenzi wa mradi.

Hatua hiyo ikishafikiwa na kukamilika, makubaliano ya utekelezaji na mkandarasi kufikiwa, Serikali itawatangazia wananchi wa maeneo husika ratiba ya utekelezaji na muda wa kukamilisha kwa mradi ili wananchi wajiandae kutumia umeme kwa shughuli zao za maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inapenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Wananchi wa Nyangh'wale na maeneo mengine ya Geita na Busanda kwamba ni nia ya Serikali yao kuboresha huduma muhimu ikiwemo ya umeme kwa lengo la kusukuma mbele maendeleo yao na kuboresha maisha kama ambavyo tumekuwa tukisisitiza humu Bungeni na kama ambavyo tuliwafahamisha wananchi wakati wa ziara tulizofanya Geita.

MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri. Mpango wa Mradi wa MCC katika Jimbo la Nyangh'wale ni sawa kabisa na Mpango wa MCC katika Jimbo la Busanda. Ninaomba basi kufahamu utekelezaji wa Mradi huu wa MCC katika Kijiji cha Bukoli, Rwamgasa, Nyarugusu pamoja na Katoro? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Katoro, Rwamgasa, Nyarugusu na Bukoli, kama nilivyosema umo katika maeneo sita ya Wilaya ya Geita kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa tunachofanya ni kwamba, tukianza kuanzia tarehe 9 Julai, tathmini inafanywa kwa maeneo siyo tu ya Geita, labda niseme ni kwa Miradi yote ya *Transmission and Distribution* ya MCC kwa nchi nzima ambayo kwa ujumla wake nadhani ni Miradi 207. Miradi 186 ya *Transmission* na *Distribution* na Miradi kama 20 ya Ujenzi ya *Substations*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kumalizika kwa tathmini ya mazingira na hii ya kutathmini mali ya wananchi wanaopitiwa na mradi huo, sambamba na hiyo tunaratajia kwamba, ifikapo mwisho wa mwezi Agosti, mkandarasi atakuwa amepatikana na kwa ujumla miradi yote hii nchi nzima inatarajiwa itumie kama miaka miwili hivi, lakini kuna ambayo itakamilika muda mfupi zaidi kuliko mingine. Karatasi ya miradi yote ni hii hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Bukwimba na Wabunge wote wanaopitiwa na Miradi hii kwamba, kama watahitaji taarifa za utekelezaji wa Mradi wa MCC, *book* ninalo hapa, tuonane baadaye ili niwafahamishe.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema tumekopa muda na tumetumia dakika zaidi ya zile tunazotumia. Kwa ujumla mtatambua kwamba, leo Mawaziri wamejibu maswali, yaani maswali yaliyoandikwa ni *page* moja, halafu inatoa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza zaidi ya Wabunge wawili. Sasa hiyo inaweka hali ya Bunge iwe changamfu. Mtu akituhutubia mpaka tunasinzia, inakuwa siyo kipindi cha maswali. Kipindi cha maswali, maswali mafupi, ya nyongeza na nini kusudi watu wote wachangamke, inakuwa kama *warm up*. Kwa hiyo, naomba endeleeni kuizingatia hiyo Mawaziri kuwa majibu yenu *page* moja inatosha.

Wageni walioko Bungeni asubuhi hii, kwanza ni wageni wa Mheshimiwa Hawa Ghasia, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi), ambao ni wasanii maarufu katika Kipindi cha Fataki, TBC 1. (*Kicheko*)

Wapo hapa Bungeni kwa ajili ya kutembelea Bunge nao ni kama ifuatavyo: Kiongozi wao anaitwa Musa Ngalemwa; asimame tumwone. Pamoja nao wapo Mohamed Ngogota, Saidi Machenje, Jumanne Mbulu, Zaibina Hassan na Sarafina Rajabu. (*Makofi*)

Nadhani hapa ndani mashabidi wa Fataki watakuwepo tu. Mimi sipendi kabisa hicho kitu. Ahsante naomba muendeleo kuhamisha hili suala zima la watoto kudanganywa na watu ambao wengine hata pesa hawana, basi tu ni Fataki. (*Makofi*)

Tunao pia wageni wa Mheshimiwa Zabein Mhita, ambao ni wanafunzi 67 na walimu 8 kutoka Shule ya Msingi Iboni, Kondo. Walimu na wanafunzi wote wasimame. Aah ndiyo hawa hapa. Karibuni sana, tumefurahi kuwaoneni. Tunaomba msome kwa bidii na walimu tunawashukuru sana kwa kazi mnayoifanya. Karibuni sana. (*Makofi*)

Halafu nina wageni wengine, Mheshimiwa naomba uwe unawapeleka kunakohusika ili waweze kuchapishwa kama wengine. Dr. James Wanyancha ana wageni wake, ambao ni Engineer Fredrick Kabori kutoka Sengerema na anafanya kazi *College of Engineering and Technology Dar es Salaam*. Ninafikiri cheo chake kule Dar es Salaam ni *Resource Mobilization Officer*. Yuko wapi huyu? Ahsante bwana *Engineer*. Tunakutakia kazi njema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba, leo hii saa 5 asubuhi katika Ukumbi wa Pius Msekwa, watakuwa na Kikao chao kukamilisha kazi inayohusika kwa Wizara ile. Kwa hiyo Wajumbe wa Kamati hiyo msikose kuhudhuria.

Tangazo la msiba. Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyofahamu, sisi hapa Mezani tunasaidiwa na Wenyeviti watatu; sasa Mwenyekiti Mheshimiwa Jenista Mhagama toka wiki iliyopita aliondoka kidharura, mume wake alikuwa anaumwa na jana kuamkia leo amefariki. Kwa hiyo, maandalizi ya mazishi watamzika tarehe 17 Kijijini kwake Marehemu Ruanda katika Wilaya ya Peramiho. Mimi pia nitakwenda kwa ajili ya mazishi hayo kesho. Kwa hiyo, hiyo ndiyo taarifa tuliyonayo ya msiba. Mwenyezi Mungu, aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi. *Amen*.

Waheshimiwa Wabunge, tunapoingia katika Muswada huu wa *Finance Bill*, mmepata wachangiaji wangapi. *Okay!* Angalau wapo hao. Mnaalikwa tena kujiandikisha wanaotaka kuchangia.

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada ya Sheria ya Fedha wa Mwaka 2010 (*The Finance Bill, 2010*)

(Kusomwa Mara ya Pili)

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2010 (*The Finance Act, 2010*), pamoja na marekebisho yake sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kutosha shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, chini ya Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Dr. Abdallah Omari Kigoda, Mbunge wa Handeni, kwa kuujadili kwa kina Muswada huu na kutoa ushauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, Muswada huu umezingatia kwa kiasi kikubwa, ushauri na mapendekezo ya Kamati na pia tutaendelea kufanyia kazi mapendekezo mengine yaliyowasilishwa. Aidha, kwa mara nyingine napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote ambao walichangia katika Hotuba ya Bajeti ya Serikali niliyowasilisha wiki iliyopita na kupitishwa na Bunge jana tarehe 14 Juni, 2010. Namshukuru pia Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa kuuandaa Muswada huu pamoja na marekebisho yake. Wadau mbalimbali katika Sekta ya Fedha, Biashara na Sekta Binafsi na wananchi kwa ujumla, ambao kwa nyakati tofauti walitoa ushauri wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu ni utekelezaji wa hatua kadhaa za mfumo wa kodi ikiwemo kurekebisha baadhi ya viwango vya ushauri, ada na tozo mbalimbali kama zilivyoinishwa katika Hotuba ya Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unakusudia kuzifanyia marekebisho Sheria 11 zinazohusu masuala ya fedha, kodi na ushuru. Kwa lengo la kuweka, kurekebisha na kufuta viwango vya kodi, ushuru na ada mbalimbali ili kurekebisha ukusanyaji wa kodi. Sheria zinazohusika ni hizi zifuatazo:-

Moja, Sheria ya Korosho, Sura ya 203. Pili, Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147. Tatu, Sheria ya Bodi ya Michezo ya Kubahatisha, Sura ya 41. Nne, Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332. Tano, Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290. Sita, Sheria ya Magari, Kodi ya Usajili na Uhamisho wa Umiliki wa Magari, Sura ya 124. Saba, Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Sura ya 348. Nane, Sheria ya Ukaguzi wa Fedha na Mali za Umma, Sura ya 418. Tisa, Sheria ya Uwekezaji, Sura ya 38. Kumi, Sheria ya Miji, yaani Ukadiriaji wa Majengo, Sura ya 289. Kumi na moja, Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148.

Mheshimiwa Naibu Spika, Madhumuni ya Muswada: Muswada huu umegawanyika katika sehemu 12; sehemu ya kwanza inayojumuisha vifungu namba (1) na (2) inahusu masuala ya utangulizi, kama vile jina na tarehe ya kuanza kutumika kwa sheria hii, ambapo sheria itaanza kutumika tarehe 01 Julai, 2010. Sehemu ya pili kama ilivyorekebisha, yenye vifungu namba (3) na (4), inapendekeza kurekebisha Sheria ya

Korosho, Sura ya 203, katika kifungu cha (17) kwa kuongeza kifungu kipya cha (17)(a) ili kutoa mamlaka kisheria kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania kukusanya ushuru kutoka korosho ghafi inayosafirishwa nje ya nchi. Aidha, inapendekezwa kuongeza kiwango cha ushuru wa korosho ghafi inayosafirishwa nje ya nchi kutoka 10% ya sasa ya bei ya korosho ghafi hadi 15% au kiasi cha Shilingi za Tanzania, sawa na Dola za Kimarekani 160 kwa kila ujazo wa tani moja kwa kutegemea kiwango kipi ni kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mgawanyo wa Mapato yatakayokusanywa na TRA, utakuwa kama ifuatavyo:-

(a) Asilimia 65 ya makusanyo yatapelekwa kwenye Mfuko wa Sekta ya Maendeleo ya Korosho, yaani *Cashewnut Industry Development Fund* na yatatumika kwa ajili ya kuendelea sekta ya korosho na kuhamasisha ubanguaji wa korosho nchini. Aidha, Waziri mwenye dhamana na masuala ya kilimo baada ya kushauriana na wadau, anatararisha Kanuni zitakazoweka utaratibu wa mgawanyo na matumizi ya fedha hizo.

(b) Asilimia 35 ya makusanyo yote yatapelekwa katika Mfuko Mkuu wa Hazina kama mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tatu inapendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147 katika vifungu namba (2), (122), (124) na jedwali la nne kama ifuatavyo:-

(a) Kurekebisha kifungu cha pili ili kuongeza tafsiri mpya ya neno *Minister* ili kumtambua Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha kuwa ndiye msimamizi wa Sheria hii.

(b) Kurekebisha kifungu cha 122(2) ili kuweka bayana kwamba, Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha atakuwa na mamlaka ya kutayarisha Kanuni kwa ajili ya utekelezaji wa sheria hii.

(c) Kurekebisha kifungu cha 124 (3), ili kuwezesha ushuru wa bidhaa katika huduma za simu za mikononi kutozwa katika muda wa maongezi pekee, yaani *air time*, badala ya utaratibu wa sasa wa kutoza kwenye huduma ya simu, yaani *mobile phone service*.

(d) Kurekebisha Jedwali la Nne ili kurekebisha kwa 8% viwango maalum vya ushuru wa bidhaa kwenye bidhaa zinazotowza ushuru huu, isipokuwa zile za mafuta ya petroli.

Marekebisho haya yamezingatia kiasi cha wastani cha mfumko wa bei. Viwango vya sasa na vile vinavyopendekezwa ni kama ifuatavyo:-

(1) Vinywaji baridi kutoka shilingi 58 kwa lita hadi shilingi 63 kwa lita.

(2) Bia inayotengenezwa na nafaka ya hapa nchini na ambayo haijaoteshwa kutoka shilingi 209 kwa lita hadi shilingi 226 kwa lita.

(3) Bia nyingine zote kutoka shilingi 354 kwa lita hadi shilingi 382 kwa lita.

(4) Mvinyo uliotengenezwa kwa zabibu inayozalishwa nje ya nchi kwa kiwango kinachozidi 25% kutoka shilingi 1,132 kwa lita hadi shilingi 1,223 kwa lita.

(5) Vinywaji vikali kutoka shilingi 1,978 kwa lita hadi shilingi 1,812 kwa lita.

(e) Kurekebisha viwango vya ushuru wa bidhaa kwenye sigara kama ifuatavyo:-

(1) Sigara zisizo na kichungi na zinazotengenezwa kutokana na tumbaku inayozalishwa hapa nchini kwa kiwango cha angalau 75% kutoka shilingi 5,749 hadi shilingi 6,209 kwa sigara 1000.

(2) Sigara zenye kichungi na zinazotengenezwa kutokana na tumbaku inayozalishwa hapa nchini kwa kiwango cha angalau 75% kutoka shilingi 13,564 hadi shilingi 14,649 kwa sigara 1000.

(3) Sigara nyingine zenye sifa tofauti na (a) na (b) kutoka shilingi 24,633 hadi shilingi 26,604 kwa sigara 1000.

(4) Tumbaku ambayo iko tayari kutengezwa sigara, yaani *cut filler* kutoka shilingi 12,441 hadi 13,436 kwa kilo.

(5) Ushuru wa sigara unabaki 30%.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili ni kupunguza kiwango cha sasa cha ushuru wa bidhaa kwenye mafuta mazito ya kuendeshea mitambo kutoka shilingi 97 kwa lita hadi shilingi 80, ili kupunguza gharama ya uzalishaji viwandani na kuongeza uwezo wa ushindani wa bidhaa zinazozalishwa nchini katika soko. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama za uzalishaji wa bidhaa hapa nchini. Aidha, punguzo hili limezingatia makubaliano kati ya Serikali na wamiliki wa viwanda ya kupunguza ushuru huu hatua kwa hatua hadi kuufuta kabisa ndani ya kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya nne inapendekeza marekebisha ya Sheria ya Bodi ya Michezo ya Kubahatisha, Sura ya 41 kwa kurekebisha Jedwali la Pili ili:-

(a) Kuongeza kiwango cha kodi inayotozwa kwenye mashine za kuchezea kamari, yaani *slot machines*, kutoka shilingi 16,000 za sasa hadi shilingi 32,000.

(b) Kutoza kodi ya kiwango cha 13% kwenye kasino ndogo zenye idadi ya mashine za kamari zilizozidi 40, yaani *forty machines site*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tano pamoja na marekebisho yake inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332, kama ifuatavyo:-

(a) Kurekebisha kifungu cha 11 ili kuweka wigo wa ukomo wa maeneo ya uchimbaji madini, yaani *ring fancying*, ili kuhakikisha kwamba, gharama zitakazotolewa wakati wa kukokotoa faida inayopaswa kutozwa kodi ya mapato kuwa ni zile za eneo husika tu, tofauti na ilivyo sasa ambapo gharama za mgodi mmoja zinaweza kufidiwa kwenye mgodi mwingine wenye faida. Pendekezo hili litaiwezesha serikali kupata mapato kutoka kwenye makampuni yanayochimba madini hapa nchini na ambayo yana mgodi zaidi ya mmoja.

(b) Kurekebisha kifungu cha 12 kwa kufuta vifungu vidogo vya (2) na (3) na kuweka kifungu kidogo kipya cha (2) ili kuweka sharti kwamba, gharama ya riba inayotozwa na makampuni katika mikopo ya uendeshaji wa biashara itakayokubalika kama mojawapo ya gharama zinazopaswa kutolewa wakati wa kukokotoa faida inayopaswa kutozwa kodi ya mapato ni ile itakayohusisha makampuni yenye uwiano wa mikopo na mtaji, yaani *debt to equity ratio*, isiyozidi 705 na mtaji usiopungua 30%; *debt to equity ratio of 70% to 30%*. Lengo la hatua hii ni kulinda wigo wa kodi kwa kudhibiti gharama za riba inayotozwa na kampuni katika mikopo ya uendeshaji.

(c) Kurekebisha kifungu cha 80 kwa kuweka kifungu kipya cha 80(a) ili kuweka sharti kwa kampuni, mtu au taasisi kutoa stakabadhi kwa malipo ya kuanzia shilingi 5,000 au zaidi, kwa huduma au bidhaa na kutunza stakabadhi husika kwa kipindi kisichopungua miaka mitano baada ya kupokea stakabadhi husika.

(d) Kurekebisha kifungu cha 83(a) ili kutoza kodi ya zuwio, yaani *withholding tax*, kwa kiwango cha 2% kwa malipo ya wafanyabiashara waliosajiliwa wanaponunua bidhaa na huduma kutoka kwa wazabuni wasiosajiliwa chini ya utaratibu wa *TIN*. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kwamba, wafanyabiashara hawa wanalipa kodi na hivyo kuchangia huduma zinazotolewa na Serikali.

(e) Kurekebisha kifungu cha 98 kwa kuongeza kifungu kidogo cha (2) ili kutoa adhabu ya kiasi kisichozidi shilingi 2,000,000 au kifungu kisichozidi mwaka mmoja au faini na adhabu kwa pamoja kwa mtu, kampuni au taasisi itakayokiuka matakwa ya sheria kuhusu kutoa risiti.

(f) Kurekebisha kifungu cha 100 (1) ili kiwango cha riba kinachotozwa kwa mlipa kodi atakayechelewa kulipa kodi, kiwiane na kiwango cha riba kinachotozwa na Mabenki ya Biashara ambacho ni kikubwa kikilinganishwa na kiwango kinachotozwa hivi sasa kwa kuzingatia riba inayotozwa na Benki Kuu, yaani *statutory rate*. Lengo la hatua hii ni kuhakikisha walipa kodi wanalipa kodi kwa wakati.

(g) Kurekebisha kifungu cha 134, kwa kuongeza kifungu kidogo cha (3) ili kuweka adhabu ya kusitisha leseni ya mshauri mwelekezi wa masuala ya kodi, yaani *tax*

consultant, pindi anapobainika kumsaidia mlipa kodi kutayarisha taarifa za uwongo kwa lengo la kukwepa kodi. Hata hivyo, mshauri mwelekezi ambaye hataridhika na maamuzi ya Kamishna, ana haki ya kupinga maamuzi hayo kwa mujibu wa Kanuni za Rufaa ya Kodi.

(h) Kurekebisha kifungu cha 145 ili kuwezesha utaratibu wa *ring fencing* kwa makampuni ya madini kuhusisha makampuni ya madini ambayo yanatoza kodi ya mapato kwa kutumia Sheria ya Kodi ya Mapato ya Mwaka 1973.

(i) Kurekebisha jedwali la kwanza katika aya ya kwanza ili:-

(1) Kupunguza kiwango cha chini cha kodi ya mapato kutoka 15% ya sasa hadi 14%.

(2) Kuongeza kiwango cha mapato ambacho hakitatozwa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya sita inapendekeza kurekebisha aya ya kwanza ya Jedwali la Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290, ili kurekebisha kiwango cha kutoza ushuru wa mazao shambani kuwa ni 3% hadi 5% ya bei ya kuuza mazao shambani ili kutoa fursa kwa Halmashauri na Serikali za Mitaa kutoza ushuru huo kulingana na uwezo na rasilimali za Halmashauri na Serikali za Mitaa husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya saba inapendekeza kufanya marekebisho kwenye Jedwali la Kwanza la Sheria ya Magari, yaani Kodi ya Usajili na Uhamisho wa Umiliki wa Magari; Sura ya 124 kama ifuatavyo:-

(a) Kurekebisha aya ya 3 ili kuongeza viwango vya ada ya usajili wa magari kutoka shilingi 120,000 ya sasa hadi shilingi 150,000.

(b) Kurekebisha aya ya 4 ili kuongeza kiwango cha ada ya usajili wa pikipiki kutoka shilingi 35,000 hadi shilingi 45,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya nane pamoja na marekebisho yake, inapendekeza marekebisho yafuatayo katika Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma katika Sura ya 348. Kwanza, kupitia jedwali la marekebisho, kurekebisha kifungu cha nne kuhusu tafsiri ya maneno Afisa Masuhuli, yaani *Accounting Officer*, ili kuhuisha Maafisa Masuhuli wa Halmashauri, wanaoteuliwa chini ya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa. Lengo la marekebisho haya ni:-

(1) Kumuwezesha Mlipaji Mkuu wa Serikali, kutekeleza majukumu yake ya kusimamia matumizi ya fedha za umma ikiwa ni pamoja na kutoa maelekezo kwa Maafisa Masuhuli.

(2) Kurekebisha kifungu cha 7(2) cha sheria ili kumpa Mhasibu Mkuu wa Serikali, mamlaka ya kusimamia fedha zinazopelekwa katika Halmashauri.

(3) Kuhuisha ndani ya sheria hii, sehemu mpya ya 5 ya vifungu vya 37 hadi 39 ili kuanzisha ndani ya Wizara ya Fedha na Uchumi, Idara ya Usimamizi wa Ukaguzi wa Ndani pamoja na majukumu ya Mkaguzi wa Ndani wa Hesabu, kama ifuatavyo:-

(a) Kifungu kipya cha 37 kinaanzisha Idara ya Usimamizi wa Ukaguzi wa Ndani pamoja na Uteuzi wa *Internal Auditor General*, ambaye atateuliwa na Mheshimiwa Rais.

(b) Kifungu kipya cha 38 kinabainisha majukumu ya *Internal Auditor General*, ambapo pamoja na mambo mengine, atasimamia utayarishaji na utekelezaji wa Sera na Taratibu za masuala ya ukaguzi wa ndani ili kuimarisha uwajibikaji kuhusu mali na fedha za umma, kufanya ukaguzi wa mali, fedha na shughuli za Serikali na kuishauri Serikali kuhusu hatua mbalimbali za kuchukua ili kuweka utaratibu mzuri wa matumizi yenye tija kwa fedha za Serikali, yaani *Value for Money on Public Expenditure*. Aidha, *Internal Auditor General*, atakagua taarifa za mali, fedha na shughuli za *MDAs*, Mikoza, Halmashauri, Taasisi za Serikali na Miradi ya Wafadhili na kuwasilisha taarifa husika pamoja na maoni yake kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali.

(c) Kifungu kipya cha 39 kinafafanua sifa za watumishi watakaoajiriwa chini ya Idara ya Usimamizi wa Ukaguzi wa Ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya 9, inapendekeza marekebisha ya Sheria ya Mkaguzi na Mdhhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, Sura ya 418, kwa kufuta kifungu cha 27 na kuweka kifungu kipya ili kumuwezesha Mkaguzi na Mdhhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwa kuwasiliana na vyombo vya dola, kushughulikia ubadhirifu wa fedha na mali za umma pindi unapobainika wakati wa kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya 10 pamoja na marekebisha yake, inapendekeza marekebisha ya kifungu cha 19 cha Sheria ya Uwekezaji, Sura ya 38 kwa kuongeza kifungu kidogo cha (3) ili kuondoa msamaha wa kodi kwa magari yenye umri wa miaka 10 au zaidi tangu mwaka wa kutengenezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya 11, inapendekeza marekebisha ya kifungu cha 23 cha Sheria ya Miji na Ukadiriaji wa Majengo, Sura ya 289, kwa kuongeza kifungu kidogo cha (3) ili kusamehe kodi ya majengo kwenye nyumba zinazomilikiwa na wazee wenye umri wa zaidi ya miaka 60, pamoja na walemavu ambao hali zao kiuchumi haziwawezeshi kulipa kodi hii. Aidha, msamaha huu utatolewa kwa wale watakoathibitishwa na Uongozi wa Serikali za Mitaa kuwa kweli hawana uwezo wa kulipa kodi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya 12 pamoja na marekebisha yake, inapendekeza marekebisha ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148 kama ifuatavyo:-

(a) Kurekebisha kifungu cha (2) ili kuhuisha ndani ya Sheria tafsiri ya maneno *Physical Receipt*.

(b) Kufanya marekebisha ya kiuandishi katika kifungu cha 5(2) ili huduma za usindikaji bidhaa; kwa mfano, kusaga nafaka, kubangua korosho na kadhalika, zitambuliwe kama ni utoaji wa huduma badala ya ilivyo sasa ambapo huduma hizi zinatambuliwa kuwa ni utoaji wa bidhaa.

(c) Kurekebisha kifungu cha 11 kwa kuongeza vifungu vidogo vya (3) na (4) ili kubainisha kwamba, misamaha itakayotolewa chini ya Sheria hii, haitahusisha magari yenye umri wa miaka 10 au zaidi, kuanzia mwaka wa kutengenezwa. Aidha, hatua hii haitahusisha magari ya taasisi za kidini.

(d) Kurekebisha kifungu cha 13 ili:-

(i) Katika kifungu kidogo cha (4), kufafanua kwamba thamani ya vocha kwa ajili ya utozaji kodi, itapatikana baada ya kuondoa kiwango cha kodi ya ongezeko la thamani kwenye bei halisi inayooneshwa kwenye vocha.

(ii) Kuongeza kifungu kidogo katika sheria kinachotoa tafisi ya nyongeza ya muda wa maongezi unaotolewa kama zawadi na unaotowza kodi ya ongezeko la thamani.

(e) Kurekebisha kifungu cha 16 ili kubainisha matumizi ya *physical receipt* katika kifungu hiki. Hatua hii inatokana na kuanza kwa matumizi ya mfumo mpya wa ukusanyaji kodi kupitia *electronic physical device* badala ya utumiaji wa *cash register* uliopo hivi sasa. Pili ni kuongeza kifungu kidogo cha (5) ili kufafanua kwamba, gharama zitakazotumiwa na wafanyabiashara katika ununuzi wa *electronic physical device* watarejeshewa kupitia Kodi ya VAT, watakayokusanya katika mauzo hayo.

(f) Kurekebisha kifungu cha 29 ili kubainisha matumizi ya *physical receipt* ndani ya Sheria hii. Pili, kurekebisha kifungu kidogo cha (3) ili kuongeza faini kutoka shilingi 500,000 hadi shilingi 1,000,000 kwa wafanyabiashara watakaokiuka matakwa ya Sheria hii, kuhusu kutoa stakabadhi ya malipo. Tatu, kuweka sharti kwa kampuni, mtu au taasisi kudai stakabadhi wakati wa kulipia huduma au bidhaa.

(g) Kurekebisha kifungu cha 47 (1) ili kuongeza kiwango cha adhabu kwa kosa la kukwepa kodi kwa njia ya udanganyifu, kutoka kiwango cha sasa cha faini ya shilingi 2,000,000 hadi shilingi 5,000,000 au mara mbili ya kodi ambayo mlipa kodi hakulipa kwa kutegemea kiwango kipi ni kikubwa, au kifungu cha miaka miwili au faini na kifungu kwa pamoja. Hatua hii inakusudia kupunguza ukwepaji wa kodi.

(h) Kurekebisha Jedwali la Kwanza linalohusu bidhaa na huduma zinazotowza kodi kwa kiwango cha zero, kama ifuatavyo:-

(1) Kwanza ni kuongeza aya mpya ya 14 ili kutoza kodi ya ongezeko la thamani kwa kiwango cha 0% kwenye uzalishaji wa mafuta ya kula kwa wazalishaji wanaotumia mbegu za mafuta zinazozalishwa hapa nchini.

(2) Kuongeza aya ya 15 ili kutoza kodi ya ongezeko la thamani kwa kiwango cha 0% kwa vyakula vya mifugo vinavyozalishwa hapa nchini.

(i) Kurekebisha Jedwali la Pili linalohusu bidhaa na huduma zinazosamehewa kodi, yaani *exempted supplies and imports* kama ifuatavyo:-

(1) Katika aya ya 5, kwa kufuta aya ndogo ya 3, ambayo inatoa msamaha wa kodi kwa vifaa vinavyouzwa kwa wataalamu wa mifugo waliosajiliwa. Vifaa hivi tayari vinapata unafuu wa kodi chini ya Jedwali la Tatu la Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani.

(2) Kurekebisha aya ya 13 ili kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye zana za kilimo kama vile mashine ya kukatia majani shambani na mashine za kusindika majani ya mifugo, yaani *hay making machine*.

(3) Kurekebisha aya ya 27 kwa kufanya marekebicho ya kiuandishi na kuongeza aya ndogo ya 2 ili kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye huduma za usafirishaji wa mazao ya kilimo kutoka shambani hadi kwenye viwanda vya usindikaji kwa wakulima wenye kilimo cha mkataba kama miwa, mkonge na chai.

Mheshimiwa Naibu Spika, msamaha huu umetolewa kwenye mazao ya miwa, mkonge na chai kwa kuzingatia asili ya mazao haya ambayo hupaswa kusindikwa ndani ya saa 24 baada ya mavuno kutoka mashambani.

Aidha, kilimo cha miwa, mkonge na chai, kwa sasa ndiyo pekee kinachohusisha mikataba baina ya viwanda na wakulima ambao huendesha shughuli za kilimo jirani na viwanda, yaani *organised farming*.

Aidha, wakulima wa mazao mengine watakojitokeza na kuanza utaratibu wa kilimo cha pamoja, yaani *organised farming* na wao watajumuishwa kwenye msamaha huu.

(4) Kurekebisha aya ya 27 kwa kuongeza aya ndogo mpya ya (3) ili kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye huduma za kuzalisha mifugo kwa njia ya kupandisha mifugo na utumiaji wa mashine maalum za kuzalishia au kutotolea vifaranga.

(5) Kufanya marekebicho ya kiuandishi kwenye aya ya 28 na kuongeza msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye mashine na vifaa vya kusindika maziwa ili kuhamasisha wawekezaji kuwekeza katika sekta ndogo ya maziwa.

6. Kufuta na kuweka aya mpya ya 30 ili kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye vyakula vya mifugo vinavyozalishwa nchini na mashudu. Hatua hii ina lengo la kuhamasisha ufugaji bora na uzalishaji wa vyakula vya mifugo hapa nchini.

7. Kuongeza aya mpya ya 31 ili kusamehe kodi la ongezeko la thamani kwenye vifungashio vya *juice* za matunda na bidhaa za maziwa. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama za uzalishaji ili kuboresha thamani ya bidhaa inayozalishwa kwenye viwanda vya *juice* na maziwa hapa nchini. (j) Kurekebisha jedwali la tatu linalohusu nafuu maalum ya kodi yaani *special relief* kama ifutavyo: -

(i) Kufuta aya ya nane na kuweka aya ya 8.8(a) ili kuanza kutoa msamaha maalum ya kodi ya ongezeko la thamani kwa kampuni za madini zenye mikataba na Serikali. Msamaha unatolewa kwa mujibu wa masharti yaliyoko katika mikataba kati ya Serikali na makampuni ya madini yaliyosaini mikataba kabla ya Julai 1, 2009.

(ii) Ili kutoa msamaha maalum wa kodi ya ongezeko la thamani *and VAT special relief* kwa kampuni za utafiti na uchambaji wa mafuta ya petroli na gesi ambapo msamaha huu utahusisha huduma na bidhaa za utafiti na utafutaji pekee ambao hufanywa na mwekezaji kabla ya kuanza uzalishaji.

(iii) Kurekebisha aya ya 19 kwa kuongeza aya mpya ya 19(a) ili kutuo msamaha maalum wa kodi ya ongezeko la thamani yaani VAT special relief kwa huduma, vifaa na bidhaa za ujenzi kwa waendelezaji wa maeneo ya uwekezaji yaliyosajiliwa chini ya sheria ya *export posting zone* ya 2006.

(iv) Kuongeza aya mpya ya 31 ili kutoa msamaha maalum wa kodi ya ongezeko la thamani yaani *VAT special relief* kwenye mabanda maalum yanayotumika katika kilimo cha maua *a green house*.

(v) Kuongeza aya mpya ya 32 ili kutoa msamaha maalum wa kodi ya ongezeko la thamani yaani *VAT special relief* kwenye uuzaji wa bidhaa na huduma zitolewazo kwa wakulima waliosajiliwa au mashamba ya Vyama vya Ushirika kwa ajili ya kujenga miundombinu ya mashamba kama vile mifereji ya umwagiliaji, barabara za mashambani, ujenzi wa maghala na huduma nyingine ya namna hii.

Aidha, kutumia jedwali la marekebisho inapendekezwa kwamba msamaha huu utatolewa kwa bidhaa na huduma zitakazoidhinishwa na Waziri mwenye dhamana na masuala ya kilimo baada ya ukaguzi utakaofanywa na maofisa wa kilimo wa eneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hatua zilizobainishwa katika hotuba ya bajeti zitatekelezwa na Mawaziri husika kupitia matangazo ya Serikali yaani *Government Notices* kwa mujibu wa matakwa wa sheria husika. Hatua hizo ni pamoja na ifuatavyo:-

(i) Kuongeza viwango vya ada ya mwaka ya leseni ya magari ambapo Waziri mwenye dhamana na masuala ya usalama barabara atatekeleza kupitia tangazo la Serikali. Viwango hivyo ni kama ifuatavyo: Ukubwa wa *engine* usiozidi CC 500, kiasi kinachotazwa sasa ni shilingi 30,000 kiasi kinachopendekezwa ni shilingi 50,000, CC 501 hadi CC 1500 kutoka shilingi 50,000 hadi shilingi 100,000, CC 1501 hadi 2500 kutoka shilingi 100,000 za sasa hadi 150,000 na CC 2001 na zaidi kutoka shilingi 150,000 za sasa hadi shilingi 200,000.

(ii) Kurekebisha Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 148 ili kutoa msamaha wa ushuru wa bidhaa kwenye bidhaa za petroli kwa kampuni za madini zilizosaini mikataba na Serikali. Msamaha huu utatolewa kwa mujibu wa masharti yaliyopo katika mikataba kati ya Serikali na makampuni ya madini yaliyosaini mikataba kabla ya Julai 1, 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, kama nilivyoeleza hapo awali mengi ya marekebisho ninayopendekeza ni utekelezaji kisheria wa mapendekezo ya Serikali kuhusu bajeti ya mwaka fedha 2010/2011. Kwa hiyo, naomba sasa Waheshimiwa Wabunge muujadili Muswada huu na hatimaye mkubali kuupitisha ili kuhalalisha kisheria bajeti iliyopitishwa na Bunge tarehe 14 Juni, 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

MHE. DR. ABDALLAH KIGODA-MWENYEKITI KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Mwaka 2007, tarehe 13 Juni, 2010, Dodoma Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2010 uliowasilishwa na Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Mustafa Mkulo, Kamati inaendelea kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa ushirikiano mzuri na Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa iliyowasilishwa mbele ya Kamati ilionyesha maeneo mbalimbali ya Muswada wa Sheria ya Fedha yanayopendekezwa kufanyiwa marekebisho katika kutekeleza kisheria hatua kadhaa kuhusu mfumo wa kodi ikiwemo kurekebisha baadhi ya viwango vya ushuru, ada na tozo kama zilivyoainishwa katika Hotuba ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2010/2011. Katika Kamati Waziri alitoa taarifa ya kukusudia kuzifanyia marekebisho sheria kumi na moja. Kamati imeridhika kuwa marekebisho mengi yamelenga katika kukuza uzalishaji kwenye sekta za fedha, viwanda, madini, kilimo na mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mambo muhimu yaliyojadiliwa na Kamati. Marekebisho katika Sheria ya Korosho, kimsingi Kamati inakubaliana na marekebisho haya yaliyofanyika na kuishauri Serikali ikae na wadau wote wa korosho kupanga mgao wa mapato wa ushuru husika pamoja na mfuko wa korosho. Kamati imeishauri Serikali utaratibu huu vilevile ufanywe pia kwa mazao mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, kama ilivyotokeza kwenye Hotuba ya Bajeti marekebisho ya sheria hii yamegusa maeneo mengi. Kamati imekubaliana na mapendekezo yote ya marekebisho, lakini iliishauri Serikali kwenda kwa kasi zaidi kuondoa kabisa ushuru wa bidhaa kwenye mafuta mazito ya kuendeshea mitambo ili kupunguza gharama za uzalishaji viwandani na kuongeza

uwezo wa ushindani. Aidha, Kamati ilisisitiza Serikali iweke mikakati ya kupunguza gharama ya uzalishaji wa simenti ili iweze kushindana na simenti inayotoka nchi za nje (Misri na Pakistan) hata kwa kutoa ruzuku, kwani nchi ikiendelea kununua simenti kutoka nje ambayo bei yake iko chini ina maana tunaendeleza ajira kwa nchi zinazozalisha simenti na tunaondoa ajira hapa nchini, tunapunguza kodi na kudidimiza Pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu marekebisho katika Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332. Kamati inakubaliana na pendekezo la Serikali la kuweka wigo wa ukomo wa maeneo ya uchimbaji madini (*ringfencing*). Rekebisho hili litasaidia Serikali kupata mapato na kuepukana na utaratibu wa makampuni ya madini kuikoshesha Serikali mapato. Kamati inasisitiza kwamba msamaha wa kodi ya mafuta uliotolewa kwa makampuni ya madini yenye Mikataba (*MDAs*) uangaliwe kwa makini kwani mafuta hayo yanaweza kutumika kwa utaratibu usiokusudiwa na hivyo kupoteza Serikali mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kufanya marekebisho kwa kuweka sharti kwa kampuni, mtu au taasisi kutoa stakabadhi kwa malipo ya kuanzia kiasi cha shilingi elfu tano na kutunza stakabadhi husika kwa kipindi kisichopungua miaka mitano. Kamati iliunga mkono pendekezo hilo ili kujenga tabia kwa wafanyabiashara wetu kutoa risiti kila inapofanya biashara kwa lengo la kuimarisha mfumo wa kutunza kumbukumbu na kuboresha mapato ya Serikali. Hata hivyo, Kamati ilishauri Serikali kutoa elimu na mafunzo katika kuhamasisha wafanyabiashara na Watanzania kwa ujumla katika hili. Aidha, Kamati imeishauri Serikali kuendelea kudhibiti wafanyabiashara wenye tabia ya kutoota risiti na hivyo kuipotezea Serikali mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu marekebisho katika kiwango cha kutoza Ushuru wa Mazao shambani kuwa kati ya asilimia tatu na asilimia tano, Kamati iliunga mkono rekebisho hili na kutoa angalizo kuwa ingawa Halmashauri nyingi zinahitaji mapato, ushuru utakaotozwa uzingatie viwango husika kutokana na maeneo yao, ili ushuru huu usigeuke kuwa ni kero kwa wananchi na vilevile kwa Halmashauri zenyewe kuzipatia mapato. Serikali iweke mikakati ya kuiwezesha Wizara ya TAMISEMI kusisitiza Halmashauri ili kutoza ushuru kwa thamani ya mazao yanayopatikana katika Halmashauri husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu marekebisho katika Sheria ya Usajili na Uhamisho wa Umiliki wa Magari, kuhusu marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Usajili na Uhamisho wa Umiliki wa Magari. Kamati ilikubaliana na mapendekezo ya Serikali lakini ilionyesha wasiwasi katika kuongeza ushuru wa kodi ya usajili na Uhamisho wa Umiliki kwa magari yenye kutoa huduma muhimu kwa jamii ikiwa ni pamoja na pikipiki, usafiri ambao hivi sasa unatumiwa sana na wananchi wenye kipato kidogo. Kamati imeishauri Serikali iangalie namna nyingine ya kupata mapato hayo kwa kuongeza kodi sehemu zingine kuliko kuwatoza wamiliki wa pikipiki ambao wengi wao kipato chao ni cha chini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na marekebisho ya kuanzisha Idara ya Usimamizi wa Ukaguzi wa Ndani na kubainisha majukumu yake. Kamati inaunga mkono

marekebisho yaliyoletwa. Hii ni kutokana na umuhimu katika kuboresha ukaguzi wa ndani na uwajibikaji wa mali na fedha za umma na kuweka utaratibu mzuri wa matumizi yenye tija kwa fedha za Serikali yaani *value for money on public expenditure*.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho ya sheria ya Miji (Ukadiriaji wa Majengo), Kamati inakubaliana na rekebisho hili ila kusamehe kodi ya majengo kwenye nyumba zinazomilikiwa na wazee wenye umri zaidi ya miaka sitini pamoja na ushauri uliotolewa Kamati inaipongeza Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura 148. Hatua ya Serikali ya kuweka kiwango cha asilimia sifuri kwenye uzalishaji wa mafuta ya kula kwa wazalishaji wanaotumia mbegu za mafuta zilizozalishwa hapa nchini na vyakula vya mifugo vinavyozalishwa hapa nchini imepongezwa na Kamati. Hivi sasa uchumi wetu unasindika kati ya asilimia tano hadi kumi na karibu asilimia 90 tunauza ghafi vivutio hivi viwekwe vilevile kwenye mazao yetu muhimu tunayoyazalisha. Aidha, Kamati inaishauri Serikali pamoja na kuweka kodi kwa kiwango cha sifuri kwenye mashudu. Hali hii vile vile ijumuishe *vitamins* zake zinazochanganywa na mashudu ya mifugo, pamoja na kuweka unafuu wa kodi kwa sekta ya uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika kuhusu marekebisho ya kutoa msamaha maalum wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa kampuni za Madini zenye mikataba na Serikali na kutoa msamaha maalum wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa makampuni ya utafiti na uchimbaji wa mafuta ya petroli na gesi, Kamati imeishauri Serikali kuendeleza majadiliano ya ziada ili tuwe na *win win situation*. Aidha, Kamati imeendelea kuishauri Serikali msamaha huo utolewe tu pale ambapo utatoa motisha kwa kampuni hizo ili kuendeleza uwekezaji nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengine yaliyojadiliwa na Kamati yanayoendana na Muswada uliowasilishwa na Serikali, Kamati imeieleza na kuishauri Serikali kuwa nchi nyingi za Afrika kama vile Afrika ya Kusini, Botswana, Ghana na kadhalika zina sera za kuhamasisha sekta binafsi, ndani ya nchi zao kushiriki katika uchimbaji wa madini. Aidha, sekta mbalimbali ndani ya nchi zao zimefungamanishwa na sekta ya madini kwa kuipatia sekta hiyo mahitaji yake muhimu ya huduma na vifaa mbalimbali. Hivyo, kuwezesha uchumi wa nchi hizo kufaidika zaidi na uwepo wa migodi ya madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba Sheria yetu mpya ya Madini inahimiza ufungamanishwaji na sekta ya madini na sekta nyingine ndani ya nchi yetu, Kamati inaishauri Serikali iangalie uwezekano wa misamaha ya kodi iliyotolewa kwa makampuni yanayochimba madini iweze kutolewa pia kwa makampuni ya hapa nchini yanayofanya kazi za ukandarasi wa uchimbaji katika migodi. Kwa kufanya hivyo tutayawezesha makampuni ya Wakandarasi ya ndani kuweza kushiriki kikamilifu katika uchimbaji wa madini badala ya utaratibu wa sasa wa unafuu wa kodi kwa wenye migodi ambao unaweka mazingira hasi kwa ushiriki wa Wakandarasi nchini. Yaani mazingira yaliyopo ya misamaha ya kodi yanahimiza utaratibu wa sasa ambao wenye migodi wanachimba wenyewe (*owner mining*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Kamati inapendekeza katika *Finance Bill* ya 2010 kuanzishwe *withholding tax* ya 15% kwa huduma za kiufundi (*technical services*) kwa makampuni ya madini yatakayo fanya uchimbaji wenyewe (*owner mining*). Kwa kuwa wakandarasi wa hapa nchini *sub contractors* wanatozwa *withholding tax* ya 5% kwa huduma za kiufundi, itakuwa ni rahisi kwa kampuni za madini kutoa fursa za uchimbaji kwa *sub contractors* wa hapa nchini. Na hivyo kuongeza fungamanisho la sekta ya madini kwenye uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hatua nzuri iliyochukuliwa na Serikali ya kupunguza ushuru wa bidhaa kwenye mafuta mazito ya kuendeshea mitambo ili kupunguza gharama za uzalishaji viwandani, Kamati imeeleza wasiwasi wake mkubwa wa vitendo viovu vya kuchakachua mafuta (kuchanganya mafuta ya taa na dizeli) vinavyoendelea nchini hivi sasa kwa baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu wa mafuta. Vitendo vya kuchakachua mafuta vina athari kadhaa:-

(1) Kujijengea utamaduni wa kutoaminika hususan na nchi jirani. Pia kuleta hofu kwa watumiaji ikiwa ni pamoja na majirani zetu wanaotumia bandari zetu;

(2) Kupoteza mapato kupitia *transit trade* na fursa za kutumia *advantage* yetu ya kijiografia ya kuwa lango kuu kwa nchi jirani;

(3) Uharibifu wa mitambo na magari yanayotumia mafuta hayo na hatimaye kusababisha gharama kubwa ya kurekebisha mitambo hiyo; na

(4) Kupoteza mapato makubwa kwa uchumi wetu mara nchi za jirani zitakapoamua kupitishia mizigo yao kupitia nchi jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ina taarifa kuwa nchi yetu inaingiza kutoka nje takriban zaidi ya lita bilioni mbili za mafuta kwa mwaka na hivyo kutufanya kuwa na matumizi makubwa ya mafuta ya taa kwa kichwa kuliko nchi yoyote Afrika (*per capital consumption*). Hiki ni kiwango kikubwa sana. Pamoja na lengo zuri lililowekwa na Serikali la kuwapunguzia wanyonge gharama za maisha kwa kupitia bei za mafuta ya taa inaonekana fursa hii inatumika vibaya na wafanyabiashara hao (tofauti kati ya bei ya dizeli na mafuta ya taa ni shilingi (450-490), hivi sasa uchumi wetu unapoteza karibu takriban shilingi bilioni 25 kila mwezi au bilioni 300 kwa mwaka kutokana na utaratibu huo, hizi ni fedha nyingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo hili baya la kuchakachua mafuta lipo Tanzania tu. Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za haraka za kukabiliana na tatizo hili la uchanganyaji wa mafuta ambalo linafaidisha wachache na kuathiri wengi pamoja na uchumi wetu. Kamati pamoja na hatua mbalimbali zitakazochukuliwa inashauri Serikali ijielekeze kwenye eneo:-

1. La kuharakisha matumizi ya ving'amuzi (*sensors*) katika biashara ya mafuta hasa hasa katika vyombo vya usafirishaji; na

2. Zoezi la kupaka rangi mafuta ya taa (*marking*) lifanyiike mapema na haraka iwezekanavyo. (*Makofi*)

Zoezi hili litajenga kuaminika kwa uchumi wetu (*Confidence building*) na washiriki wetu katika biashara yetu ya mafuta nchini na katika uchumi wetu. Kamati imeelezwa kuwa wafanyabiashara wanaochanganya mafuta ya taa na dizeli wanatenda kosa la jinai.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatimaye bado ni muhimu kwa Serikali kuwa na mapato ya kutosha kwa ajili ya kuendeleza uchumi wa nchi yetu. Kamati imeisisitiza Serikali kuendelea na hatua za kupanua wigo wa kodi ili kuongeza mapato badala ya kutegemea vyanzo vichache kila mwaka. Kamati inatumaini kuwa ushauri wa Kamati utazingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda kuwatambua Wajumbe wanaounda Kamati hii ya Fedha na Uchumi kama ifuatavyo; Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Mwenyekiti; Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mjumbe; Mheshimiwa Andrew J. Chenge, Mjumbe; Mheshimiwa Anthony Diallo, Mjumbe; Mheshimiwa Fatma Abdulhab Fereji, Mjumbe; Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mjumbe; Mheshimiwa Athuman Said Janguo, Mjumbe; Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mjumbe; Mheshimiwa Eustace Katagira, Mjumbe na Mheshimiwa Anna Maulidah Komu, Mjumbe. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Clemence B.Lyamba, Mjumbe; Mheshimiwa Dr. Binilith S. Mahenge, Mjumbe; Mheshimiwa Monica N. Mbega, Mjumbe; Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mjumbe; Mheshimiwa Felix Mrema, Mjumbe; Mheshimiwa Mossy Mussa, Mjumbe; Mheshimiwa Devota M. Likokola, Mjumbe; Mheshimiwa Damas Nakei, Mjumbe; Mheshimiwa Richard Ndassa, Mjumbe; Mheshimiwa Dr. Omary Nibuka Mzeru, Mjumbe; Mheshimiwa Suleiman Ahmed Sadiq, Mjumbe; Mheshimiwa Martha Umbulla, Mjumbe; Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mjumbe; Mheshimiwa Sijapata Nkayamba, Mjumbe na Mheshimiwa Charles Kajege, Mjumbe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, kwa niaba ya Wanakamati wenzangu naomba kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati na pia kukushukuru wewe, Naibu Spika na Katibu wa Bunge kwa kuiwezesha Kamati hii kufanyakazi ya kuchambua Muswada huu wa Sheria ya Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee naomba nimshukuru Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii pamoja na wajumbe wenzangu wa Kamati ya Fedha na Uchumi kwa michango yao katika kuboresha mijadala, maoni na mapendekezo ya Kamati. Nawashukuru sana. Napenda kumshukuru Mheshimiwa Mustapha H. Mkulo, Waziri wa Fedha na Uchumi; Manaibu Waziri, Mheshimiwa Jeremiah Solomon Sumari na Mheshimiwa Omar Yusuf Mzee; Katibu

Mkuu na wataalam wote waliotusaidia katika shughuli zetu pamoja na kuuchambua Muswada huu. Kamati inawashukuru sana na kuwatakiya mafanikio makubwa katika kazi za ujenzi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Ndugu Michael Kadebe na Ndugu Lawrence Robert Makigi kwa kazi nzito ya kuihudumia Kamati hii ikiwa ni pamoja na kuandaa maoni ya Muswada huu kwa wakati unaotakiwa nawashukuru sana. Mwisho, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja hii.
(*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana na sasa nitamwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusiana na Wizara hii. Namwona Mheshimiwa Ismail Jussa kwa niaba ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani ambaye ndiye Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani katika Wizara hii ya Fedha.

MHE. ISMAIL JUSSA LADHU - KIONGOZI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Naibu Spika, utangulizi. Awali ya yote ningependa kutumia fursa hii kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kwa niaba ya Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani na Waziri Kivuli wa Wizara ya Fedha na Uchumi kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2010 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, kanuni ya 86(6), Toleo la 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru pia Waheshimiwa Wabunge wote wa Kambi ya Upinzani pamoja na watu wote ambao kwa njia moja ama nyingine wametoa mchango wao katika kufanikisha hotuba yetu ya Bajeti Mbadala kwa mwaka wa fedha 2010/2011. Kupitia Bunge hili Tukufu, natoa ahadi kwa niaba ya Kambi nzima kuwa tutaendelea kutetea maslahi ya Watanzania wote kwa ujumla kama ambavyo tumekuwa tukifanya siku zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuzungumzia vifungu mahsusi vya Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2010, napenda kueleza maoni ya jumla ya Kambi kuhusiana na maudhui ya Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2009 (Ukurasa wa 5), sehemu ya Ongezeko la Ukusanyaji Kodi inasema: “Wahusika wote katika ukusanyaji wa kodi wanatakiwa kufanya kazi hiyo kwa juhudi kubwa zaidi ikizingatiwa kuwa hadi sasa makusanyo ya mapato yako chini ya asilimia hamsini (50%) ukilinganisha na fedha inayotakiwa kukusanywa kutoka kwenye vyanzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na migodi, utalii, bidhaa za kilimo, biashara na

kadhhalika. Ukwepaji wa kulipa kodi pamoja na kulipa kodi kidogo, kutumia mianya ya udhaifu wa sheria zilizopo imekuwa ni desturi ambayo inastahili kupigwa vita”.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuthibitisha hayo kwa mujibu wa Taarifa ya Msajili wa Hazina iliyonukuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, hadi kufikia tarehe 30.6.2009 kulikuwa na mashirika ya umma yenye madeni yaliyofikia shilingi 102.5 bilioni ambayo ni sawa na asilimia 25 ya bakaa yote ya madeni iliyodhaminiwa na Serikali ambayo yalitakiwa yalipwe ifikapo tarehe 30.09.2009. Wakati huo kulikuwa na bakaa ya mapato ya shilingi 110.1 bilioni ikijumuisha na shilingi 93.4 bilioni ya deni la zamani ambalo hadi leo halijalipwa, hivyo kufanya jumla kuwa Tsh. 203.5 bilioni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na taarifa hiyo, matumizi yote ya Serikali ya kawaida na maendeleo kwa Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala wa Serikali na Serikali za Mitaa kwa mwaka 2007/2008 na 2008/2009, hesabu za matumizi (*Expenditure Account*) iliongezeka kutoka shilingi 3.7 trilioni 2007/2008 hadi shilingi 4.9 trilioni, sawa na ongezeko la 34% wakati matumizi ya maendeleo yaliongezeka kutoka shilingi 1.3 trilioni hadi shilingi 1.6 trilioni sawa na ongezeko la asilimia 20.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini taarifa ya mapato yasiyokusanywa yameongezeka kwa kiwango cha kutisha kutoka shilingi 789.2 milioni kwa mwaka wa 2007/2008 hadi kufikia shilingi 10.02 bilioni sawa na asilimia 1,170. Hiki ndicho kiwango cha udhaifu wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeanza na utangulizi huu kwa sababu Serikali imekuwa inaongeza kodi kila uchao hasa kwa Watanzania maskini, lakini inashindwa kubana mianya ya kukwepa kodi hadi kufikia kiwango hicho cha kutisha cha asilimia 1,170. Katika hali kama hii, ni dhahiri nyongeza hizi ni za kumwongezea mzigo mlaji, Mtanzania maskini, badala ya kumwendeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani imekuwa ikiishauri Serikali wakati wote kuwa ipunguze misamaha ya kodi kwa angalau asilimia 50. Mara zote Serikali imekuwa ikidai kuwa wanalifanyia mkakati suala hili lakini ukiangalia hali halisi hakuna kinachofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirejee kauli ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwamba, ili Serikali iweze kuongeza mapato inapaswa ipunguze misamaha ya kodi, hasa ukizingatia ukweli kwamba misamaha hiyo ya kodi jumla yake ni shilingi 752 bilioni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali ingekuwa na nia ya dhati ya kuwaondolea kodi kama za pikipiki na gari za boda boda, ingeweza kufanya hivyo kwa kufidia kiwango hicho cha mapato kwa kupunguza angalau asilimia 50 ya misamaha, ambayo itafanya si chini ya shilingi 376.2 bilioni. Maelezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) yanaonyesha mchanganuo wa misamaha hiyo ya kodi kama ifuatavyo:-

Taasisi Jumla	Idara ya Forodha Shs.	Idara ya kodi ya Ndani Shs.	
Shs. Taasisi za Serikali	21,617,300,000		21,617,300,000
Mashirika ya umma	7,125,600,000	7,125,600,000	
Taasisi za Kidini	408,000,000		408,000,000
Taasisi zisizo za Kiserikali	37,237,700,000	37,237,700,000	
Miradi ya wafadhili	21,552,700,000	21,552,700,000	
Makampuni na watu binafsi	51,236,400,000	51,236,400,000	
kituo cha uwekezaji (TIC)	380,090,500,000	380,090,500,000	
Misamaha ya Kodi na ongezeko la thamani 170,097,500,000		170,097,500,000	
Misamaha ya kodi katika maduka yasiyotozwa kodi		3,892,400,000	3,892,400,000
JUMLA	578,408,900,000	173,989,900,000	752,398,800,000

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani haikubaliani na hatua ya kusamehe kodi makampuni ya madini kama inavyopendekezwa na Serikali kwa kutaka kurekebisha Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 148.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kitabu cha Mapato (*Revenue Book*) fungu la 137, hakuonekani mapato yoyote mwaka huu kutokana na leseni za uvuvi. Uvuvi wa ukanda wa pwani huwa na wastani wa meli 15-20 zinazovua kamba (*prawns*) ambazo kila moja inalipia leseni ya wastani wa USD 18,000. Kuvua wastani wa tani 80 -100 kwa mwaka, Serikali hutoza asilimia tano kama mrahaba kwa samaki wanaovuliwa. Kambi ya Upinzani tunajiuliza ni kwa nini kitabu cha Mapato kisionyeshe angalau mapato haya? Umakini wa kukusanya mapato uko wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata katika uvuvi unaofanyika kwenye bahari kuu, Serikali haikusanyi mapato kwenye meli zinazovua huko. Wastani wa meli zinazovua huko ni 150 - 170 na zina uwezo wa kuvua wastani wa tani 500 – 2,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hivyo basi, kama Serikali ingeiwezesha Wizara ya Uvuvi na Mifugo ingeweza:-

(a) Kuongeza mapato kutokana na leseni za uvuvi wa bahari kuu na bahari ndogo ambao kwa mujibu wa *Revenue Book* mwaka huu hakuna makusanyo kabisa pamoja na kwamba zipo meli zinazovua.

(b) Tungeweza kupata *levy* ya asilimia tano kutokana na mauzo ya wastani wa tani 100 za kamba (*prawns*).

(c) Tungeweza kuongeza ada ya leseni kutoka USD 18,000 hadi USD 30,000 ambazo hazikusanywi kwa sasa.

(d) Tungeweza kupata *levy* ya asilimia mbili ya samaki wanaovuliwa bahari kuu ambapo wastani wa meli 150-170 zenye uwezo usiopungua tani 500 - 2,000 zinavua na kuondoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wazi kuwa kama Serikali ingekuwa sikivu tungeweza kukusanya si chini ya Tsh. 130 bilioni. Serikali haifanyi hivyo na badala yake inakimbilia kuongeza leseni ya boda boda ya shilingi 10,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya Muswada. Naomba sasa kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Fedha wa mwaka 2010 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mabadiliko katika Sheria ya Korosho, Sura ya 203, Kambi ya Upinzani inaona kuwa kwa ajili ya kutoa motisha zaidi kwa wafanyabiashara kusafirisha korosho ambazo tayari zimebanguliwa na hivyo kuongeza thamani ya bidhaa tunazouza nje na pia kutoa ajira kadhaa kwa wananchi ni bora wangepewa unafuu kadhaa katika kodi za ndani. Kwani ushuru wa usafirishaji wa korosho ghafi nje wa kulipa USD 160 kwa tani moja ingekuwa ni bora uongezwe ili

kusitisha usafirishaji wa korosho ghafi. Wakati huo huo, Serikali ikae na viwanda vya kubangua korosho, ili visaidiwe kutoka tani 17,000 zinazobanguliwa sasa ifikie angalau tani 50,000 kwa mwaka. Maana kuzuia usafirishaji wa korosho ghafi, hakusaidii kama hakuna ongezeko la viwanda vya kubangua korosho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mabadiliko katika Sheria ya Ushuru wa Bidhaa za Ndani, Sura ya 147, kifungu cha 9 cha Muswada kinachofanyia marekebisho Jedwali la Nne, *H.S. Code No. 2201.10.00* na *H.S 2202.90.00* vinavyohusiana na kupandishwa kwa sh. 5.00 kwa kila lita ya maji na vinywaji baridi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaona pendekezo hili la Serikali badala ya kuviinua viwanda vyetu hasa vile vinavyotengeneza *juice* za matunda kwa bidhaa zake kuweza kununuliwa na wananchi wa kada zote za maisha, inavikandamiza. Hali ya umaskini kwa wananchi inazidi kuwa mbaya hivyo bei kupandishwa kidogo maana yake ni kwamba kundi kubwa la watumiaji watashindwa kununua, na wakishindwa kununua viwanda vitashindwa kuendelea na uzalishaji kwani mzunguko wa bidhaa utasimama. Je, tunavilinda viwanda vyetu au tunaviua?

Mheshimiwa Naibu Spika, mabadiliko yanayofanywa katika Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332, kifungu kipya cha 80A kinachoongezwa cha kumtaka: “Yeyote atakayenunua bidhaa za zaidi ya sh. 5000/- kupatiwa risiti ambapo risiti hiyo inatakiwa pia iwe na anuani ya mnunuzi”. Sote tunaelewa Watanzania walio wengi ambao ndio watakaofanya manunuzi haya ya sh. 5,000/- hawana anuani halisi za makazi kutokana na ukweli kuwa utaratibu wa anuani za mitaa haujawekwa na nchi yetu, hivyo basi kifungu cha 80A(2)(d) utekelezekaji wake utakuwa ni mgumu sana kama si kutotekelezeka kabisa, jambo ambalo tunaona litasababisha kughushi nyaraka husika. Mwisho wake ni kutiwa hatiani na kifungu kipya cha 17(3).

Mheshimiwa Naibu Spika, pili kwa kuwa kuna utaratibu wa kutumia mashine za kutoa risiti (*electronic fiscal receipts*) ambao umekwishatangazwa kuanzishwa na TRA, hivyo basi tunadhani TRA iweke utaratibu wa kuwakopesha wafanyabiashara wadogo ambao hawana uwezo wa kununua mashine hizo ili wawe wanalipa kidogo kidogo kadri biashara zao zitakavyokuwa zinakua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mabadiliko ya Sheria ya Magari (Usajili na Uhamisho wa Miliki), Sura ya 124, vifungu vya 24(a) na 24(b) vya Jedwali la Kwanza, vinavyoongeza viwango vya ada za usajili wa magari na pikipiki, Kambi ya Upinzani haikubaliani na jambo hili kabisa kwani badala ya kumpunguzia mwananchi adha ya usafiri, ongezeko hili litazidisha gharama za bei ya nauli kwa pikipiki na bajaji na pia taxi. Hivyo basi, Kambi ya Upinzani inaliona ongezeko hili halileti tija katika kumsaidia mwananchi wa kawaida wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mabadiliko yanayopendekezwa kwenye Sheria ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148, kifungu cha 43 kinachofanya marekebisho kwenye Jedwali la Pili, kwa ujumla marekebisho hayo ni kuwanufaisha zaidi wafanyabiashara na wawekezaji katika sekta za kilimo na mifugo. Kambi ya Upinzani

inataka kuelewa unafuu huo unamnufaisha vipi mzalishaji, mkulima na mfugaji ili na yeye aweze kuzalisha kwa moyo? Au Kilimo Kwanza kimekusudia kuwanufaisha wawekezaji na wafanyabiashara wa sekta hizo badala ya wakulima na wafugaji walioko vijijini?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaona ingekuwa ni vyema unafuu unaopatikana kutokana na punguzo hilo au msamaha wa VAT basi mfanyabiashara katika sekta husika, nusu yake irudi kwa mkulima kama motisha ya kuzalisha zaidi. Lakini ukiacha hayo, Kambi ya Upinzani ingependa pia kuona sekta ndogo ya uvuvi pia inajumuishwa katika unafuu ili kuwanufaisha wananchi wanaoishi kando ya bahari au maziwa ambao wanajishughulisha na uvuvi kama njia ya kuendesha maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la mwisho la kulizungumzia ambalo ni muhimu sana ni lile linalohusu mabadiliko yanayopendekezwa kwenye Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 148, ili kutoa msamaha wa ushuru wa bidhaa za petroli kwa Kampuni za Madini zilizosaini mikataba na Serikali. Kambi ya Upinzani imeshangazwa na hatua hii kwani misamaha hii ilikuwepo na iliondolewa katika bajeti ya mwaka jana lakini sasa Serikali imeamua kuirudisha.

Hoja iliyotolewa na Serikali ni kwamba inafungika na mikataba iliyosaini yaani *MDA's*. Kambi ya Upinzani siyo tu kwamba inashangazwa kwamba Serikali haikuiona hoja hii wakati inafuta misamaha hii mwaka jana bali pia inashindwa kuamini kama Serikali ikidhamiria kweli inashindwaje kujadiliana na kampuni zinazohusika ili waone haja ya Watanzania pia kufaidika na sekta hii ya madini. Hivi mikataba ya *MDA's* imekuwa na nguvu hata ya kulinyang'anya Bunge mamlaka yake ya kuanzisha na kufuta kodi katika nchi yetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa msamaha huu unasaidia Kampuni za Madini kuzalisha umeme wao kwa kutumia mafuta ambapo kampuni zimetoa zabuni kwa kampuni binafsi za kuzalisha umeme kutoka nje, hapatakuwa na vivutio vya kuongeza uzalishaji wa umeme nchini na kulifanya Shirika la *TANESCO* kuuza umeme wake kwa migodi ya umeme. Msamaha unaua dhana nzima ya fungamanisho la sekta ya Madini na sekta ndogo ya Umeme. Katika muundo wa gharama za Kampuni za Madini (*cost structure*), gharama za umeme ni asilimia 13 ya gharama za uzalishaji ambazo kwa kuwarejeshea misamaha hii sasa fedha hizi zitakwenda kwa kampuni binafsi za nje zilizopewa zabuni za kuzalisha umeme kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande mwingine, kwa kuwa msamaha huu hautahusisha wakandarasi wa ndani wanaofanya biashara na Kampuni za Madini (*local contractors na sub contractors*), hivyo hapatakuwa na vivutio kwa kampuni za madini kutumia wakandarasi wa ndani. Kampuni za madini zitaona ni rahisi zaidi (*less costly*) kufanya shughuli ya kuchimba wenyewe (*owner mining*). Hii itaua dhana ya fungamanisho kati ya sekta ya madini na sekta ya ujenzi (*construction*) ambayo ilikuwa ni miongoni mwa madhumuni ya Sheria mpya ya Madini iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu katika Mkutano uliopita tu, ili kujibu changamoto ya fungamanisho dogo la sekta

ya Madini na sekta nyingine za Uchumi (*low integration of the mining to other sectors of the economy*). Katika muundo wa gharama za uzalishaji kwa Kampuni za madini, takribani asilimia 30 ni gharama za kuchimba.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuifanya nchi yetu na watu wake wafaidike na rasilimali za madini yaliyomo nchini na pia kuifanya sekta ya madini ichangie zaidi katika Pato la Taifa, Kambi ya Upinzani inapendekeza msamaha huu wa bidhaa za mafuta uendelezwe pia kwa kampuni za ujenzi katika migodi ambazo ni wakandarasi wa ndani (*local contractors*). Utafiti unaonyesha jumla ya kampuni hizo za wakandarasi wa ndani ni saba na hivyo kuwa na uwezo wa kutoa mchango wa kutosha katika pato la nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuzidi kuifanya nchi inufaike na sekta ya madini na kuongeza mapato ya Serikali, Kambi ya Upinzani inaitaka pia Serikali isimamie vizuri utekelezaji wa Sheria ya Usajili wa Wakandarasi (*The Contractors Registration Act*) ya 1997 ambayo inataka Bodi ya Usajili wa Wakandarasi (*Contractors Registration Board*) kusajili kampuni za nje zinazotaka kutoa huduma hapa nchini kama matawi ya kampuni zao mama zilizosajiliwa nje ya nchi badala ya kuziruhusu kujiandikisha hapa nchini kama kampuni tanzu (*locally incorporated as a subsidiary company*). Kumekuwa na mwanya mkubwa kwa upande wa *CRB* kuruhusu kampuni hizo kujisajili kama kampuni tanzu zilizosajiliwa hapa nchini na hivyo kutambuliwa kama kampuni za ndani na hivyo kuikosesha Serikali mapato kwa kukwepa kulipa kodi ya zuio (*withholding tax*) ya asilimia 15 wanayopaswa kulipa kama wakandarasi wa nje na badala yake kulipa kodi hiyo ya zuio kwa asilimia tano tu wanayopaswa kulipa wakandarasi wa ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuruhusu ukiukwaji wa Sheria hii ya Usajili wa Wakandarasi ya 1997, Serikali inapoteza mapato mengi kutoka kwa wawekezaji wa sekta ya madini na badala yake inakimbilia kuwakamua wananchi maskini. Mfano ni kwamba ukiwa na wakandarasi 10 wa nje waliachiwa kujisajili kama wakandarasi wa ndani na hivyo kulipa kodi ya zuio ya asilimia tano badala ya asilimia 15 na hawa kila mmoja akafanya kazi yenye gharama ya USD 30 milioni, jumla yake itakuwa ni USD 300 milioni. Wanapokwepa kulipa tofauti ya kodi ya zuio ya asilimia 10 kutoka kiasi hicho cha jumla, hiyo maana yake Tanzania imekosa mapato ya USD 30 milioni ambazo ni kiasi cha shilingi 45 bilioni za Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiki ni kiasi kikubwa sana kwa nchi yetu kupotea hivi hivi. Ni sawa na ile hadithi ya kuruhusu kulipwa kwa midimu na mibaazi huku utajiri wa nchi ukiendelea kumalizika. Nchi yetu haimudu upotevu huu na tunazihitaji fedha hizi kwa kuziba nakisi iliyopo katika vyanzo vyetu vya mapato ya ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hili pengine kuna haja pia ya Sheria hii ya Fedha kuanzisha kodi ya zuio (*withholding tax*) ya asilimia 15 kwa huduma za kiufundi kwa kampuni za madini zitakazofanya uchimbaji wenyewe (*owner mining*). Kwa kuwa wakandarasi wa ndani wanatozwa asilimia 5 ya kodi ya zuio kwa shughuli kama hizi za kiufundi, itakuwa ni rahisi (*cheap*) kwa kampuni za madini kutoa zabuni

kwa kampuni za ndani kama ambavyo pia ilipendekezwa na Kamati ya Fedha na Uchumi ambayo imesoma taarifa yake punde.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, Kambi ya Upinzani inapenda kulikumbusha Bunge lako Tukufu kwamba Watanzania wamechoka kuishi kwa matumaini chini ya sera za Chama Cha Mapinduzi zinazowakatisha tamaa huku wakiendelea kusota katika umaskini wakati nchi yao ni tajiri wa rasilimali zinazoweza kuanzisha vyanzo vingi vya mapato badala ya kuendelea kuwakamua wao kupitia vyanzo hivyo hivyo kila mwaka vya soda na vinywaji vingine baridi, vileo, sigara na ada za leseni za magari na pikipiki.

Kambi ya Upinzani inadhani wakati umefika wa Serikali ya CCM kuacha kumkamua ng'ombe ambaye sasa anatoa damu badala ya maziwa. Tuwe tayari kutumia vyanzo vingine vya mapato ambavyo vitamnufaisha Mtanzania badala ya kuendelea kumkandamiza. Vinginevyo, watakuwa na haki ya kutafuta mbadala utakaowaletea maisha yenye neema kwao na kwa vizazi vyao chini ya misingi ya haki sawa kwa wote na uchumi imara unaotoa ajira na tija kwa wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, iwapo Serikali itakubali kufanya marekebisho tuliyo yapendekeza kwa maslahi ya nchi yetu na watu wake, Kambi ya Upinzani itaiunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana kwa mawasilisho yako ambayo yametumia muda unaopaswa. Waheshimiwa Wabunge, mpaka sasa tunao wachangiaji wanane, lakini leo siku nzima ni ya kujadili Muswada huu, kwa hiyo wale wanaofikiria wangependa kuchangia orodha bado haijafungwa.

Sasa kwa wale waliojiandikisha, kwanza nitamuita Mheshimiwa Godfrey Zambi, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed, halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga. Mnaona ninakwenda taratibu najaribu kutopanga watu wa aina moja wakati huo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Zambi karibu.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuwa mchangiaji wa mwanzo wa Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2010, *The Finance Act 2010*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, Mustafa Mkulo, Manaibu wake pamoja na Katibu Mkuu na Manaibu Katibu Wakuu pamoja na Wataalam wote wa Wizara kwa kutuandalia bajeti nzuri ambayo tumeipitisha jana, nampongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia naomba nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuwasilisha Muswada huu mbele ya Bunge lako Tukufu ili tuweze kupitisha na kwa maana hiyo bajeti tuliyopitisha jana iweze kufanya kazi.

NAIBU SPIKA: Amewasilisha Waziri mwenyewe.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia maeneo machache sana kama ifuatavyo kwani mambo mengi muhimu yameishawasilishwa na wasemaji ambao wamepita na mimi nitachangia kwa ufupi sana maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni Sura 332, sehemu ya (5), Marekebisho katika Sheria ya Mapato. Jambo ambalo nimeliona hapo na linapaswa tuweze kulijadili na pengine kuishauri Serikali ni utaratibu ambao unataka wafanyabiashara kutoa stakabadhi katika mauzo kwa lengo la kupata ankara sahihi ya walipa kodi katika nchi hii. Hili naona ni hatua nzuri na ni jambo jema ambalo linaweza likaifanya Serikali iweze kupata mapato zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nina wasiwasi na maeneo kadhaa kama kweli yanafuatiliwa vizuri na kwa maana hiyo kuipatia Serikali mapato. Kwa mfano, leo ukienda kwenye vituo vya mafuta, unaulizwa unataka risiti au hutaki risiti? Uchague wewe mwenyewe, uende kutengeneza gari katika gereji, unaulizwa unataka risiti au hutaki risiti? Maana yake kama unataka risiti pale ndipo kunapokuwa na VAT, ile pesa ambayo inakwenda Serikalini. Lakini kama hutaki risiti maana yake unalipa ile hela tu bila VAT.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo naona pia Serikali inapoteza pesa maana udhibiti wake siuoni sawasawa ni sehemu ya maduka ya kubadilisha fedha za kigeni. Wengi tunakwenda kwenye maduka ya kubadilisha fedha za kigeni, unanunua pesa dola au pesa yoyote unayotaka kununua lakini maduka mengi hayatoi risiti. Nadhani Serikali kupitia maeneo hayo inapoteza pesa nyingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ukiangalia kwenye vituo vya mafuta, kwenye maduka ya kubadilisha fedha za kigeni, ukienda kwenye magereji na maeneo mengi hakuna utaratibu mzuri wa Serikali kufuatilia kwamba, watu hawa wanalipa kodi inayostahili. Kwa hiyo, labda Waziri atatueleza hapa wanafuatilia na kudhibiti namna gani pesa zinavyopotea katika maeneo hayo maana nimeyaona wazi kabisa pale ambapo unaulizwa *whether* unataka au hutaki risiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hatua nzuri hizi, Serikali itafanya jitihada gani kuhakikisha watu wote katika maeneo yale ambayo tunaona yanakwepa kodi waziwazi wanaweza kulipa kodi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia naomba nizungumzie jambo la marekebisho yanayolenga kumlazimisha huyu mfanyabiashara, jambo ambalo wenzangu

wamelizungumza. Hawa wafanyabiashara ambao wanapokea zaidi ya shilingi 5000/= kwa kulazimishwa watoe stakabadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sijui kama tunafanya mambo mengine kwa kuwa na uhakika nayo. Leo wapo Wamachinga ambao wanapitisha bidhaa barabarani, hawa tunawadhibiti namna gani maana nina hakika wanafanya biashara ya zaidi ya shilingi 5000/=. Wanatoaje risiti? Tunaweka mazingira gani? Lakini lazima tuseme hawa ni Watanzania wa kawaida sana, lakini nadhani kuna maeneo mengi ambayo watu wanaachwa kutozwa kodi tunawafuata watu wadogowadogo sana ambao wanatafuta pesa kwa ajili ya kujikimu. Nadhani kiwango kilichowekwa ni kidogo sana na Serikali iangalie namna ya kurekebisha eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni ushuru wa mazao shambani 3% mpaka 5%. Mimi, Mbozi tunalima kahawa sana, bado mpaka leo tunatoza kodi hiyo kati ya 3% na 5%, lakini naona tunatoa mwanya kwa Halmashauri kuweza kupanga kodi inavyoona inafaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili kwa Wilaya ya Mbozi lilileta utata mkubwa sana kwa wakulima wa kahawa kulalamika kwa sababu Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi ilikuwa inatoza ushuru wa 5% na Halmashauri nyingine zinazolima kahawa hiyo hiyo zilikuwa zinatoza ushuru wa chini ya 5%. Sasa wafanyabiashara na wakulima wa kahawa wakawa wanafuatilia kwanini kodi ya kahawa inatofautiana pamoja na kwamba Halmashauri zina tofauti? Kukawa na mabishano makubwa na mimi kama Mbunge nililazimika kuingilia kati na kwa kweli nilimwona Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI na nilishughulika sana na Mheshimiwa Mwanri katika kuhakikisha kwamba tunaleta mapatano kati ya wakulima wa kahawa na viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninachoona hapa ni kutoa mwanya wa Halmashauri. Halmashauri zingine bado zinaweza zikatumia mwanya huu kwa ajili ya kuwakomoa wakulima na kwa hiyo tukasababisha mapambano ambayo hayana sababu ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali iangalie utaratibu mzuri zaidi pamoja na nia nzuri ya kutoza kodi hiyo lakini kuacha wigo tu kwamba kila Halmashauri itoze inavyotaka kati ya 3% na 5% naona pengine tutakuwa tunawaweka viongozi wa Halmashauri katika wakati mgumu ambao unaweza kusababisha pia watu wasielewane kulekule chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Magari, Sura 124 ambayo inalenga kubadilisha ada ya usajili na uhamisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule vijijini usafiri unaotumika sana ni magari yale ya *Pickup*, lakini zaidi siku hizi tunatumia sana pikipiki. Wenzangu wengi wamezungumza na niliona ni jambo muhimu lazima nilizungumze.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nishauri kwamba, Serikali badala ya wakati wote kuamua kupandisha viwango vinavyolenga kuwakamua zaidi wananchi wadogo hebu tupandishe kodi kwenye magari makubwa kwa mfano, gari kama vile *VXs*, *Benz*, *BMW* na magari mengine ambayo ni ya starehe kuliko kupandisha ushuru na ada kwenye usafiri kama wa pikipiki pamoja na magari haya kama ya *pick up*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwatendei haki Watanzania. Kule Mbozi kuna eneo fulani wanaita Karasha-Ivwanga, ni njia panda ya kwenda Mbozi *Mission*. Wananchi wanaokwenda hospitali ya Mbozi *Mission* walikuwa wanapata tabu kwa kulazimika kutembea karibu kilomita saba kwa mguu kwa sababu palikuwa hapana usafiri pale. Walikuwa wanatumia usafiri wakati mwingine wa baiskeli na wananchi walikuwa wanaanguka na kuumia sana. Lakini kwa kuja hizi pikipiki za Wachina, zimekuwa mkombozi, vijana wa pale wamejiunga wengi wamenunua pikipiki na leo wananchi wanaokwenda hospitali wamepata nafuu kubwa sana. Sasa leo tunapopandisha ushuru wa pikipiki maana yake tunataka wenye pikipiki zile pia wapandishe nauli kwa ajili ya wananchi hawa wa kawaida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani katika eneo hilo Serikali ifikirie kuhamisha kodi kwenda kwenye maeneo mengine kama nilivyosema, kwa mfano, kwenye magari makubwa *VXs*, *Benz*, *BMW* na magari mengine maana hayo ni magari ya anasa ambayo hayawasaidii Watanzania wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo napenda nichangie ni marekebicho ya Fedha za Umma, Sura 348. Nimeona tunaanzisha Idara mpya ya Usimamizi na Ukaguzi wa Ndani. Ni jambo jema lakini pia nafurahi kwamba Mkaguzi Mkuu atakuwa anateuliwa na Rais. Lakini kama hatutampa uwezo wa kusimamia yale mapungufu atakayompa kwa maana ya kumpa utaratibu wa kisheria kuwadhibiti wale atakaowakuta wana makosa tutakuwa bado hatujafanya jambo jema sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyo leo kwa *CAG* pamoja na kwamba nimeona katika Sheria hii *CAG* sasa anapewa nguvu za kisheria za kushughulika na wale ambao atakuta wamehusika na ubadhirifu. Kwa hiyo, naomba na huyu Mkaguzi Mkuu wa Ndani, ambaye sasa Sheria hii inamuanzisha basi apewe nguvu za kisheria kuweza naye kukabiliana na yale ambayo atayabaini kama mapungufu kutoka katika Wizara na Idara mbalimbali za Serikali, tusipofanya hivyo tutakuwa tunazidi tu kuuweka mzungu kwa Serikali wa kuanzisha vyombo vingi ambavyo haviwezi kufanya kazi zake sawasawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ambalo ningependa nilizungumze ni marekebicho ya Sheria za Miji. Kurekebisha Sheria hii tunalenga kuwasaidia wazee wale wa miaka sitini (60) ili wasiweze kulipa kodi za majengo wanayoishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kwenye ilani ya Chama Cha Mapinduzi, tumeweka kifungu ambacho kinawapa nafuu wazee wasiweze kulipa gharama za matibabu, leo tunakuja na Sheria hii ya Fedha tunataka tuwape wazee unafuu kwenye kulipa kodi za majengo. Jambo hili ni jema lakini badala ya kuwa na visheria vingivungi,

naishauri Serikali hebu ije na Sheria moja ambayo itatoa mapendekezo au unafuu wa kodi unaowalenga wazee katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, nataka nipendekeze iletwe sheria hiyo lakini ikitaja wazee hawa wasamehewe matibabu, michango mbalimbali, wapate nafuu katika vyombo vya usafiri, lakini pia ununuzi, mathalani wale wanaojishugulisha na kilimo wapate msamaha hata katika ununuzi wa vocha za kilimo ambazo tunawasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ikija sheria moja ambayo inaangaalia maeneo yote haya tutakuwa tumewasaidia, kuliko leo tunakuja na msamaha katika sheria ya majengo, kesho tutakuja tutasema msamaha katika sheria nyingine, haitapendeza sana. Kwa hiyo, naishauri Serikali iletwe sheria moja na ianishe maeneo mbalimbali ambayo tunafikiri wazee hawa wanaweza wakasamehewa ili waweze kuishi vizuri zaidi katika nchi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa na mchango huo mdogo tu. Naomba niunge mkono hoja hii ya Muswada wa Sheria ya Fedha, nashukuru sana. (*Makofi*)

MHE. HAMAD RASHID MOHAMMED: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza niungane na Waziri kwamba mapendekezo haya aliyoyaleta yatasaidia kwa kiasi fulani, lakini moja ambalo ningependa niliseme ni kwamba sheria zipo lakini ukaziaji wa sheria zenyewe ndiyo tatizo kubwa la msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo la kwanza, ningependa Serikali itafute utaratibu sasa wa kusimamia hii sheria kwa sababu marekebisha ya kuziba mianya ya kukwepa kulipa kodi tumeyafanya mengi sana lakini bado ukiangalia Taarifa ya Mdhidhi na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG), bado tunaona kuna mianya mingi ya watu kuweza kukwepa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ina maana kwamba usimamiaji wa sheria yenyewe bado haujakuwa mzuri, kwa hiyo, tunafanya mabadiliko ya sheria, tunaweka vikwazo vingi ndani ya sheria lakini usimamiaji wake bado haujakuwa mzuri. Hilo ni jambo la kwanza ambalo ningependa kulisema.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, nilisikitika sana nilipoangalia *revenue book* na kuona kwamba katika sekta ya uvuvi hakuna mapato yaliyooneshwa. Nimestuka sana, nimestuka kwa sababu naelewa kwamba, kuna aina tatu za vyombo ambavyo vinavua baharini, ukiacha kwenye ziwa. Kuna meli zile za *trawlers* ambazo tunazikuta pale Dar es Salaam ziko kama 15 mpaka 20, huwa zinapata lesseni zinakwenda kuvua, halafu kuja pale bandarini kupakua samaki wao na kuuza na Serikali inakusanya 5% ya ushuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nasikitika sana kuona kwamba katika *revenue book* haonekani kama kuna mapato ya aina yoyote yanayotoka kwenye *fisheries*. Hapa nafikiri kuna tatizo la msingi ambalo linahitaji kuelezwa na Waziri ni kwa nini katika sekta hii ya uvuvi mara hii hainonekani kama kuna mapato katika *revenue book*, ama

kuna tatizo la uchapishaji au kuna tatizo gani la msingi kuonesha kwamba hakuna mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini baya zaidi ni kwamba, baharini kuna meli si chini ya 150 au 120 zinavua na bahati nzuri katika Jimbo langu la Wawi niko katika *Deep Sea*. Kila siku ukisafiri na ndege utakuta si chini ya meli tano au sita ziko katika ukanda huo zinavua. Sasa meli hizi zina wastani wa tani 500 mpaka 2000 na katika meli hizi hakuna zinazovua chini ya miezi mitatu mpaka minne mfululizo. Kwa hivyo, wastani wa kupata tani 500 mpaka 600 upo mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa tumeishauri Serikali, wala haihitaji kutumia vyombo vya ulinzi wala nini, wakati mnapowapa leseni ambapo mnawatoza dola \$18,000/= kwanza tunashauri kwa nini iwe dola 18,000/? Miaka mingi sana imekuwa kiasi hicho, ifanywe dola 30,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili unapowapa leseni uwaambie kwamba samaki mnaokwenda kuvua sisi tunakisia kama meli yako ina uwezo wa tani 500 utavua tani 150. Katika tani 150 tupe ushuru wa 2% ya samaki hao mapema, umepata tani 500 au 600 wewe shauri yako. Kwa sababu huna vyombo vya kuweza kuwadhiti kule, hiyo ndiyo njia rahisi ya kuweza kupata mapato yako, Namibia wanafanya hivyo na nchi nyingine nyingi. Hakuna haja ya kutafuta boti za ulinzi wala nini, ni utaratibu tu wa kutoa leseni na kuwabana palepale upate pesa zako za kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa nini inashindwa kufanya hili? Tumeshauri miaka mingi, Waziri jana anasema ushauri tuulete mapema, tumeuleta miaka mingi lakini Mheshimiwa Waziri, hautekelezi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili., kuna meli hizi zinazovua kimagendo. Hizi meli zinazovua kwa magendo ukishirikiana na nchi nyingine za jirani katika utaratibu wa *SADC* unaweza kuzibana kabisa na ukapata mapato kutokana na samaki. Tumeona ile meli iliyokamatwa juzi na Mheshimiwa Magufuli pale, pamoja na Serikali kusema imepata hasara pale, kile kitendo cha kukamatwa ile meli ni kuthibitisha kwamba tunaibiwa raslimali zetu kwa idadi kubwa sana.

Hili ni jambo jema kabisa, kwamba huku kukamatwa kwa meli *whether* mmepata hasara au faida lakini tumethibitisha kweli tunaibiwa kwa kiwango kikubwa raslimali zetu, ni jambo jema tufanye utaratibu wa kuweza kudhibiti wizi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu ni misamaha hii ya madeni. Ukiangalia taarifa ya Mdhiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (*CAG*) maeneo ambayo tunatoa misamaha ni mengi. Kuna taasisi za Serikali karibu shilingi bilioni 21, Mashirika ya Umma karibu shilingi bilioni 7, Taasisi za Kidini shilingi milioni 808, Taasisi zisizo za Kiserikali shilingi bilioni 37, miradi ya Wafadhili shilingi bilioni 21, Makampuni ya watu binafsi shilingi bilioni 51, Kituo cha Uwekezaji shilingi bilioni 380, misamaha ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*) shilingi milioni 170, Misamaha ya Kodi katika Mashirika yasiyotowza kodi ni kama shilingi bilioni 3. Jumla ni shilingi bilioni 752.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachosema hebu kakaeni mkokotoe, mashirika haya yote hatuwezi kupunguza 50%? Kaeni *seriously* mnaweza mkapunguza 50% ya hii, haya ni mapato makubwa ya Serikali, kwanini hili linakuwa na kigugumizi? Mimi sioni sababu ya kuwa na kigugumizi hivi, badala yake tunakwenda kutoza kodi ya shilingi 10 kwenye boda boda itatusaidia nini, tunaacha *billions and billions of moneys* zinapotea bure? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema Serikali kaeni *seriously*, kaeni na watu hawa msememe jama hapa kuna tatizo na njia nyingine tulifanya hapo nyuma, tulivyowaambia hawa watu tunawasamehe, lipeni halafu tuwarudishie. Tulipofanya utaratibu ule watu wengi walikwepa kwa sababu kuna udanganyifu katika kusamehe kodi, kwa hiyo unapomwambia mtu lipa *in advance* halafu wewe njoo uchukue *refund*, hakuna anayefanya hivyo, matokeo yake wengi waliokuwa wanapata misamaha wakakwepa, wakakimbia.

Mheshimiwa Naibu Spika, why dont we come with the same system? Kwa nini tusirudie utaratibu ule wa zamani? Hilo lilikuwa jambo lingine ambalo nilikuwa nataka kulisema. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hili la Makampuni ya Madini, ili nchi ifaidike na madini, kuna mambo manne lazima yafanyike. La kwanza, nchi iwe na uwezo wa kifedha wa kuweza kuyaambia Makampuni hayo msikope nje kopeni katika Mabenki yetu. Kwa wenzetu kama Wachina, wanasema ukitaka kufanya *investment*, asilimia 70 lazima ukope ndani ya nchi yao, asilimia 30 ndio utoe nje, wakielewa kwamba asilimia 70 ukilipa ndani fedha hizi zitazunguka ndani. Sasa njia ya kwanza ya kufanya, ni benki zetu kama zina uwezo na *Central Bank*, tutafute njia ya kuwaambia Makampuni, kama unataka kukopa Dola milioni 30, kopa hapa Tanzania, hiyo ndio njia ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, njia ya pili, yako Makampuni ambayo yanatoa huduma katika madini, makampuni ya ujenzi, lazima uyaambie Makampuni kwamba lazima watafute tenda kwa Makampuni yaliyoko ndani, hilo ni sharti lazima liwekwe. Kila siku hawa watu watatoa fedha nje, wataleta *subsidiary* Kampuni zao watoe fedha nje, hilo lazima liwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, lazima uhakikishe vile vile una wataalam wa kutosha ndani na uyaambie Makampuni kwamba msiajiri watu kutoka nje. Kwanza, lazima mtazame ndani, soko letu la ajira liko kiasi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, ni huduma za kawaida, *supplies*, lazima uhakikishe Makampuni hayo yanatumia *supplies* za ndani. Usipoweka masharti hayo, hii *levy* tunayoitoa, haitusaidii kitu kwenye Makampuni hayo na huwezi kujenga taaluma ya *Mining Industry* kama huziwezeshi Kampuni zako za ujenzi ndani ya nchi, *simply theory*, hebu tufanyeni hivyo katika sheria zetu badala ya kusema tu tuna *MDA*, hizi *MDA* ziko dunia nzima, Congo wamesema basi *MDA* tunasimamisha miezi sita, tukae tuzungumze, wamezungumza mbona wamekubaliana, imeshindikanaje hapa Tanzania? Venezuela

wamezungumza na Kampuni ya Mafuta, mbona wameweza, inakuaje Tanzania ndio pekee tuko kwenye kigugumizi cha *MDA*?

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema ni vizuri Serikali ikaheshimu mikataba, lakini sio kwa gharama za Watanzania. Nakubali kabisa Serikali iheshimu mikataba, ni jambo jema kabisa, ni utawala bora, lakini ufike mahali useme maslahi ya watu yako wapi, hili ni jambo la msingi sana. Kwa hiyo, naomba Serikali iangalie katika maeneo haya manne. Tuangalie sheria zetu, mnazibana vipi Kampuni hizi ili kutumia rasilimali zetu zilizoko hapa nchini. Nilitegemea Mheshimiwa Waziri alipoleta hii *amendment*, angalau lile pendekezo la Kamati angeliangalia, lakini bado pendekezo aliloleta katika *amendment* limesahau lile pendekezo la Kamati na la Kambi ya Upinzani, nafikiri hili lingeangaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, namtegemea Waziri atakapojibu hoja vizuri na naamini atajibu vizuri, nitaiunga hoja hii mkono, ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. SIRAJU J. KABOYONGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Muswada huu wa *Finance*. Nianze kwa kumpongeza Waziri na timu yake yote katika Wizara ya Fedha na Uchumi na vyombo vikubwa vya fedha kama Benki Kuu, kwa kazi nzuri wanayoifanya. Vile vile nisisitize kwamba hoja zilizosomwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, kwa kiasi kikubwa zimekidhi sehemu ya maoni ambayo hata mimi ningependa niyachangie, lakini naomba nisisitize yafuatayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, ni suala zima la Kodi za Majengo. Kodi za Majengo, ni eneo moja ambalo likisimamiwa vizuri, kwa bahati mbaya si sehemu ya Muswada, lakini ni katika maeneo ambayo yangeweza yakaifanya Serikali yetu ipate fedha nyingi lakini mpaka sasa hivi fedha hazipatikani. Hebu tuangalie na upande huo. Kodi za Majengo, jiji kama la Dar es Salaam, Mwanza yanaweza yakapata fedha nyingi na kwa kweli hapa ndipo inapokuja eneo lingine la kuanzishwa *Municipal Bond* ambazo zingeziwezesha hizi Serikali za Mitaa na Majiji kuwa na chanzo kingine cha fedha za uhakika na kwa maana hiyo mchango wao katika bajeti ungeongezeka kama tu eneo hili la Kodi za Majengo hasa katika miji yetu mikubwa ya Mwanza, Dar es Salaam na Mbeya kwa kuanzia ikiwekwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo la kupunguza ushuru kwenye mafuta mazito, Mheshimiwa Waziri katika pendekezo lake anapendekeza kutoka shilingi 97 kwenda shilingi 80/=, kwa hiyo ni punguzo tu la shilingi 17. Ni punguzo dogo sana kuwa na *impact* kwenye *costs structure* ya haya Makampuni. Miongoni mwa Makampuni ambayo yatafaidika na punguzo hili ni yale yanayozalisha saruji. Tatizo letu moja kubwa katika viwanda vyetu vya saruji, tunasema kwamba saruji yetu ni ghali, moja ya sababu inayoifanya saruji yetu iwe ghali ni vitu kama hivyo, ushuru kwenye *ingredients* zinazokwenda kwenye *production*. Kwa hiyo, njia moja ambayo Serikali inaweza ikasaidia viwanda hivi, kwa sababu ni lazima viwepo, ni kupunguza kodi na ushuru wa namna hii. Kwa hiyo, Serikali ingejaribu kuangalia kwa sababu nilisema katika mchango wangu huko siku zilizopita, kama Egypt wanaweza wakatoa *subsidy*, Pakistan wanatoa

subsidy halafu saruji yao ikaja kuuzwa Tanzania, kwa nini sisi hatuvisaidii viwanda vyetu na vyenyewe vishindane na hawa Wa-Pakistan na Wa-Egypt kwa faida ya uchumi wetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mtiririko huo, kuna eneo la kupunguza ushuru kwenye vifungashio lakini vifungashio vilivyozungumzwa katika Muswada huu ni vifungashio vya *juice* na maziwa. Mimi kwa tafsiri pana ya vifungashio, ningeweka na magunia. Sasa kama magunia ni kifungashio muhimu cha bidhaa zetu za kilimo, chini ya utaratibu mzima wa kauli mbiu hii ya Kilimo Kwanza, tunasema tuzalishe mkonge, sasa mkonge tukishauzalisha tufanye nini? Moja ya vitu vya kufanya, ni kutengeneza magunia. Sasa magunia haya ukiyashindanisha na magunia ya Bangladesh ambayo kule tena wanayawekea ruzuku, haya ya kwetu hayawezi kushindana na kwa maana hiyo tutaendelea kutumia magunia ya Bangladesh na ku-*export* ajira zetu kwenda Bangladesh wakati tunaweza na sisi kutengeneza magunia kwa kutumia mkonge ambao tunaulima hapa hapa nchini. Kwa hiyo, eneo hili la vifungashio, hebu tuongeze na magunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la madini, Sheria yetu mpya ya Madini, inasema na inahimiza fungamanisho la sekta hii ya madini na sekta zingine za hapa nchini. Mimi nilitarajia *the Fiscal Regime* ingekuwa sasa ni moja ya njia ya kusaidia fungamanisho hili tunalozungumza liwe la vitendo lisiwe la maneno tu. Njia ya kufanya liwe fungamanisho la vitendo, ni kuangalia sasa *our tax regime* kwa kiasi gani inaweza ikazisaidia Kampuni za ndani kuweza kuwa ndio wachimbaji katika Makampuni haya ya nje. Kwa utaratibu wa sasa, Makampuni ya nje yanaona ni afadhali kuajiri Makampuni ya nje kuja kuchimba kuliko kuyapa Makampuni wazalendo wachimbe. Pendekezo limeshatolewa na liko kwenye hotuba aliyosoma Mheshimiwa Kigoda, kwa hiyo twende na utaratibu huo. Ukiweka *withholding tax* kwa Makampuni ya nje 15%, weka 5% kwa Makampuni ya ndani, Makampuni ya Migodi yatawapa kazi ya uchimbaji Makampuni ya Ndani kwa sababu ni rahisi na hapo ndipo linapokuja suala zima la fungamanisho baina ya sekta ya madini na sekta nyingine katika uchumi wetu kwa maana ya vitendo sio kwa nadharia tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo tulilionalo lingine ningependa kulisisitiza tu katika eneo la magari, tunapandisha hizi ada, nasema sawa, tupandishe ili tuongeze uwezo wa Serikali kupata mapato. Tatizo letu kubwa ni udhibiti. Kuna magari mengi yanatembea barabarani hayana hizo leseni, kwa hiyo tukiwa tunapandisha tuhakikishe kwamba tunafuatilia na tunasimamia hapo, ndipo tutakapoweza kuchanganya haya ninayosema nay ale ambayo Mheshimiwa Hamad ametoka kueleza sasa hivi, tatizo letu kubwa ni udhibiti (*enforcement*), sasa hilo hebu tuliwekee mkazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili hili eneo la *enforcement*, napenda vile vile kwenye eneo la kuleta sheria ya kumtaka kila anayeuzwa kitu kuanzia shilingi 5,000/= atoe stakabadhi, *is this realistic?* Maana tusije tukawa tunafanya mambo halafu tunatakiwa na sisi hapa tuseme ndiyo kumbe tukienda kwenye *practice*, haiwezekani. Wafanyabiashara wetu wengi ni pamoja na hao Wamachinga, wanauza vitu zaidi ya shilingi 5,000/= utawezaje ku-*enforce* hii? Kwa maana hiyo, nasema pendekezo kwa maana ya kuweka kumbukumbu ni sawa, lakini hebu kwa kuanzia tungeweka *threshold* tunaanza kushughulika na akina nani. Mimi nashauri tuanze kushughulika na wale ambao ni VAT

registered. Tushughulike nao hao kwanza, tuone rekodi zao kwa kiasi gani zinakidhi mahitaji halafu ndio tuanze kupanua wigo, tuanze ku-*capture* na watu wengine wanaouza hata anuani hawana wao kila mahali ni mahali pa kufanyia biashara tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitoe pongezi maalum kwa Serikali kuona umuhimu wa kuweka uwiano kati ya deni na mtaji ili kuweza kupata kiasi cha riba ambayo inaruhusiwa kukokotolewa katika kupata faida ambayo italipiwa kodi. Hili ni pendekezo zuri sana na kwa kweli lilichelewa, lakini Waswahili wanasema “Chelewa Ufike”, sasa tumefika. Haya Makampuni makubwa yalikuwa yanakuja na *capital gearing* yao ambayo ilikuwa zaidi kwenye deni kuliko kwenye mtaji. Kwa hiyo, tulikuwa tunalipa sana *interests* na kwa maana hiyo katika kukokotoa faida kila siku walikuwa wanaonyesha hasara tu. Naipongeza Serikali kwa kutuletea pendekezo hilo na mimi nasema naliunga mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo lingine ambalo nina wasiwasi nalo, ni eneo la uchakachujaji wa mafuta. Mafuta haya yanachakachuliwa kwa sababu kuna tofauti kubwa baina ya bei ya dizeli na bei ya mafuta ya taa. Sasa leo hii kitendawili tulichonacho ni kwamba ama tupandishe bei ya mafuta ya taa ambayo tunasema hiyo tutatumumiza Mtanzania wa kawaida na mimi nakubali tutatumumiza Mtanzania wa kawaida, kwa hiyo, tusifanye hivyo. Lakini vile vile kuna uwezekano au kuna *option* nyingine, ni kupunguza bei ya dizeli, iteremke chini, ielekee kwenye bei ya mafuta ya taa. Ukifanya hivyo, utasaidia *transport sector* ya nchi hii pamoja na *agriculture sector* ya nchi hii ambayo inatumia sana dizeli.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tusiwaangalie tu wanaotumia mafuta ya taa, tuwaangalie pia ni akina nani wanatumia dizeli. Dizeli ndiyo injini ya uhai wa uchumi wetu kwa sababu ndiyo inayotumika kwenye usafiri wa malori, mabasi, matrekta na kadhalika. Kwa hiyo, hebu tuangalie uwezekano wa kuitaremsha yenyewe ifuate mafuta ya taa mwisho wa siku hizi bei zisipishane sana na kwa kufanya hivyo ukipunguza bei ya dizeli, ni njia nyingine ya ku-*stimulate economy* hii. Kwa sababu kama unategemea dizeli ili ulime, unategemea dizeli ili magari moshi yatembee, malori na mabasi yaende, ukipunguza bei kule *you are stimulating the economy*. Kwa hiyo, hili ni eneo lingine la kulitazama, tusiangalie ooh tukipandisha mafuta ya taa tutawaudhi wakulima angalia ukiteremsha dizeli utawezesha ku-*stimulate economy* yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii, kwanza kabisa, kushukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia Muswada huu wa Fedha. Lakini vile vile nichukue nafasi hii, kuipongeza sana Wizara kwa kutuletea Muswada huu mzuri ambao hakika unaeleweka. Nina michango yangu michache sana kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako, naomba nianze na kile Kifungu cha 4, ukurasa wa tatu, kuna maneno yametumika kuhusiana na *US dollars one hundred sixty per metric tone*. Najiuliza kwa nini tutumie Dola kwenye sheria yetu. Baadhi ya sheria tumekuwa tukijadiliana, tukasema kama tunaweza tukatafsiri viwango vya Dola katika

fedha ya Kitanzania na hii ni sheria ya Tanzania basi itakuwa ni vyema zaidi. Kwa hiyo, ninaomba nishauri Wahasibu walitafakari hilo maana hata ukiweka Dola wakati mwingine inapanda na kushuka. Kwa hiyo, tungeweza kutafakari jinsi gani badala ya kutumia *US dollars one hundred sixty per metric tone* basi tutafsiri fedha hiyo ya Dola kwa viwango vya fedha yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale pia kuna kifungu kinaelezea kwamba kutakuwa kuna *export levy* itakayokusanywa na TRA kutokana na zao la korosho na kiwango hicho kitakachokusanywa na TRA ni asilimia 65. Ukienda ukurasa wa nne pale juu, inaeleza kwamba asilimia 65, nazungumzia *Section 4(17A)(2)(a)*, inaelezea kwamba hiyo *levy* itakayokusanywa kutokana na korosho, hiyo kodi asilimia 65 itakwenda kwenye Halmashauri husika na asilimia 35 itakwenda kwenye *consolidated fund*. Sasa nikawa nasema kama watakaokuwa wanakusanya ni TRA, *unless* kama ni TRA katika *respective council* ndiyo wanakusanya lakini kama TRA, TRA wakati wa *ku-export*, nilikuwa natafakari kwamba watatumia *mechanism* gani, utaratibu gani, mfumo gani kujua kwamba hizi korosho zimenunuliwa kutoka Wilaya X au Wilaya Y au Wilaya Z inaweza ikatokea kwamba kuna mtu wa katikati ananunua korosho, anakusanya, zinapatikana, baada ya kukusanya zile korosho ndipo ana-*export*. Maana yake pale ndipo wanapolipa *exporty levy* na tumekubaliana kwamba *export levy* lazima irudi kwenye Wilaya husika, sasa kama huyu mtu wa katikati ananunua korosho maeneo mbalimbali, anakusanya halafu baadaye ndiyo analipa *export levy* kwa ajili ya kurudisha sasa tutajuaje kama hizi korosho zimepatikana kutoka Wilaya X, Y, Z lakini naunga mkono wazo hili la kurudisha asilimia 65 ya *export levy* kwenye Wilaya husika, hili ni jambo muafaka na linafaa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo ningeomba kutoa ushauri ni juu ya ushuru wa mazao asilimia 3 - 5. Jambo hili ni jema sana lakini ningeomba kushauri kwamba ushuru wa mazao utumike kwa mazao ya biashara. Yako mazao mengine wananchi wanunua kwa madhumuni ya kujikimu kwa mfano mimi ninayetokea Mkoa wa Iringa, wako akina mama pale Wilaya ya Kilolo, eneo la Ilula wanauza nyanya na vitunguu, kule Ludewa mahindi ya kula, pale Njombe wanauza viazi debe moja, amenunua kwa ajili ya kujikimu na anapita navyo kwenye geti, kuna geti pale Madope Lusitu, kuna geti pale unapoingia Wilaya ya Makete na maeneo kama hayo, kuna mageti mengine Wilaya ya Mufindi. Hasa, watu wanaponunua mazao kwa ajili ya kujikimu, wanapopita nayo pale getini, ningeomba Serikali za Mitaa, TAMISEMI tuangalie wale wanaonunua kwa ajili ya kujikimu wasitozwe ushuru wa mazao, ndio ushauri wangu. Wale ambao wanapaswa kutozwa kama mtu amejaza *fuso* la viazi, mtu amejaza lori la mahindi kwa ajili ya kufanya biashara, maeneo hayo ni hakika ni vyema kabisa wanatakiwa kulipa lakini kwa ajili ya kujikimu debe moja, ndoo moja tuangalie hawa akina mama kwa sababu wao ni asilimia 51 na unapozungumzia kuboresha maisha kwa kila Mtanzania basi wao akina mama wanakuwa ndio walengwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo ningeomba kutoa ushauri ni kifungu kinachohusiana na Kodi za Wazee (*Property Tax*) kwamba Serikali imeamua kuwapunguzia mzigo wazee hawa wenye umri kuanzia miaka 60 na kuendelea. Hili ni jambo jema sana. Ukienda kwenye Madhumuni ya Muswada huu, madhumuni yake

yamekuwa mazuri, inaeleweka sana kwenye lugha ya Kiswahili na Kiingereza inasema kwamba ukurasa wa 24 “*Exempt old person who are 60 years and above from paying levy on one residential rentable building*”. Lakini hapa katika Kifungu cha 33, haijaonyesha kwamba watasamehewa kodi ya nyumba moja (*on one rentable*). Sasa nikawa najiuliza inawezekana huyu mwananchi ana nyumba moja Dodoma, ana nyumba nyingine Iringa, ana nyumba nyingine Dar es Salaam, wanajua ana nyumba moja na ndiyo huyo huyo, sasa hapo tuliangalie vizuri, lakini hili ni jambo jema kuwasamehe. Kwa hiyo ninaomba wanao-*draft* Sheria basi maneno haya ya-*capture* yale madhumuni na hapa katika Sheria anasema kwamba, *a person living with disabilities who has no other means of earning than a residential house...*, ukienda kwenye tafsiri yake anasema *who have no reliable sources*. Sasa hapo tuangalie maana Kiswahili inaelezea kwamba endapo hana kipato cha kutosha cha kulipa kodi ya majengo ndipo atasamehewa, inaonesha kwamba si wote na inaonesha kwamba atasamehewa nyumba moja. Sasa kama ndivyo hivyo basi tungepata ufafanuzi lakini hata yale maneno yaweze ku-*capture* madhumuni yake, haisemi kwamba endapo kama hana kipato cha kutosha, inasema endapo hana kipato kingine, kwa hiyo, hapo ingekuwa *clear*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango wangu huo, ninaunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Awali ya yote, nataka kutumia nafasi hii, kuipongeza sana Serikali kwa uamuzi wake wa jana wa kumrudishia CAG Tshs.8 bilioni kwenye Bajeti yake. Hii inaonesha wazi kwamba wanajua umuhimu wa kuwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali na zaidi pongezi hizi nampa Waziri Mkuu kwa uamuzi wa papo kwa papo, hiyo ndiyo maana ya uongozi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, napenda kutumia nafasi hii kusema kwamba, jana nimesema “Ndiyo” kwa Bajeti hii kwa sababu hii ni *Vote* yangu na ni *Personal Vote* ambayo mimi wakati wowote nikaulizwa nitaweza kui-*defend* na mimi nashauri sisi viongozi wa vyama, nimeambiwa naweza nikaondolewa kwenye Kambi, lakini sisi viongozi wa vyama tujifunze kuweka maslahi ya Taifa mbele kuliko maslahi ya vyama vyetu. Huu ndio msimamo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende kwenye *Finance Bill...*

NAIBU SPIKA: Nadhani jana watu walichukia vibaya sana.

MHE. JOHN M. CHEYO: Shauri yao. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye *Finance Bill*, nataka kujielekeza katika maeneo machache. La kwanza, ni *amendment* juu ya umuhimu wa kuweza kupata *receipt*. Mimi wasiwasi wangu hapa kwanza kuna adhabu kali kwa kutotoa *receipt* lakini tumejiandaa namna gani na kuna utaratibu gani, la sivyo tutajaza jela watu ambao ni wafanyabiashara. Kwa hiyo, natoa tahadhari tu na kuna Mheshimiwa mmoja amesema

hapa labda tuiweke awamu kwa awamu ili tujenge hii tabia ya kutoa *receipt*, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, juu la *Local Government, crops cess*, hili mimi naliunga mkono kwamba ni vizuri Halmashauri zetu zikapata pia mapato ya pale kwenye Halmashauri. Najua Serikali inasukumwa sana na wafadhili kwamba hii sehemu isiwepo lakini utegemezi ndiyo tumeukemea, kama tusipojenga tabia ya watu kuweza kupata mapato tutaisha. Lakini kitu ambacho mimi nimeona hakipo hapa, Serikali iko makini sana katika kutoa adhabu kwa kodi zinazoenda kwa Serikali Kuu, sasa hapa mbona hakuna adhabu kwa mtu asiyelipa? Sisi Halmashauri tuna tabu sana, sisi kule tunawalipaji wa *cess* za pamba. Bariadi peke yake tunadai mpaka sasa shilingi milioni 800 kwa muda wa miaka miwili, mitatu na hatuna njia ya aina yoyote. *Cess* ni kodi, *cess* si madai siyo kwamba tumekopesha, kwa hiyo, ninamwomba Waziri atutafutie njia, kwa watu wa korosho, amefanya vizuri amewapa *TRA* ndiyo wanakusanya, kwenye pamba je, hakuna utaratibu ambao unaweza kuwekwa na yule ambaye asiyelipa atozwe adhabu inayostahili isiwe sasa madai kati ya Halmashauri na yule ambaye anapaswa kulipa hiyo kodi na hiyo ndiyo hali halisi kwa sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Internal Auditor*, hili mimi kama Mwenyekiti wa *PAC* tumelisemea sana, tumefika hatua hili jambo ni zuri sana. Pia nataka kusesitiza Kifungu cha 15 ambapo *Internal Auditor* atakuwa anaingia kwenye vikao vya *PAC*, ili aweze kushauri *PAC* juu ya mambo mbalimbali ambayo ameyaona. Mimi naona ni jambo zuri na utaratibu uandaliwe ili iweze kutusaidia katika kudhibiti matumizi mazuri ya fedha ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Sehemu ya Tisa, kumekuwa na *amendment* juu ya *Public Audit Act* ambapo hapa kuna sehemu ambapo baada ya *DPP* kuona kwamba hatampeleka mtu Mahakamani lakini kuna vitu lazima vifanyike ili kuweza kurekebisha yale ambayo yaliharibika. Hiyo *section* inampa mamlaka *CAG* kuweza kuchukua hatua, mimi naona hii hatekelezeki, *CAG* atachukua hatua gani? Mkaguzi anaweza kuchukua hatua gani kwa *Accounting Officer* ambaye ameharibu mali ya Serikali kwa uzembe wake? Mimi naona hapa ndiyo ilikuwa nafasi nzuri ya Sheria hii kutoa meno kwa Kamati kama vile ya *PAC* kwamba badala ya kumwajibisha tu kwa tozo la asilimia tano ambayo imesemwa katika Kanuni za Mheshimiwa Waziri hapa ndiyo ilikuwa nafasi sasa kwamba kama mambo yameshindikana kule kupelekwa mtu Mahakamani angalau *PAC* iweze kumwomba Mheshimiwa Waziri au *Pay Master General* amwondoe yule mtu katika *U-Pay Master General* na jambo hili lishinikizwe kisheria ili tukisema hivyo kweli mtu huyo anaondolewa. Hii ndiyo itakuwa inatoa meno.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu Uganda ukienda kwenye *PAC* unakuta Polisi yuko pale na pingu ziko pale na ubaya kule Mawaziri wanaitwa, ukifanya blaablaa, pingu iko hapo na *CAG* anakuchukua mnakwenda naye, utakwenda kumwomba mama akuletee chakula kule gerezani. Hiyo ndiyo hali ya wenzetu ambayo wamefikia. Tuangalie kwa hii, *CAG* hawezi akamwajibisha mtu yoyote. Kwa hiyo, Sheria hii hapa haijatatendea haki katika kujaribu ku-*correct* mambo ambayo hayafai.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kuzungumzia kwa haraka mambo ya *Value Added Tax*. Kwa mfano, Kifungu cha 43(2) inazungumzia juu ya kusamehe kodi ya *VAT* kwa usafiri wa mazao kutoka pale yalipolimwa na kwenda kwenye viwanda, ni jambo zuri. Lakini sisi ambao tunalima pamba, tunategemea kwa kuondoa baadhi ya gharama zinazohusika na pamba kama vile kusafirisha marobota kutoka kwenye *station* kwenda Dar es Salaam yanapokwenda *for export*, hii pia ingeondolewa *VAT* ili hiyo gharama irudi kwa wakulima na kama ninavyosika mwaka huu tunaanzia shilingi 600/- kwa kilo moja ya pamba labda itapanda ifike shilingi 800/- na hivyo ndivyo tutakuwa tunamkomboa mtu wa kawaida. Kwa hiyo, nafikiri usizungumzie juu ya miwa, *sisal*, *tea*, mbona hujasema kahawa, pamba na vitu kama hivyo, kwa nini iwe mazao matatu tu? Mimi nafikiri ungeongeza hapo ingeweze ikatusaidia sisi wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nataka nizungumzie jambo hili la kuchanganya mafuta ya taa na *diesel*. Mimi mwenyewe naweza kujisemea. Nilikuwa na *BMW* yangu nimeiweka kwenye ghala haiendi, nimetumia fedha nyingi sana zaidi ya shilingi milioni 15 kujaribu ku-*change* hiki, kugeuza hiki haiwezekani, imeharibiwa kabisa na huu mchanganyo wa mafuta ya taa na *diesel*. Mimi nafikiri pamoja na yale yaliyozungumzwa, tatizo kubwa liko kwa watu ambao tumewapa madaraka ya kuangalia hizi *Petrol Station*, wametushinda nini? Kwanza *Petrol Station* zenyewe nyingi mno, mimi sijaona, ukitoka pale Morogoro kwako Mheshimiwa Waziri kila baada ya mita 500 *Petrol Station*, wanamuuzia nani? Ukiwa pale Kibaha karibu mita 500 unakuta *Petrol Station*. Mimi nafikiri vyombo vilivyopewa jukumu hili kama *TBS*, *EWURA* wafanye kazi yao na watu wafungwe kwa kufanya kitendo hiki. *Petrol Station* zifutwe na wafutiwe biashara hiyo kwa kufanya kitendo hiki kwa sababu wanaiibia Serikali, wanaharibu magari ya watu mpaka wanatuaibisha kwa kumsimamisha Rais wetu njiani kwa sababu magari yake hayawezi kwenda. Naomba muwe wakali kwa hili, fungu watu, fungu *Petrol Station* zao na hatuna haja ya kufanya jambo lingine, wananchi wapate mafuta kwa bei rahisi lakini hawa waadhibiwe kama inavyostahili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, maana pale Kibaha kila kona yaani hiyo biashara ya namna gani, kila kona na hasa Mkoa wa Pwani. Namwita Mwenyekiti wa UWT, Mkoa wa Pwani, Mheshimiwa Zaynab Vulu. (*Makofi*)

MHE. ZAYNAB M. VULU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Awali ya yote, napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu na nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia. Lakini la pili napenda kuzungumzia suala la vituo vya mafuta kwenye Mkoa wa Pwani, hilo suala nafikiri limeshafika kwenye ngazi za kisheria na linashughuliwa kwenye vyombo vinavyohusika, hata sisi linatukera, kubwa zaidi linatukera hasa kwenye mafuta ya taa. Sisi Mkoa wa Pwani, watu wengi wanatumia mafuta ya taa kwa ajili ya matumizi ya taa na shughuli zingine za nyumbani lakini nafikiri kuna haja ya kuliangalia suala la bei. Ikipunguzwa bei ya *diesel* basi tatizo hili litapungua kwa sababu athari yake ni kubwa na haiwapati watumiaji wa mafuta ya taa peke yao, athari hii inaharibu hata jina la nchi kwa sababu mafuta wanayoyachakachua kwa kutumia mafuta ya taa na kuyapeleka nje ya nchi, yanapokwama kule, sifa mbaya

inakuja kwa nchi ya Tanzania. Ninaomba suala hili, vyombo vinavyohusika vichukue mkondo wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, nafikiri wahesabu muda watanihesabia dakika zangu kwa sababu nilikuwa najibu hoja ya Mheshimiwa Naibu Spika na haikuwa kwenye mada yangu. (*Kicheko*)

NAIBU SPIKA: Hapana, ulikuwa unajadili. (*Kicheko*)

MHE. ZAYNAB M. VULU: Mheshimiwa Naibu Spika, nina mawili ya kuzungumza. La kwanza, niipongeze Wizara kwa kuleta Muswada huu lakini pia nataka nitoe pongezi kwa kutoa msamaha kwa wazee na wale wasiojiweza katika kodi ya majengo. Lakini nitoe ushauri, kuwekwe vigezo vya kuwatambua wazee ili wasipate usumbufu. Hii inatokana na uzoefu uliokuwepo kwa wale wazee wa kuanzia miaka 60 ambao hawalipi pesa za matatibu lakini unakuta wanapokwenda Hospitali wazee wale wanasumbuliwa sana. Hivi jamani mtu akiangaliwa usoni haonekani kama huyu yuko zaidi ya miaka 60? Anafika pale anaambiwa lazima atoe barua kutoka kwa Mwenyekiti wa Kijiji, Mtendaji wa Kata na kadhalika. Sasa cha kwanza kuhudumia pale ni nini? Ni ule ugonjwa au kuipata ile barua? Naomba hili suala kama Serikali tumeshaamua basi viwekwe vigezo ambavyo havitaleta usumbufu kama usumbufu wanaopata wazee wetu wanapokwenda kupata matibabu Hospitalini wanaambiwa wapeleke barua kutoka kwa Watendaji. Mtu kafikwa na ugonjwa usiku ghafla, afunge safari mpaka kwa Mtendaji akapate barua, arudi aende Hospitali uwezo huo anautoa wapi? Naomba Wizara na Serikali kwa ujumla iangalie uwezekano wa kutoa usumbufu katika suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ya pili nataka kuzungumzia vifungashio vya dawa kwa dawa za binadamu. Nashukuru katika Muswada huu, katika ukurasa wa 25, *Part* ya 12, umezungumzia suala la kuhimiza Kilimo Kwanza. Mimi hili nalikubali na nalipongeza sana lakini Kilimo Kwanza kinalimwa na binadamu na binadamu huyu anatakiwa awe na nguvu, awe na afya bora ili aweze kufanya kazi za kilimo na azalishe mazao yake kwa ufanisi. Lakini unakuta binadamu huyu anapougua anakwenda kununua dawa, dawa anazonunua, kuna dawa zinazotoka nje ya nchi na kuna dawa zinazotengenezwa hapa nchini. Dawa zinazotoka nje ya nchi hazitozwi ushuru zinapoingia haswa kwa upande wa vifungashio lakini viwanda vyetu vya hapa Tanzania, tumewashawishi wazalendo na wawekezaji waweke viwanda vya dawa lakini huko nyuma viwanda hivi walikuwa hawalipi ushuru wa vifungashio. Sasa hivi wamerudishiwa ushuru wa vifungashio matokeo yake wanakuta wanapata hasara, wanaingia kwenye ushindani ambao hawana uwezo kwa sababu wenzetu kutoka nje dawa zao wanazozileta hazina ushuru kwa hiyo dawa zile zinazuzwa kwa bei rahisi ukilinganisha na dawa zinazotengenezwa hapa nchini. Athari yake si kwa wao tu, athari yake hapa ninayoiona mimi ni kwa sisi watumiaji, tunanunua dawa za kwetu wenyewe Watanzania lakini dawa hizo zinakuwa ghali sana kutokana na wao lazima waingize gharama zao ili waweze kufidia na kupata faida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, bado hao hao wenye viwanda vya nje hawawezi kuingia katika ushindani wa masoko, hawezi akaitoa dawa yake hapa Tanzania akaenda kuiuza nje ya mipaka ya Tanzania. Tumehimiza soko la Afrika Mashariki, mwenye dawa huyu wa Tanzania kwa mtindo huu wa vifungashio kuwa na ushuru, hawezi akafanya lolote la kumwezesha yeye kuwa na kipato cha kutosha. Ombi langu kwa Serikali, ikiwezekana wakati huu tunajadili suala hili, utafutwe utaratibu wa kuingizwa kipengele cha kwamba vifungashio za dawa zinazouzwa hapa na kutengenezwa hapa nchini vitolewe ushuru ili wanunuzi waweze kupata kwa bei nafuu. Faida hii tutaipata sisi tunaouguza watoto wetu, sisi wenyewe, wazee wetu na hata hawa wawekezaji na wenye viwanda watakuwa na wao wamepata faida kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili suala ni muhimu na hasa ukizingatia tunaingia katika ushindani wa kiuchumi kati yetu sisi na soko hilo la Afrika Mashariki na sio tu kwamba tunataka tuuze hapa Afrika Mashariki dawa hizi tunataka zifike mpaka nje ya Tanzania na nje ya mipaka ya Afrika Mashariki. Ni vyema Mheshimiwa Waziri na timu yake wakaangalia ni jinsi gani wataweza kutoa ushuru kwa vifungashio vya dawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba niunge mkono hoja lakini naomba hoja yangu izingatiwe. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwi Wabunge, ninawakatisha majadiliano ili wale wanaohusika waweze kuchukua hatua zinazostahili. Watakaokwenda kwenye msiba wa Mume wa Mheshimiwa Jenista Mhagama ambao wanapaswa kuwa *Airport* saa saba na dakika kumi na tano hii leo ni Mheshimiwa Dr. Emmanuel Nchimbi, Naibu Waziri, Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib, Mheshimiwa Samwel Chitalilo na Mheshimiwa Vita Kawawa na watakwenda na watoto wa marehemu wako hapa. Kwa hiyo, hawa saa saba na nusu wawe *Aiport*.

Waheshimiwa Wabunge, halafu mnamuona Mheshimiwa Waziri amekaa peke yake na anao Manaibu Waziri wawili, kumbe Naibu Waziri, Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee, juzi nyumba yake iliingiliwa na majambazi, kijana wake mmoja ameumizwa vibaya na baadhi ya mali zake zimechukuliwa. Kwa hiyo, Waziri amemruhusu aende akaangalie hali hiyo na Naibu Waziri, Mheshimiwa Jeremiah Sumari, yeye bado yuko kwenye matibabu India, ndiyo maana Waziri yuko peke yake. Sasa tunaendelea na Mheshimiwa Shellukindo halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Mohamed Mnyaa.

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana na mimi kwa kunipa nafasi ili nitoe mchango wangu kidogo kwenye Muswada huu wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2010, *The Finance Bill 2010*. Muswada huu unahusiana na masuala ya fedha, kuangalia vyanzo vya kusaidia kuongeza mapato. Sasa kuna jambo moja limetokea hapa ambalo sisi kama Wabunge tusingelinyamazia tu, ni hili suala la kupoteza mapato ya biashara ya mafuta. Ni jambo kubwa sana na siyo la kiuchumi tu ni la kisiasa vile vile kwa sababu yaliyotokea yanahusu uhusiano kati ya nchi yetu na nchi za jirani ambapo mafuta yale yanapelekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Wabunge, hili suala nadhani tusilinyamazie tu hivi hivi kwa kweli. Mimi ninapendekeza kwamba Wabunge tukubali kwamba hili ni suala la kukemea kwamba tusingependa vitendo kama hivi vijitokeze tena na kuiagiza Serikali kwamba ichukue hatua za haraka kuhakikisha kwamba haiharibu uchumi wetu na vilevile haiharibu uhusiano na nchi jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku ya Jumapili, Mwenyekiti wa Wasafirishaji hawa wa Mafuta, alinipigia simu kuniuliza kama ninajua hilo tatizo na nikamwambia ninalijua na bahati nzuri Kamati ya Uongozi tulifahamishwa kwamba suala hili limetokea na wakati ule yalikuwa yamekamatwa magari kule Burundi, Rwanda na DRC kwa sababu ya kuchakachuwa mafuta. Kanieleza kuwa kuna magari kama sitini hivi yamerudishwa ambayo yana mafuta yaliyochakachuliwa yanarudi nchini. Kwa hiyo, hapo kuna hasara kubwa kwanza kwa wenye mafuta hayo na vilevile kwa nchi kwa maana ya mapato ambayo yangetokana na mafuta hayo na amenifahamisha kwamba kama hatuchukui hatua za haraka basi tutapoteza biashara hiyo kabisa. Kwa sababu Rwanda sasa wanaagiza mafuta yao yapitie Mombasa, Kenya, sasa Waheshimiwa Wabunge hili nadhani ni la kwetu, tulikemee, mambo haya yasijirudie tena na waliohusika kwa kweli wachukuliwe hatua bila kuchelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningeongeza ni ile Sheria ya *EWURA* inahitaji itazamwe haraka sana kwa sababu adhabu zinazotolewa ni ndogo sana. Halafu Sheria ile haimbani Dereva, inambana mwenye gari na kama matukio haya yanatokea huko njiani, yeye hana habari, yeye ndiye anaadhibiwa. Mimi ninadhani kwa Madereva pale tungeshauri Serikali muweke adhabu ya kifungo. Watu wafungwe kidogo waone kuwa hili suala ni la hatari sana, magari ya wananchi yanaharibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu kingine cha hovyoy kabisa, magari ya Rais kuhusika, hili kwa kweli ni fedheha (*embarrassment*) kubwa sana. Kwa hiyo, mimi napenda kutamka kwamba hilo suala kwa kweli silipendi na nalichukia, la hovyoy ni la kihuni na linadhalilisha nchi yetu.

NAIBU SPIKA: Sasa, dawa yake siyo kukemea, hayo uliyosema kubadili au kuongeza vifungo vya adhabu kwenye Sheria, ndiyo maneno hayo.

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Naibu Spika, eneo nililotaka kuipongeza Serikali, ni hili la kuweka ushuru kwenye usafirishaji wa korosho ghafi na napenda kusema kwamba tumechelewa. Hili suala tulitakiwa tulifanye juzi kwa sababu limefanya hata viwanda sasa vya korosho vimefungwa na havifufuliwi kwa sababu nadhani kuna manufaa ya hawa wanaopeleka korosho nje huko na tunajenga uchumi wa wenzetu. Hizi korosho zetu zinakwenda kufungua viwanda India huko na sehemu nyingine na vya kwetu hapa vimelala. Kwa hiyo, mimi ninaliunga mkono kabisa na tusirudi nyuma na kama wanaendelea, tunaongeza huu ushuru kutoka hiyo asilimia 15, kwa hiyo, itazamwe katika muda mfupi unaokuja ili tuweze kurekebisha uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Muswada huu, ninapenda Mheshimiwa Waziri atazame Ukurasa wa 11, nadhani pale kuna tatizo kidogo. Katika maelezo ya maneno

Ukurusa wa 11, Kifungu 24 pale, inaeleza kwamba “*the phrase one hundred thousand shillings (Shs.120,000/=)*”, hiyo nadhani ingetazamwa. Nataka kuuliza hiyo ni Shs.120,000/= au Shs.100,000/= kwa sababu maneno yanasema Shs.100,000/= kwenye mabano imewekwa Shs.120,000/=, hilo ni moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo napenda kulichangia ni kuhusu Sheria ya Fedha za Umma. Katika eneo hili, napenda sana kuipongeza Serikali kwa kuipandisha hadhi Idara ile iliyokuwa ya Ukaguzi wa Ndani, ni jambo zuri sana. Lakini nilitaka kusema hivi, Idara hii haina tofauti kubwa sana na Ofisi ya *Controller and Auditor General*. Inatakiwa iwe na uhuru (*some independence or autonomy*). Uhuru wa kuweza kufanya mambo ambayo pengine yangukuwa ni makosa ya hesabu. Kwa hiyo, katika kile Kifungu cha 37, ule Ukurusa wa 12 badala ya kusema, “*there shall be an Internal Auditor General under the Permanent Secretary*”. Mimi nadhani hapa tungeandika, “*in the Ministry of Finance*” kwa sababu ukiweka “*under the Permanent Secretary*”, huyu atamsimamia huyu Afisa Masuhuli wa Hazina. Lakini kile Kifungu cha 38 kimekaa vizuri kwamba “*the Internal Auditor General shall be responsible to the Paymaster General*”. Nadhani mmenipata hapa, kwa sababu hapo Hazina penyewe atakuwepo yeye ambaye ni wa Kitaifa lakini patakuwepo na “*Senior Internal Auditor*” wa kushughulikia Hazina yenyewe hapo lakini chini ya “*Paymaster General*” ambaye anamsimamia “*Internal Auditor General*”. Kimuundo ingekaa hivyo ili asiwekwe chini ya mtu mwingine ambaye anamsimamia. Kwa hiyo, huyu atakuwa kwenye ngazi ya kuwajibika kwa “*Paymaster General*”. “*Paymaster General*”, ninavyojua mimi siyo Afisa Masuhuli wa Hazina, nadhani mmoja wa “*Deputy Permanent Secretaries*” ndiyo Afisa Masuhuli ambaye anaweza kuulizwa maswali na watu wengine hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine nilitaka kulizungumzia liko katika ile Sheria ya “*Public Audit Act*”, Kifungu cha 29, Ukurusa wa 16. Mimi ninafurahi sana kwamba imewekewa muda kwamba masuala hayo yachunguzwe katika muda wa siku 60. Kuweka muda huo, ni kitu kizuri sana na ninadhani mambo mengi hayaendelei kwa kasi (*speed*) inayotakiwa kwa sababu hayana muda maalumu wa kuyashughulikia. Sisi baadhi yetu ambao tuko katika fani hii ya “*Management and Public Administration*”, tunaamini na tunasema kwamba mtu ukimuwekea muda maalumu (*time frame and deadline*), atafanya kazi kwa haraka na kwa bidii ili katika muda huo aweze kuyatekeleza. Sasa kwa Sheria hii imenifurahisha, ningependa sana kuweka Kifungu cha muda wa kutekeleza na siyo lazima mtu angoje mpaka siku 60. Anaweza kutumia hata siku tano, sita na hata mwezi mmoja lakini isizidi siku 60. Mimi nakubaliana kabisa na pendekezo hili, kuna vitu vingine vidogo vidogo tutakuja kuvitazama wakati wa kupitia vifungu kwenye Kamati ya Bunge Zima.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante. (*Makofi*)

MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kutoa mchango wangu kidogo katika hii *Financial Bill*. Kwanza, nishukuru kwamba inaonekana mawazo ya Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, hayatofautiani sana na mawazo ya Kambi ya Upinzani kwa sababu kile walichopendekeza kuhusu misamaha ya kodi ya mafuta, kuhusu mapato ya Halmashauri,

kodi, usajili, kuhusu marekebisho ya VAT, msamaha wa kodi ya ndani na uchakachujaji wa mafuta, ni hayo hayo na sisi ambayo tumeyazungumzia kwa nguvu zetu zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nina mawili tu muhimu sana ambayo nilikuwa ninataka niyazungumze. Kwanza, inahusiana na mabadiliko ya Sheria ya Korosho, Sura ya 203, ili kutoa motisha zaidi kwa wafanyakazi na kuongeza ajira zaidi, ilikuwa kuna umuhimu sana wa kupunguzwa hizi kodi za ndani ili kuongeza motisha kwa viwanda na wafanyakazi wa korosho na kuongeza ajira zaidi. Lakini kitendo cha ushuru (*export duty*) wa *dollar* 160 ili kuweza kuzuia kusafirisha korosho ghafi, ni jambo zuri ambalo Serikali imefanya na ikiwezekana labda zingengezwa ikawa ni zaidi ya *dollar* 160 kwa sababu tutakaposafirisha korosho ambazo zimebanguliwa, ni tija zaidi kwa viwanda vyetu na wafanyakazi kupata ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili, inabidi tuwe waangalifu kwa kitu kimoja kikubwa sana kwamba inaonekana usafirishaji wa korosho ghafi utazidi kuendelea, tena utaendelea zaidi, kwa hiyo, hata hicho kiwango cha dola 160 bado hakitazua usafirishaji wa korosho ghafi nje na sababu kubwa hapa ni kwamba uwezo wa viwanda vyetu ni kubangua korosho tani 17,000 kwa mwaka, lakini uzalishaji wa korosho ni tani 100,000 kwa mwaka kwa maana hiyo usafirishaji wa korosho ghafi utaendelea hapa. Ningeishauri Serikali kwamba hebu mtumie ujanja kama kwenye makampuni ya madini mlisema kwenye mikataba ya MDA Serikali itafanya mazungumzo ili kuona huo uwezekano wa kuondoa huo ushuru wa mafuta. Sasa kwa nini hapa Serikali isifanye mazungumzo na wenye viwanda vya kubangulia korosho na yakatazama ni matatizo gani walionayo na Serikali ikaweza kuvisaidia hivi viwanda ili korosho nyingi zikabanguliwa hapa nchini na uwezo wa hivi viwanda ukaongezwa badala ya kubangua tani 17,000 kwa mwaka wakaongeza hata kama utaweza kulingana na uzalishaji wa tani 100,000. Kwa hiyo, ili ni eneo ambalo ningemuomba Waziri alifikirie, ikiwa leo Serikali ina uwezo wa kuzungumza na wawekezaji wa nje ambapo wawekezaji wengi wa hivi viwanda vya korosho, ni wa ndani na wa nje ni wachache sana, kwa nini tusiongee nao hawa, Serikali ikafanya mazungumzo kwa ajili ya kunyanyua uzalishaji na ubanguaji wa korosho katika viwanda tulivyonavyo. Nafikiri hii ingekuwa ni faida kwa Taifa letu, ni kwa faida ya wafanyakazi, ni faida kwa kuongeza ajira lakini vilevile ndiyo tungeweza kuzuia siyo kuweka ushuru mkubwa tu wa 160 lakini pia tungeweza kuzuia huo usafirishaji wa korosho ghafi kwenda nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo limezungumzwa katika Kamati ya Fedha na Uchumi, yamezungumzwa pia na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, ni kuhusu marekebisho haya ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148. Haya makampuni ya madini ambayo Serikali katika jibu lake imesema kwamba wataongea nao siyo kwamba wamesamehe moja kwa moja lakini wataongea nao hatua kwa hatua kupata hiyo *win, win situation*. Hapa kitu kinachoshangaza ni kwamba Serikali ilipoondoa huu ushuru katika bajeti ya mwaka jana, wakasema kwamba kwa makampuni mapya ambayo yataanza Julai 1, 2009, hayo hayajasamehewa lakini yale ya zamani yamesamehewa. Sasa muda umekuwa mkubwa, je, hayo yaliosamehewa kwa muda huo wote, mmezungumza na makampuni mangapi na hali iko vipi? Hicho kitu kilikuwa hata katika marekebisho ya Sheria ya Madini ya juzi, ni kitu ambacho kilileta mtafaruku mkubwa

sana. Kwa hiyo, ninaomba Serikali, suala hili ilianganalie ili kuweza kuongeza mapato nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini siyo hilo tu, pamezungumziwa meli ambazo ziko nje, nyingi sana zinavua na ni zaidi ya 100 na meli zile zinaweza wa kukaa baharini miezi miwili au mmoja na zinavua kwa kiwango kikubwa sana. Hizi meli hazirejei tena, zinapeleka nje lakini Serikali imefanya utafiti kuhusu meli zile katika kuongeza mapato nchini, zina *refuel* wapi? Inaonekana kuna tabia ya meli kuja na wana-*refuel* huko huko na Serikali haina taarifa hiyo, je, Serikali imeweza kuchunguza? Je, tunakosa mapato kiasi gani kama nchi na meli zile ambazo mbali ya kulipa ushuru mdogo na kuondoka na samaki lakini hata *refuelling*? Haziweki mafuta katika bandari zetu na tuna vyombo vya ulinzi vya kila aina na rada za ghali sana lakini Serikali bado haijatangazama hapo. Ninaomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, hili suala alichunguze kwa sababu suala hilo linatukosesha mapato kwa hali ya juu. Kama meli zote zile zingekuwa zina *refuel* hapa hapa au zinaweka mafuta yake hapa hapa nchini, tungekuwa tuna hali nzuri sana na hili suala tunalolizungumzia leo lisingekuwa la namna hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu huu uchakachujaji wa mafuta ambapo kila mtu anauongelea. Mimi nafikiri wakati umefika sasa, Serikali kufanya haraka mbali ya rai zilizotolewa kama rai ya Mheshimiwa Kaboyonga ya kupunguza ushuru wa dizeli lakini pia hii rai ambayo imezungumziwa ya kuweka rangi yale mafuta ya *kerosene* au mafuta mengine yoyote kuwa na rangi ambayo itakuwa ni alama, mbona yameshaongelewa muda mrefu sana, Serikali ina kigugumizi gani kutofanya hiyo shughuli au kutofanya jambo hilo haraka iwezekanavyo? Ni aibu kwa nchi kama hali itaendelea hivi. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali isichukue muda tena, katika mambo haya mawili yaliyotolewa hapa Bungeni basi mojawapo lifanywe haraka ili kuondoa matatizo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, ni kwamba tunaangalia sana...

(Hapa kengelele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

MHE. MOHAMED R. ABDALLAH: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hii *Finance Bill* iliyoko mbele yetu. Michango ya Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kwa kweli imezingatia yale matatizo ambayo yamejirudia mara nyingi. Hii inamaanisha *concern* ya Wabunge juu ya masuala haya. Ninaomba Serikali isilipuuze suala hili na ilifanyie kazi kwa haraka ili tuweze kuleta mafanikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninataka nishereheshe zaidi katika suala zima la mafuta ya taa. Hivi sasa inakadiriwa kuwa tunaigiza lita bilioni mbili za mafuta ya taa nchini kama alivyosema Mwenyekiti wa Kamati lakini matumizi kwa kila kichwa kimoja cha Mtanzania utakuta tunatumia mafuta ya taa mengi kuliko nchi yoyote katika Bara la

Afrika kitu ambacho hakiwezekani, lakini ikiwa tunachakachuwa 20% Serikali inapoteza shilingi bilioni 300.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini inafahamika kwamba uchakachuaji unazidi asilimia 20 unafika mpaka asilimia 50, kwa hiyo, tunapoteza zaidi ya shilingi bilioni 750. Hii ni hasara ambayo inapatikana moja kwa moja. Mbali ya hilo, tunapata hasara katika mitambo inayoharibika kwa kutumia mafuta haya ambayo yamechakachuliwa, kuanzia magari na mitambo ya viwandani inayotumia *diesel* na mitambo mingi tu mpaka *TANESCO* wanatumia *diesel*.

Mheshimiwa Naibu Spika, *engine* moja ya kutoa umeme ambayo *piston* yake ni sawasawa na pipa lile tunalolijua ndiyo ukubwa wa *piston* ya injini inayozalisha umeme pale Ubungo, sasa *imagine piston* ile inauzwa kiasi gani na inaharibiwa kwa lita moja ya *diesel* ambayo imechakachuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na kupoteza vipuli vya mashine kama hizi, vile vile kama alivyozungumza Mheshimiwa Shellukindo kwamba sasa *transit good* zitahama kutoka Tanzania zitakwenda maeneo mengine. Hii kazi inafanywa na madereva, ni kwa utashi wao au wanakubaliana na matajiri hiyo sijui, lakini sisi tunamjua yule ambaye ana mafuta ya *diesel* ambaye anasafirisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyoelezwa hapa, malori yaliyozuiliwa huko mpakani ni aibu kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile *diesel* imeongeza gharama ya maisha kwa ughali wake, mbali ya bei ya dunia jinsi inavyopanda na kushuka na huku pia inapanda, lakini ile kodi ambayo iko kati ya Sh. 450/= mpaka Sh. 490/= kwa lita ni kubwa. Sasa utakuta kilimo kinapanda bei, usafirishaji wa malori unapanda bei, usafirishaji wa mabasi unapanda bei. Kwa hiyo, gharama ya maisha kwa mwananchi ndiyo imekuwa ngumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kusafirisha mazao yake yeye mwenyewe Mtanzania anasafiri kwenda huku na huku, wakati mwingine anakodi malori kusafirisha mizigo yake, gharama zote hizi zimepanda bei.

Mheshimiwa Naibu Spika, kodi ya mafuta ya taa sasa hivi ni Sh. 152/=, ningependekeza kodi hii ingepanda iwe mpaka Sh. 200/= au Sh. 250/= ambayo itakuwa haijapanda sana, lakini faida yake tukishapunguza kodi ya *diesel* kama alivyoshauri Mheshimiwa Kaboyonga na mimi nakubaliana naye, kutoka Sh. 450/= na Sh. 490/= iwe Sh. 250/=, tutakuwa tume-*balance* kati ya mafuta ya taa na mafuta ya *diesel*. Serikali inachoogopa ni kupoteza ile kodi kutoka kwenye *diesel* na ndiyo mapato mengi yanayopatikana katika mafuta, tukiweka kodi ya *diesel* Sh. 250/= utapunguza makali ya maisha kwa wananchi, lakini *volume* ya *diesel* nchini itaongezeka kwa sababu imepungua bei.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukipunguza bei ya *diesel* wateja pia watafaidika kwa sababu gharama ya kilimo itapungua, gharama ya usafirishaji wa malori itapungua, gharama ya mabasi itapungua, gharama ya uzalishaji umeme itapungua na mitambo mingine yote ambayo inaendeshwa na *diesel* gharama zake zitapungua kwa kiasi kikubwa sana, kwa sababu tumepunguza hapo zaidi ya Sh. 250/= na vyakula pia vitapungua bei katika masoko kwa sababu wakulima wameshapata nafuu katika kilimo chenyewe na katika kusafirisha yale mazao yakiingia sokoni na mwananchi sasa naye atapata nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile mafuta ya ndege, *Jet One* na hapa ndipo penye udanganyifu mkubwa. Yale mafuta ya ndege yanaingia katika soko, yanauzwa kama mafuta ya taa. Kwa kuyapa unafuu mafuta ya ndege, basi utumike utaratibu kwamba siyo kampuni za kuuza mafuta hapa, yale ya makampuni ya ndege yanunue mafuta kwa kodi halafu warudi *TRA* warudishiwe kodi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tujue kwamba yale mafuta ya ndege yametiwa ndani ya ndege na tusiamini kwamba mafuta yametiwa na kampuni inayouza mafuta, hao ndiyo wanaotorosha mafuta ya taa na kuingiza kwenye soko na kuuza kama mafuta ya taa. Kampuni ya ndege ipeleke risiti *TRA* kwamba haya mafuta tumetia kwenye ndege yetu, kwa hiyo, kodi tuliyoilipa irejeshewe na wao wapate nafuu kama ilivyo hivi sasa bila kuamini makampuni ya mafuta. Kwa kitendo hiki kutakuwa kuna ongezeko la mapato, nina hakika. Watalaam wafanye mahesabu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunashauri kwa sababu tunaona inaweza ikafanya kazi, mapato haya ya ziada yatakayopatikana na unafuu utakaopatikana katika maisha ya wanachi, wananchi wenyewe wataridhika ikiwa tutapunguza bei ya usafirishaji, bei ya kilimo tukawaambia kwa sababu tumewapandishia mafuta ya taa, wataridhika kwa sababu hata hao wananchi wanaotumia mafuta ya taa tusiamini kwamba wanatumia sana mafuta ya taa kuliko kuni na mkaa. Mkaa unatumika mwingi sana, kuni zinatumika nyingi sana, uharibifu wa mazingira unazidi kuendelea.

Lakini mafuta ya taa pia kwa hali ya mwananchi wa kawaida kununua lita moja kwa siku hawezi, ni nyingi. Bei ya mafuta ya taa kwa lita moja kwa siku na kuni kwa bei hiyo hiyo, ataona anunue kuni kwa sababu gharama ni chini zaidi, lakini atazidi kukata miti na kuweza kuharibu mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapato hayo yatakayoongezeka, Serikali tunaweza kabisa tukaondoa ada ya Sekondari ikawa ni bure ambayo nchi za wenzetu majirani wameshafanya hivyo, ada ya Sekondari ni bure. Kwa sababu Sh. 20,000/= anayokwenda kulipa ada Sekondari, basi aitumie katika kununua hayo mafuta ya taa ambayo yamepanda bei.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile nafikiri hata soda hebu ibakisheni kama ilivyo maana yake mwisho watoto wetu hawatakunywa soda. Sasa hivi soda Sh. 500/= na unajua mtoto na soda, basi ile soda ambayo ninyi Serikali mmeongeza Sh. 5/= katika kodi, sasa hivi hebu irudisheni ibaki pale pale Sh. 58/= badala ya Sh. 63/= ili angalau

yule mtoto mdogo ambaye hajui soda inatengenezwa vipi lakini anaipenda ili abaki na matumaini ya kwamba baba yake au mama yake au kaka yake anaweza akamnunulia ile soda.

Mheshimiwa Naibu Spika, itafika mahali sasa soda itauzwa Sh. 1,000/=, ninyi mkiongeza Sh. 5,000/= huko kwenye soko wataongeza Sh. 500/=, wafanyabiashara wanapata faida. Kwa sababu hiyo, ndiyo wanafidia zile gharama nyingine za usafirishaji wa *diesel* katika malori na kadhalika, na kuleta vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeishauri Serikali ijaribu kuyafanyia kazi haya. Kitendo cha kuchakachua kina-*stabilise* nchi kwa hali mbaya kabisa. Ninyi mnaelewa na madhara yake yanaeleweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sitaki kurudia zaidi ya hayo ambayo yamekwishaongelewa isipokuwa tu naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na ninaunga mkono hoja Muswada huu wa fedha. Ninayo mambo machache ambayo ningependa kutoa ushauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijatoa ushauri huo, napenda kwanza kumsifu na kumpongeza Mheshimiwa Cheyo kwa kutumia akili na uhuru aliopewa na Mwenyezi Mungu na Katiba ya nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nataka niwaeleze Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba mimi sasa nina miaka mitano nafanya kazi na Mheshimiwa Cheyo katika Kamati moja. Mheshimiwa Cheyo ana akili nzuri sana na mimi nataka niseme hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hilo nilikuwa na ushauri kama ifuatavyo:-

NAIBU SPIKA: Hujafafanua, maana yake wengine hatuna akili?

MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, hapana. Nimemsema yeye, sijasema wengine hawana.

NAIBU SPIKA: Wewe fafanua basi.

MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naogopa dakika zitakwisha. Nataka kusema kwamba Mheshimiwa Cheyo sisi tunafanya naye kazi, ana akili nzuri kwa sababu ana uwezo wa kuwaelewa wenzake na kufanya kazi na wenzake vizuri na ndiyo maana hata shughuli zinazofanyika hapa, alizielewa vizuri ndiyo maana akaunga mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, nilitaka kutoa ushauri. Jambo la kwanza, Tanzania tunalima maua na kuuza Ulaya, hao hao Watanzania tunaagiza maua

bandia kutoka nje. Kwanini tuagize maua bandia kutoka nje? Napendekeza Serikali ifute uagizaji wa maua ya bandia ili tupate hela za kigeni, vinginevyo tuweke kodi kubwa sana kwa maua ya bandia.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, nataka nimsifu Waziri ninaposema jambo hili. Juzi, Serikali imetambua na yeye mwenyewe akasema kwamba kutoka sasa Serikali itanunua fanicha au samani kutokana na mbao zinazotengenezwa hapa hapa nchini.

Leo hii ukienda Ulaya, kila mahali, mti wa asili unaotengenezwa mbao kama hizi zinatoka kwetu ndiyo yenye thamani na inayoheshimiwa. Sisi wenye rasilimali hiyo tunaagiza mbao za ovyo, meza bandia kutoka nje. Kwa hiyo, naomba fanicha na vitu bandia vyote hivi tunavyoangalia viwekewe kodi ili tuongeze mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, sisi ndiyo wenye nafasi ya kuweza kuwa na viwanda vya kusindika mazao. Nina mapendekezo mawili, la kwanza, naomba Wizara ifanye utafiti wa kuona ni namna gani sekta ya usindikaji wa mazao inavyokuwa ili tuanze na sisi kuweka sera ya *subsidy* kwa sababu nchi za wenzetu sisi tunatembea unaona kwa mfano ukienda kwenye masoko ya mazao ya kusindika maziwa, nyama na vitu vingine, nchi nyingi wanatoa *subsidy* ndiyo maana sisi hatutashindana nao kwa kuwa sasa nchi yetu tumejiandaa kuingia kwenye viwanda vya kusindika, naomba na suala la *subsidy* tuanze kulitazama hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niipongeze Serikali. Safari hii wamefanya vizuri kweli, wamesamehe VAT katika vitu mbalimbali vitakavyozalishwa kutokana na kilimo ikiwa ni pamoja na vyakula vinavyotengenezwa kwa ajili ya kulisha kuku na mifugo na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, kwa kuwa Wizara hii ni Wizara ya Fedha na Uchumi, tusihangaikie kila wakati na hesabu za kodi bila kuangalia kukua kwa uchumi. Siri ya maendeleo na kuongeza kodi ni kuongeza uwezo wetu wa uzalishaji na maeneo ambayo tunaweza tukafanya vizuri zaidi ni kuongeza viwanda vya usindikaji vya mazao. Hivyo tuna nafasi kubwa kuliko nchi yoyote. Kwa mfano, juzi tumekuwa na ugomvi hapa, hatuelewani kuhusu kodi ya mafuta yanayoitwa *crude oil* ya kutoka Malaysia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli ni kwamba hakuna *crude oil* kutoka Malyasia ni *refined*. Lakini mimi nasema ugomvi huo hauna maana kwa sababu sisi tungesema kwamba wale wenye viwanda wote vya kusindika mafuta, waelekezwe waende Mikoani wakafanye mikataba na Mikoia ya kulimiwa mbegu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, waende Singida kwa ajili ya mikataba maana si wanajua *capacity* ya viwanda vyao waende Singida, waende Morogoro, waje Dodoma ili waingie mikataba na Mikoia kuwa na wakulima watakaowalimia kutosheleza mahitaji ya viwanda vyao. Kwa sababu kuendelea kungojea mawese ya Malyasia ni *cost* za kosa kiuchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili mimi nimekwenda Malyasia mara tatu na nilipokelewa na Waziri Mkuu mwenyewe wakati ule Martin Mohammed alipokuja Tanzania akamwaahidi Rais wetu akasema mkitaka njooni Malyasia, sisi tutawapa mbegu ya kisasa ya michikichi, eneo la kulima michikichi Tanzania ukichukua Kigoma, Rukwa, Pwani, Tanga na Morogoro ni kubwa kuliko eneo la Malyasia, lakini bado sisi tunaagiza hiyo inayoitwa *crude oil* kutoka Malyasia mpaka lini? Ndiyo swali tujiulize.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu wa Kenya wanasema Tanzania mngejitahidi, sisi tungenunua mbegu za mafuta kwenu, ninyi ndiyo mngekuwa nchi ya kwanza *East Africa* kutuuzia mafuta ya kupikia chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba tunapozungumza Kilimo Kwanza, tuweke suala la kujitegemea kwa mbegu kama sehemu ya Kilimo Kwanza kwa sababu mafuta pia ni chakula, matunda ni chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningependa kushauri na tukijitegemea tutaacha kungombana na haya mambo ya kodi, kwa nini hivi sasa Tanzania tunafika mahali tunaabudu dola? Tunakuwa watumwa wa biashara ya dola? Fedha ya Tanzania ndiyo imeandikwa kwamba ndiyo pesa halali ya biashara hapa. Hivi leo watu walioagiza bidhaa nje mwaka jana kwa ajili ya thamani ya fedha kushuka wanapata faida mara dufu kwa sababu wanatufanyia biashara kwa dola.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda madukani wanatoa *invoice* kwa dola, kila wakati Serikali imesimama kukanusha na imekemea, sasa nataka kujua leo, ni hatua gani itachukuliwa ili wanaofanya biashara ya dola wadhibitwi? Tutumie fedha yetu kwa ajili ya biashara ya kila siku na uzuri Tanzania tuna maduka yanayofanya biashara hiyo, kwa nini na wauza nguo na wauza mitumba na magari nao wameingia kwenye mchezo huo wa dola? Hii ni kuwaumiza wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ambalo ningependa kumalizia ni kwamba, hili jambo ambalo Waheshimiwa Wabunge wamesema sana la mafuta, mimi nashauri Serikali itume *delegation* kwenda kwa majirani zetu kwenda kueleza kwamba jambo hili limefanyika kwa uhuni na bahati mbaya, lisiwaharibie sifa nchi. Waelezwe kwamba siyo sisi tuliota, siyo Serikali, lakini ni wahuni wanaotaka utajiri wa haraka ndiyo wamefanya mambo haya, ili waendeele kuwa na imani na kujenga imani kwa Serikali yetu tuendeele kufanya biashara nayo. Hili ndiyo ombi langu la mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupewa nafasi. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Sasa wasipowafunga wahuni wale, wataamini vipi kwamba walikuwa wahuni?

MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ni njia mojawapo. Nakuunga mkono.

NAIBU SPIKA: Maana yake ni lazima hawa wahuni wawekwe mahali waonekane waseme kweli nia yao ilikuwa ni uhuni. Sasa ikiwa hivi hivi tu, kwa kweli inatia aibu sana na hasa baada ya magari ya Mheshimiwa Rais nayo kuonekana hakuna maana, mimi nadhani Serikali kweli hapa tuchukue hatua zinazostahili na ionekane kwamba tumechukua hatua. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyowaeleza, Waziri yuko peke yake, kwa hiyo, tunasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 ili kusudi aweze kupata ushauri wa wataalamu wake ili aweze kuwajibu hoja zenu vizuri. Tukirudi hapa jioni, jina nililionalo mbele ya orodha yangu ni Mheshimiwa Masilingi tu, basi. Lakini haizuii na wengine kuchangia. Kwa hiyo, nasitisha shughuli mpaka saa 11.00 jioni.

(*Saa 6.57 Mchana Bunge lilifungwa Mpaka Saa 11.00 Jioni*)

(*Saa 11.00 Jioni lilirudia*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, wakati tunaahirisha shughuli za Bunge Asubuhi nilikuwa nimesema kwamba orodha yote niliyokuwa nimepewa walipata nafasi ya kuzungumza isipokuwa Mheshimiwa *Senate* Wilson Masilingi tu. Karibu Mheshimiwa Masilingi.

MHE. WILSON M. MASILINGI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kushiriki kuchangia huu Muswada wa Sheria ya Fedha. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Muleba Kusini na kwa niaba ya familia yangu na kwa niaba yangu binafsi, natoa salaam za rambirambi kwa Mheshimiwa Jenista Mhagama - Mbunge wa Peramiho ambaye pia ni Mwenyekiti wa Bunge kwa msiba mkubwa uliomfika wa kufiwa na mume wake. Naomba Mwenyezi Mungu ampe nguvu katika kipindi hiki kigumu. Bwana ametoa na bwana ametwaa, jina lake lihimidiwe. Amin.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru Serikali kwa kuitikia kilio cha wananchi wa Muleba Kusini na kuanza kuchukua hatua za haraka haraka kushiriki mnyauko unaoshambulia migomba. Malengo ya bajeti hii ni kuchochea ukuaji wa haraka wa uchumi na kuondokana na umaskini na migomba, ikiisha umaskini utatimaliza.

Lakini Serikali imesikia kilio, chetu hatua zimeanza kuchukuliwa. Natoa wito kwa wananchi wa Muleba na Kagera nzima na wakulima wote wa migomba, ugonjwa huu hauna tiba, tumeridhishwa, sasa wasisite kung'oa migomba na kuchoma moto au kuizika mbali sana ili ugonjwa usisambae. Wasiogope, Serikali yao ipo, ina chakula cha akiba, tukihitaji mahindi na maharage watatupatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kunukuu Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kifungu 138, kabla sijazungumza ninayotaka kuchangia, Ibara ya 138 (1) imetoa mwongozo kwa Bunge hili kwamba hakuna kodi ya aina yoyote itakayotowza isipokuwa kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge au kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa kisheria na uliotiliwa nguvu kisheria na sheria iliyotungwa na Bunge. Haya ni maneno mazito sana ya kutuongoza katika Bunge hili na siku zote tulikuwa

tumeyarudiarudia tangu tumeanza Bunge hili la 20. Nataka kuyasititiza haya ili niseme yafuatayo:- Kwanza, ibara ya 138 imetoa fursa kwa Baraza la Mapinduzi la Zanzibar kuweza kutumia madaraka ya kutoza kodi kwa mamlaka iliyo nayo.

Sasa ushauri ninaotoa kwa Serikali ni kwamba katika hii *Finance Bill*, ibara ya 33, tumekuja na pendekezo zuri sana la kuweza kuzingatia mazingira maalum ya wazee wetu wastaafu hasa kwa kutambua kwamba ibara hii imeainisha kwamba mtu yeyote mwenye umri wa miaka 60 au zaidi au akiishi katika mazingira au katika hali ya kutokuwa na uwezo kama ulemavu na hana namna nyingine ya kupata kipato, basi mali yake isitozwe kodi kama vile nyumba.

Sio mara ya kwanza Bunge hili linajikita kujali matatizo ya wazee wetu waliotujengea misingi Taifa hili kuwepo katika hali tuliyonayo iliyoboreka zaidi kuliko hali zao za kimaisha. Sasa ninaona mapungufu kwa sababu nina imani kubwa na Serikali yetu, ni sikivu kwa mambo yote na ina uwezo, na ina mwanasheria Mkuu mwenye uwezo mkubwa. Ninaomba ushauri huu uzingatiwe. (*Makofi*)

Ibara ndogo tatu ya sheria hii ya *Urban Authorities Rating Act* ambayo ndiyo tunairekebisha kuwapa uwezo na haki yao wazee wetu na walemavu au watu wasio na uwezo kimaumbile kupata kipato wasitozwe kodi ya mali (*property tax*). Tusiwaachie Serikali za Mitaa.

Hii ni kazi yetu, Katiba imetupatia sisi kwa sababu katika Ibara ndogo ya nne mmeongeza kwa kusema, *The Local Government Authorities Shall Establish a Mechanism for Better Implementation of sub section, three* ambayo ndio nimeifanua kwa Kiswahili ya kuwapa kama upendeleo maalum wazee wetu wa miaka 60 na kuendelea na Wabunge wengi ambao hawatachaguliwa hapa wenye miaka 60 na kuendelea watajikuta wana nyumba moja Dar es Salaam na hata Miji mingine hawatakuwa na uwezo wa kulipa kodi. Tusiachie sasa watendaji wa mitaa na Serikali za Mitaa kuweka utaratibu wa kumchambua ni nani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri hili kwa sababu tuliposema wazee wa miaka 60 wapate matibabu bure tukaweka neno lisilokuwa na ufafanuzi sahihi kwamba wasio na uwezo, Tanzania ni wazee wachache wanaofikisha miaka 60 mitaani na vijijini wenye uwezo. Heri tuwaachie sasa. Anasema wana uwezo athibitishie yeye, siyo wao wajithibitishie kwamba wana uwezo waende kwa watendaji wa vijiji kwa wale wanaokwenda kutibiwa bure kwenye Hospitali za Serikali na kwa hizi kwa sababu inahusu mambo ya Mijini, mali Mijini au Miji Midogo kwamba isitozwe kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, huo ni ushauri ambao nawaomba kabisa ibara ndogo ya nne. Sikuja na taarifa ya awali ya kuwasihii Wabunge wenzangu, mniunge mkono ifutwe, Serikali hii ni sikivu. Hiki kipengele hakina maana, kinapingana na Katiba kabisa. *The Local Government Authority shall establish a mechanism for better implementation of subsection three.*

Masuala yote, hata tulipoanzisha Serikali za Vijiji na Mitaa Ibara ya 145 na 146 imekuwa wazi kabisa, shughuli zao bado inatuachia sisi Bunge, ndiyo tunapaswa kuweka utaratibu wa utekelezaji wa shughuli za vyombo hivyo. Sisi sio wao, wanajiwekea utaratibu wa utekelezaji wa mambo ambayo yanahusu maslahi ya watu waliotupigia kura na hususani wazee.

Kwa hiyo, hii mimi nitakaa vilevile na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa sababu mwezi Novemba tutakutana tena hapa tusipoelewana nitakuja na Muswada maalum, muangalie hii kitu ya kuwa sisi madaraka ya Bunge tunaachia hawa watu ambao wengi wanakiuka maadili na wanasumbua wazee wetu, tuseme na hii tu itatupa heshima. Mzee wa miaka 60 nyumba moja ina vyumba sita anapangisha msimfuatufuate, uwezo gani mwingine? Ni kilema, ana nyumba moja, mnamfuatafuata nini? (*Makofi*)

Mtendaji akisema ana uwezo awaambie *TRA*; *TRA* ni wastaarabu wametokusanyia kodi za kutosha na tunapata kodi za kutosha bila kukopa, nawapongeza sana. Tusitoe madaraka yetu, kwa hiyo hii Ibara ya nne mkifuta hampotezi kitu, sina muda wa kuleta *notice*, mkichelewa vitazuka mwezi wa Kumi na Moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, muda umekwisha na nilikuwa na hilo.

NAIBU SPIKA: Bado, ni kengele ya kwanza.

MHE. WILSON M. MASILINGI: Mheshimiwa Naibu Spika, bado nina muda, *Okay* hilo la kwanza. Sasa nitaongeza lingine kwa sababu hilo ndilo lilikuwa limenikera mno kwa sababu linagongana na madaraka yetu ya kikatiba ya kutunga sheria na kuweka utaratibu, halafu sisi tunasema utaratibu uwekwe na wengine na mmeona nifafanue zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwenye Kijiji changu kimoja huko kuna Mwenyekiti, anatembea na muhuri mpaka leo kwa sababu Mtendaji wa Kijiji amesimamishwa kazi. Mwenyekiti huyo anasema usiponiona vizuri sikuwekei muhuri, akajaribu kuwanyima watoto wanaokwenda *Form One*, *Head Master* kachukua madaraka ya muhuri wake *fake*, akasema nitawawekea wa kwangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu *Head Master* yule alikuwa na uchungu na watoto akasema, kama Mwenyekiti wa Kijiji hawezi kuweka muhuri, mimi si nina wa kwangu, njoo mtasoma. Sasa utapata *Head Masters* wangapi wenye ujasiri huo?

Wazee wetu wananyimwa dawa za bure kwa sababu Watendaji kutoa barua ya kwamba mzee hana uwezo ni mpaka abembelezwe. Sasa hii sitaki tuirudie. Mwanasheria Mkuu wa Serikali najua ni rafiki yangu atalitifakari, kama haina haraka sasa hivi, mtashughulika baadaye, mtafuta huko, mkichelewa tutaonana mwezi wa Kumi na Moja. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo napenda kuchangia hapa ni lile la ibara ya 27 Ibara ndogo kwenye Muswada. Tumesema:

“The Controller and Auditor General shall after studying the matter report the fraud or any related offences to an appropriate investigative organ and serve a notice to the director of Public Prosecutions.” Mwisho wa kunukuu. Kwamba Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali baada ya kuchunguza jambo hili ni masuala ya ku-audit mambo kwa ajili ya thamani ya fedha mahususi kwa miradi inayotekelezwa, atatoa taarifa kuhusu masuala hayo kwa chombo ambacho kinahusika na uchunguzi ili kiweze kuchunguza na baadaye kutoa taarifa kwa Mkurugenzi wa Mashitaka ya Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi ninajiuliza hapa Bunge tuna vyombo vyote tunavitengeneza sisi, chombo cha Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa tumekizaa sisi hapa tukakipa jina, sasa *appropriate organ* maana yake nini? Weka *PCCB* hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunisikiliza naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Haizuii kama Waziri hatakusikiliza, haikuzuii, tukifika katika kifungu hicho utarudia tena kusudi upate maelezo dhahiri. (*Makofi*)

Kama nilivyosema katika orodha yangu kwa mchana walibakia Mheshimiwa Masilingi tu, sasa tulikuwa na mashaka kama Masilingi angemaliza, sasa ingekuwaje. Tunashukuru umekuja lakini siyo utaratibu mzuri. Sasa namwita Mheshimiwa Mtoa hoja.

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba radhi kwamba nimechelewa kufika, tulikuwa tunajitahidi kuandaa majibu ya hoja zilizojitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia Muswada huu kwa kuzungumza hapa Bungeni na wale waliochangia kimaandishi. Naomba niwatambue Waheshimiwa Wabunge hawa kwa majina kama ifuatavyo:-

Waliochangia kwa kuzungumza ni hawa wafuatao:- Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda -Mbunge wa Handeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu - Mbunge wa Kuteuliwa kwa niaba ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi - Mbunge wa Mbozi Mashariki, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed - Mbunge wa Wawi, Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga - Mbunge wa Tabora Mjini, Mheshimiwa Pindi Hazara Chana - Mbunge wa Viti Maalum Iringa, Mheshimiwa John M. Cheyo - Mbunge wa Baridi Mashariki, Mheshimiwa Zaynab Matitu Vullu - Mbunge wa Viti Maalum Pwani, Mheshimiwa William H. Shellukindo - Mbunge wa Bumbuli, Mheshimiwa Injiniya Mohamed Habib Juma Mnyaa - Mbunge wa Mkanyageni, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah - Mbunge wa Pangani, Mheshimiwa Dr. Chrisant M. Mzindakaya - Mbunge wa Kwela na mwisho Mheshimiwa Wilson Masilingi - Mbunge wa Muleba. (*Makofi*)

Waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Shoka Khamis Juma - Mbunge wa Micheweni, Mheshimiwa Eustace O. Katagira - Mbunge wa Kyelwa, Mheshimiwa Martha Umbulla - Mbunge wa Viti Maalum Manyara, Mheshimiwa Juma H. Killimbah - Mbunge wa Iramba Magharibi, Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo - Mbunge wa Viti Maalum Singida, Mheshimiwa Zainab M. Vullu - Mbunge wa Viti Maalum Pwani, Mheshimiwa Fatma A. Mikidadi - Mbunge wa Viti Maalum Lindi, Mheshimiwa Mohamed Missanga - Mbunge wa Singida Kusini, Mheshimiwa Lucas L. Selelii - Mbunge wa Nzega, Mheshimiwa Pindi H. Chana - Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Felister A. Bura - Mbunge Viti Maalum Dodoma, Mheshimiwa Profesa Philemon M. Sarungi - Mbunge wa Rorya, Mheshimiwa Hawa Abrahaman Ghasia - Mbunge wa Mtwara Vijijini na Mheshimiwa Salum Khamis - Mbunge wa Chambani. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi kwa maoni na ushauri wao na pia kwa kuunga mkono Muswada. Aidha, napenda pia kutoa shukrani zangu kwa Kambi ya Upinzani kwa maoni na ushauri wao pia. Ninaahidi kwamba Serikali itayafanyia kazi maelekezo na mawazo mazuri yaliyotolewa na Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi na Kambi ya Upinzani. Naomba nianze sasa kujibu hoja mbalimbali kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge kwa ujumla kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba korosho iwekewe mikakati maalum ya kuboresha zao hilo. Bodi ya Korosho ikishirikiana na wadau, ina mikakati ya kuendeleza sekta hii ikiwa ni pamoja kuhamasisha ubanguaji na kuongeza uzalishaji. Asilimia 65 ya ushuru wa korosho ghafi inayosafirishwa nje ya nchi itatumika kwa kuwezesha kufanikisha shughuli hizo kwa ushirikiano wa wadau mbalimbali wa sekta ya korosho.

Hoja ya pili ilihusu mgawanyo wa fedha zinazotokana na ushuru wa korosho kulingana na uzalishaji kiwilaya na ukusanyaji wa mapato kwa *TRA*. Bodi ya Korosho Tanzania inasimamia mchakato mzima wa usafirishaji wa korosho nje ya nchi kwa kutumia nyaraka mbalimbali za usafirishaji nje ya nchi.

Msafirishaji wa korosho nje ya nchi anatakiwa aombe kibali Bodi ya korosho ambacho kitamwezesha kufanya hivyo. Kabla ya kupata kibali anatakiwa aeleze korosho hizo amezinunua Wilaya gani kwa kuwasilisha kwenye Bodi nyaraka iitwayo *PDN au Procurement Dispatch Note*. *PDN* ni nyaraka inayotayarishwa na Bodi na kusambazwa kwenye vyama vya ushirika kupitia Halmashauri husika.

Kupitia *PDN*, hizo bodi inakuwa na takwimu zinazoonyesha ununuzi wa korosho kutoka katika kila Halmashauri na kwa zile zinazosafirishwa nje ya nchi zikiwa ghafi zinatambulika kwa takwimu, hivyo kila Wilaya inaeleweka ilizalisha korosho kiasi gani na kiwango gani kilichosafirishwa nje ya nchi hujulikana kiwilaya.

Katika ukusanyaji wa mapato kwa *TRA*, Bodi ya Korosho ndiyo inayosimamia bandari ujazo unaosafirishwa na mhusika kwa kutoa kibali cha usafirishaji, yaani *export permit* mpaka aonyeshe malipo aliyoyafanya *TRA* ndiyo hupewa kibali hicho. Aidha,

Bodi ya Korosho Tanzania ikishirikiana na wadau wa sekta, itaweka mikakati na mipango ambayo itahamasisha ubanguaji kwa kuanzisha viwanda vidogo vidogo kwa kutumia sehemu ya ushuru wa asilimia 65. Uanzishaji wa viwanda vidogo utakwenda sambamba na utoaji wa elimu ya ubanguaji kwa wenye viwanda vidogo na wajasiriamali wadogo. Kwa kufanya hivyo, suala zima la ubanguaji korosho nchini litaongezeka.

Hoja nyingine ilihusu kupiga marufuku uingizaji wa mafuta usiofaa kwa afya. Bidhaa ambazo hazikidhi viwango chini ya sheria ya *TBS* haziruhusiwi kuingizwa nchini. Kodi kwenye muda wa maongezi kwenye simu ipunguzwe. Tunajibu kwamba marekebisho yaliyofanywa kwenye Muswada wa Sheria ya fedha hayajalenga kupandisha kodi isipokuwa ni kufafanua *base* inayotumika kukokotoa kodi.

Hoja nyingine ilihusu kupunguza misamaha ya kodi. Tunajibu kwamba hatua zimechukuliwa na misamaha imeshuka kutoka asilimia tatu ya *GDP* mwaka 2008/2009 hadi asilimia mbili ya *GDP* mwezi Machi, 2010. Hatua zitaendelea kuchukuliwa ili kuhakikisha kwamba misamaha ya kodi inaendelea kushuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, malimbikizo ya *tax areas*, tunajibu kwamba *TRA* imeweka mkakati wa kukusanya *tax areas* ili zisizidi asilimia tano ya *current assessments*. Hatua hii itaondoa tatizo na malimbikizo ya *tax areas*. Maduka ya kubadilisha fedha na vituo vya petroli hayatoi stakabadhi ya kubadilisha fedha na vituo vya petroli havitoi stakabadhi, hivyo kupoteza mapato. Tunajibu kwamba biashara ya kubadilisha fedha na vivutio vya mafuta, yaani *petrol stations* hazitakiwi kisheria kujisajili na *VAT* kwa vile bidhaa za mafuta ya petroli na maduka ya fedha zimesamehewa kodi ya *VAT*.

Hata hivyo, kwa mapendekezo ya kurekebisha sheria ya kodi ya mapato, kila mfanyabiashara ambaye hajasajiliwa na *VAT* sasa atalazimika atoe stakabadhi ili biashara za kubadilisha fedha na vivutio vya mafuta na magereji ambayo mengi yako chini ya kiwango cha usajili wa *VAT*, yaani *VAT Threshed* zitafuatiliwa ili ziweze kutoa stakabadhi.

TRA itatekeleza mpango huu wa maendeleo ya miaka mitano ambao unafanywa kwa njia ya vitalu, yaani *block management system*. *TRA* itaendelea kuwakagua walipa kodi wote ili kuhakikisha kuwa wanatoa stakabadhi na wanalipa kodi stahili.

Hoja nyingine ilihusu Serikali kuongeza kila mwaka kodi kwenye vinywaji baridi. Tunajibu kwamba ushuru wa bidhaa ulioongezwa ni kutokana na mfumuko wa bei na hivyo ni kulinda thamani ya mapato ya Serikali. Vile vile haya ni makubaliano maalum baina ya Serikali na viwanda vinavyotengeneza soda, bia na sigara. Hoja ya kutotoza ushuru katika kusafirisha maua kwa ndege, faida yake ni ndogo sana kwa kuwa inahusisha watu wachache.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajibu kwamba, msahama huu wa kusafirisha maua ni sehemu ya mauzo ya nje, yaani *part of exports*, yaani inapaswa kutozwa *VAT* kwa kiwango cha sifuri, yaani *zero rated*. Hatua hii itasaidia ushindani wa maua ya Tanzania kwenye Soko la Dunia.

Aidha, hatua hii itawezesha sekta hii kukua na kuchangia Pato la Taifa. Hoja nyingine ilihusu mashine za kutolea risiti zihusishe walipakodi wadogo wadogo kwa *TRA* kuzinunua na kuwakopesha ili walipe taratibu. Tunajibu kwamba, Serikali imepanga kuanza na walipakodi wachache wanaolipa *VAT* ili kuona mafanikio na changamoto zitakazojitokeza na hivyo kujipanga vyema wakati wa kuanza kutumiwa na walipakodi wote.

Hoja nyingine ilihusu kuondoa *VAT* kwenye vifungashio vya madawa za binaadamu, tunajibu kwamba madawa ya binadamu yanayotengenezwa hapa nchini yanatozwa *VAT* katika kiwango cha sifuri. Kodi ya Ongezeko la Thamani wanaolipa kwenye vifungashio, yote hurejeshwa kwa watengenezaji wa madawa haya. Kwa hiyo, hakuna kodi inayokwenda kwa mlaji. Mahitaji mengine yatafanyiwa kazi katika mwaka ujao wa fedha. Kodi za pikipiki ziondolewe kwa kuwa ni gharama kwa wananchi masikini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajibu kwamba, pikipiki nyingi kwa sasa zinatumiwa kibiashara ambayo kimsingi inafanyika katika sekta isiyo rasmi. Kutoza kodi kwenye vyombo hivyo, ni njia mojawapo ya kuingiza sekta hiyo katika mfumo rasmi ambayo ndio azma ya Serikali.

Ada ya usajili iliyoelezewa na Waheshimiwa Wabunge ya Sh. 45,000/= hutozwa mara moja tu wakati pikipiki hizo zinaponunuliwa na kusajiliwa na haiwezi kuathiri bei ya mlaji kwani pikipiki nyingi ambazo sasa ziko kwenye biashara hiyo hazitalipa ada ya usajili kwa sababu zilishasajiliwa tayari.

Hoja nyingine ilihusu msamaha unaotolewa kwenye makampuni ya madini kwamba utolewe pia kwa wakandarasi wa ndani. Ushauri huu ni mzuri, tumeupokea na tutaufanyia kazi wakati wa kuangalia mikataba ya uendelezaji madini, yaani *MDA's*. Kinachozungumzwa kwenye makampuni ya madini ni *sub-contractors* badala ya *contractor* wa ndani. Kwa hiyo, hili litashughulikiwa wakati tunaitazama ile mikataba upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilihusu Mkaguzi Mkuu wa Ndani kuwa chini ya mamlaka ya Mlipaji Mkuu wa Serikali badala ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Uchumi. Kupitia jedwali la pili la marekebisho lililowasilishwa na ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Marekebisho yamefanyika kwa kurekebisha kifungu kipyaa cha 37 kinachopendekezwa kupitia kifungu cha 27 cha Muswada ili kubainisha kwamba Mkaguzi Mkuu wa Ndani atakuwa ndani ya muundo wa Wizara yenye dhamana na masuala ya fedha.

Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 38 kinachopendekezwa kupitia kifungu cha 27 ukurasa wa 12 wa Muswada, Mkaguzi Mkuu wa Ndani atawajibika kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa hivyo, hoja ya Mheshimiwa Shellukindo ilishafanyiwa marekebisho tayari.

Hoja, kurekebisha kifungu cha 27(a) cha Muswada ili kuondoa maneno *one hundred thousands* na kuweka *one hundred and twenty thousands* ili kuhuisha na takrimu zilizopo kwenye Muswada, Sheria ya Magari, yaani kodi ya usajili na uhamishi wa wamiliki wa magari, sura ya 124 kama ilivyo hivi sasa, imebainisha kimakosa kwamba kodi ya usajili wa magari ni kiasi cha *one hundred thousand* shillings, marekebisho yaliyobainishwa kupitia ukurasa wa kumi na moja katika Muswada, yana lengo ya kurekebisha makosa ya kiuandishi yaliyopo kwenye sheria ya sasa. Kwa hiyo, tunakiri kwamba kulikuwa na tofauti kati ya maneno na tarakimu, lakini yameshafanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilihusu kwa nini hatupati pesa kutoka kwenye ukanda maalum wa uvuvi wa *exclusive economics zone*. Uvuvi katika ukanda wa bahari kuu au *deep sea fishing* unasimamiwa na mamlaka ya uvuvi katika bahari kuu, yaani *deep sea fishing authority* ambacho ni chombo cha Muungano. Mamlaka hii imeanzishwa kwa ajili ya kusimamia uvuvi katika bahari kuu. Chombo au mamlaka hii ndio yenye mamlaka ya kukusanya mapato yatokanayo na uvuvi katika eneo hili. Kwa hiyo, mapato yote yanayotokana na leseni za namna hiyo yameoneshwa kwenye shirika hilo na hayawezi kujionyesha kwenye bajeti hii ya Serikali.

Msamaha wa kodi wa majengo kwa wazee na walemavu, kupitia jedwail la pili la marekebisho kifungu cha 33(a) cha Muswada, kimefanyiwa marekebisho ili kubainisha kwamba msamaha wa kodi ya majengo utatolewa kwenye nyumba moja ya kuishi kwa wazee wenye umri wa mika sitini au zaidi na walemavu ambao hawana kipato.

Uchakachujaji wa mafuta, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mbali mbali kuhusu suala hili linalotia aibu Taifa letu. Serikali imeanza kuchukua hatua za haraka za kudhibiti uchakachujaji wa mafuta ikiwa ni pamoja na kuweka maafisa maalum kwenye vituo vya ukaguzi wa magari yanayokwenda nje ya nchi, yaani *transit check point* kwa kushirikiana na *EWURA* watakuwa na vifaa maalum vya kufanyia ukaguzi. *EWURA* watatumia *mobile laboratory* katika kukagua mafuta hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo yanayoonekana kuhusika na uchakachujaji yanatafanyiwa ukaguzi na usimamizi muda wote. Katika hatua za muda mrefu, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia itaanzisha mfumo wa *cargo tracking system* utakaoweza kulifuatilia gari lenye mzigo popote lilipo na iwapo itatokea linakwenda nje ya njia lililopaswa kupita kengele au *alarm* itaonyesha na Afisa wa kituo cha jirani atalifuatilia.

Aidha, Serikali imeyapokea maoni kuhusu suala la kuhainisha bei ya dizeli na mafuta ya taa ili kuondoa kichocheo cha kuchanganya mafuta na kwamba italifanyia kazi. Serikali itashughulikia adhabu za kutoa katika kosa hili na tumechukua pia ushauri wako Mheshimiwa Naibu Spika kwamba haifai tu kuchukua hatua ndogo ndogo, inafaa watu hawa wafungwe, lakini huo ni mchakato ambao Serikali utaufanyia kazi na adhabu husika itatekelezwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, naomba kutoa hoja.

(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)

KAMATI YA BUNGE ZIMA

Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2010

(The Finance Bill, 2010)

Kifungu cha 1
Kifungu cha 2
Kifungu cha 3
Kifungu cha 4

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 5

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)

Kifungu cha 6
Kifungu cha 7
Kifungu cha 8
Kifungu cha 9
Kifungu cha 10
Kifungu cha 11
Kifungu cha 12
Kifungu cha 13
Kifungu cha 14

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 15

MHE. ISMAIL JUSSA LADHU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara ya 15, kwenye kifungu kipya cha 80 A Kambi ya Upinzani tulipendekeza kwamba kile kifungu kidogo cha 2(d) ambacho kinataka katika yale jumla maelezo yanayopashwa kuwemo katika ile stakabadhi ya risiti ni pamoja na *full name and address of the person*, tulipendekeza kwamba lile neno 'address' liondoke kwa sababu kama ulivyosema Tanzania bado haijaweka utaratibu huu, inaweza kuleta usumbufu zaidi kuliko kusaidia katika shughuli hizi.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba ibaki kama ilivyo kwa sababu *address* tunayozungumza hapa inaweza kuwa ni *physical* au *postal*.

MHE. ISMAIL JUSSA LADHU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema kwa yote mawili bado inaweza kuleta usumbufu kwa sababu tukichukulia jumla ya Watanzania wangapi wanazo hizo, *physical address* tunakubaliana kwamba hazijawekwa utaratibu, lakini hizo *postal address* ni wangapi katika Watanzania wa kawaida wanaweza kuwa nazo kiasi ambacho hata katika yale mauzo ya Sh. 5,000/= tu au zaidi ya ambayo yanatajwa yanapaswa yatolewe risiti?

Kwa hiyo, nasema bado haijajibu hoja na nadhani inaweza tu kuleta usumbufu pengine kusababisha watu kuja kufungwa kwa sababu kuna *penalties* huko mbele kwa kugushi nyaraka kwa sababu atakuwa hawana *address proper* ambazo zitapashwa kuingizwa katika risiti hizi, kwa hiyo, ningepomba tu kwamba Serikali ikubaliane na sisi liondoke wala haliathiri lolote kwa upande wa Serikali.

MWENYEKITI: Mimi ninavyoona tatizo sio la kisheria ni la kiutekelezaji ambalo litatekelezwa kufuatana na maoni mliyotoa ninyi.

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)

Kifungu cha 16

Kifungu cha 17

Kifungu cha 18

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 19

MHE. ANDREW J. CHENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi niweze kutoa ushauri kwanza wa kiandishi tu kwenye mstari wa kwanza, hilo neno ‘abide’ linapashwa liwe ‘abides’ na msitari wa mwisho.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge, ngoja tuzungumze, tuko ibara ya ngapi?

MHE. ANDREW J. CHENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 19 kifungu kidogo cha tatu kinachoingizwa.

MWENYEKITI: Cha tatu, ok. Tuendele tafadhali.

MHE. ANDREW J. CHENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi ukasema *a consultant who abide*. Kwa hiyo, Kiingereza tu hapo, lakini nitarudi tena hapo baadaye

na kwenye msitari wa mwisho kwa sababu lengo ni ku-*buy from*, sasa neno ‘*and*’ nashauri liondolewe *from practicing*.

Sasa hapa nina dhana moja ya msingi sana na ningelipenga Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali atusaidie. Iliyokaa, dhana ni nzuri sana lakini kwenye makosa haya ya jinai unataka uipate ile dhamira yake kwamba alikusudia kufanya kitu fulani, sasa mimi nilikuwa nashauri tuangalie uwezekanaji wa kusema ‘*unapproved tax consultant who knowingly,*’ akijua *or recklessly* kwa kutokujali kabisa anamwambia *you know* fanya namna hii kwa lengo la ku-*evade tax* kutoa a *misleading*. Kwa sasa hivi imekaa bila hata ku-*create* hiyo tunaita kwa sheria ile *mensrea*.

Sasa mimi napendekeza baada ya neno ‘*who*’ tuseme *knowingly or recklessly abides*. Na mara nyingi unapoinzisa neno ‘*abides*’ unataka yaendane kama wanasheria wanavyojua, *adding, abating, counselling* na *inducing* yote haya *you know* unakwenda nayo, lakini kama hawataki kufika huko nataka tu lile la Kiingereza likae.

Ningelisema: “*who knowingly or recklessly abides a tax payer*”, na tuondokane na *towards*. Ukimwambia, *towards filing* ni kitu gani? Unataka tu uende *straight, a tax payer, to file a misleading or Fordland statement. shall be disqualified and banded from practising*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakuwa ni *straight* kabisa umeshapata ile, alikusudia kabisa kumfanyia haya *knowingly or recklessly* ndiyo hayo Mwenyekiti nilikuwa nasema nikijaribu kuingiza hapo ku-*capture concept* ya *mensterer*.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa kifungu hicho kisomeke kama ifuatavyo; “*An approved Tax Consultant who knowingly or recklessly aids, abets, conceals or induces a taxpayer to file a misleading or fraudulent statement commits an offence under this Act.*” Nafikiri tutakuwa tumekidhi haja ambayo Mheshimiwa Andrew Chenge ameizungumza. Nafikiri ni sawa sawa kwamba ni lazima u-*create* ile *mental status* yaani *man’s rare* kabla hujaanza kum-*punish* huyu *Tax Consultant*.

MWENYEKITI: Naomba usome tena. Tunaomba urudie.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Tunachofanya Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kufuta neno, baada ya neno *who*, tuongeze maneno *knowingly or recklessly* na neno linalofuata ni *abets* ongeza *s and then* baadaye ufute *and* kwenye mstari wa pili ile *and* ya mwisho, ufute pia na *bad* na ufute *and* inayofuata. Kinasomeka Kiingereza na linasomeka vizuri, tunamshukuru Mheshimiwa Chenge.

MHE. SIJARU J. KABOYONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mjadala unaliokuwepo kwenye Kamati pamoja na masahihisho haya mazuri yaliyofanywa. Lakini ilisisitizwa kwamba mshauri huyu afikishwe Mahakamani. Sasa hapa haijitokezi dhana ya kumfikisha Mahakamani na kwamba atafungiwa. Sasa nani atakayethibitisha kwamba *knowingly or unknowingly* alifanya makosa hayo.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi watu hawa wanazo *professional bodies* ambazo zinawabana katika maadili ya kazi yao. Sasa ni kupeleka Mahakamani, mimi nachelewa sana kila kitu tunapeleka Mahakamani. Nafikiri tungeishia kwenye hizo *professional bodies*.

MHE. SIJARU J. KABOYONGA: Kwa maana hiyo Mheshimiwa Mwenyekiti, iwekwe basi kwenye kipengele hiki kwamba *irrelevant professional body will commit this Consultant* kwenye hii *penalty*. Maana vinginevyo ina-*hang* tu.

MWENYEKITI: Mimi nilivyoelewa Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu...

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana ya kuongeza maneno hayo nafikiri inakubalika kwamba *disqualification* ije baada *professional body* kufanya *inquiry*. Maana yake nayo hiyo wakifanya *inquiry* ndiyo wana-*disqualify*. Hawawezi ku-*disqualify* tu kwa sababu mtu amelalamika kwamba alidanganywa. Sasa sielewi tena, nafikiri kabla sijamaliza, naomba Waandishi wa Sheria watengeneze maneno yenye kuonyesha kwamba ni *professional body* itakayofanya hiyo *inquiry* na kutoa adhabu inayopashwa. Tutawapatia *version* kabla hatujamaliza hapa.

MWENYEKITI: Ahsante. Kwa hiyo tulishakubaliana kwamba kifungu kinapita, lakini tutasubiri maneno hayo wakati tutakapokuwa tunarudi tena.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilisubiri Wanasheria kukiandika upya)

Kifungu cha 20

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 21

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)

Kifungu cha 22

MHE. JOHN M. CHEYO: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatumaini Kifungu cha 22 kama inavyosomeka kwenye kitabu hiki ambayo inazungumzia mambo ya *CESS*.

MWENYEKITI: Sasa ile ya 21 basi. Kama tunayotaja sisi tuko kwenye 21 ya kwenye kitabu, lakini baada ya mabadiliko ya kuongeza Kifungu cha 20, hii inakuwa Kifungu cha 22.

MHE. JOHN M. CHEYO: Kwa hiyo ile itakuwa ni ya 22, itakuwa ni ya 23.

MWENYEKITI: Eee sawa 23.

MHE. JOHN M. CHEYO: Basi nitasubiri hiyo Ibara itakayotajwa.

MWENYEKITI: Sawa sawa.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 23

MHE. JOHN M. CHEYO: Wakati nazungumza, Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema kwamba jambo hili la *CESS* watu ambao wanalipa *CESS* ni wafanyabiashara na imeandikwa hapa moja kwa moja. Lakini pia nililiambia Bunge lako Tukufu kwamba kwa sasa hivi inaonekana ni kama uhusiano wa madai na mdaiwa hauonekani kwamba ni msimamo wa kodi na hakuna mahali popote huyu mtu asipolipa *CESS* anafanywa kitu gani. Hakuna kabisa katika Sheria. Kwa hiyo, nilikuwa nauliza kama kulikuwa na njia ya kuweza kuweka namna fulani ya kuwabana hawa watu waone hii ni kodi na siyo fedha inayokopeshwa kwao na Halmashauri na kwa hiyo, pawepo na kitu cha kuwabana, wasipolipa, aidha, wanafungwa au wanafanywa nini au wanapeleka Mahakamani, lakini iwekwe wazi. Kwa hiyo, ningependa Mheshimiwa Waziri anipe ufafanuzi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri au nani, si umemwelewa? Anachotaka huyo mtu ambaye hajafanya hivyo, anachukuliwa hatua gani. Kwa sababu inakuwa kama ni kudai, mnaweza kudaiana wee mpaka msieleweke.

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Naibu Spika, *CESS* hii inasimamiwa na wenzetu wa *Local Government*. Sasa hiki kifungu ni *enforcement*. Sina hakika kama

MWENYEKITI: Sijui kwetu sisi *CESS* tumewapeleka watu Mahakamani, wamelipa.

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, unawapeleka watu Mahakamani inakuwa ni kesi ya madai. Sasa mimi nasema kama tumeiweka hii na ndani ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri, amesema mapato ya Serikali kutoka *Local Government* ni shilingi bilioni 178 ambayo ni mojawapo, ni vitu kama hivi *CESS*. Sasa mapato mengine yote yana-*sanctions* kwamba usipofanya hivi utapata hiki. Lakini inapokuja kwa *CESS* tunakuwa kimya, ndiyo maana hawa wanaweza kuwazungusha hizi Halmashauri miaka hadi miaka. Bariadi kuna watu tunawadai tangu mwaka 2004 na hii siyo mambo ya kukopeshana. Hii ni kulipa kodi ya Serikali, *so* usipolipa *there should be a sanction*. Kama wengine wote usipolipa leo *TRA* wanakupeleka Mahakamani, siyo kukudai, *you will go to jail*.

MWENYEKITI: Nani anayejibu, Mwanasheria Mkuu wa Serikali au Waziri. Yeye anasema *Local Government*, mnasema nini hii? Mheshimiwa Chenge, yuko Bariadi kwenu. (*Kicheko*)

MHE. ANDREW J. CHENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme masuala ya Bariadi tuwaachie watu wa Bariadi. Nimemwelewa vizuri sana Mheshimiwa Waziri, kwa sababu huo ndiyo utaratibu. Masuala haya yaachiwe Halmashauri zenyewe kwa utaratibu uliomo katika Sheria husika za Serikali za Mitaa na *CESS* huwezi ukai-*criminalize*, ni madai ya kawaida tu, unamdai hii, nitalipa kwa utaratibu ambao tumejiwekea.

Kwa hiyo, huwezi ukasema kwamba aburuzwe Mahakamani kwa *criminal case* au kwa kosa la jinai. Haya ni madai tu. Kwa hiyo, wahusika kama wapo, wameenda Mahakamani, masuala haya yaachiwe yaende Mahakamani tu kama ilivyo kawaida. Nakushukuru sana Mwenyekiti.

MWENYEKITI: Sisi kwenye Halmashauri yetu kwa kweli walikuwa hawalipi hii *CESS* ya zile mbao, walikuwa hawalipi, tulikuwa tuna kiwanda cha *Small Kiberiti*, walikuwa hawalipi. Sasa hivi wanalipa, tumewapeleka Mahakamani wamelipa na sasa tumeshakubaliana wanaendelea kulipa. Lakini tuliwapeleka Mahakamani kwa kesi ya madai na tunalipwa. Mheshimiwa John Cheyo nimeona umesimama tena.

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza mimi nataka kusema kwamba hili siyo jambo la Bariadi tu.

MWENYEKITI: Aaah Bariadi tuache, ni mimi niliyesema hivyo.

MHE. JOHN M. CHEYO: Ukienda *across* kila Halmashauri ina matatizo haya. Kwa hiyo, mimi nilikuwa sizungumzii Bariadi, nimetoa tu kama mfano, hiyo moja. Lakini mimi nasema *I think* tukubali kwamba huu ni udhaifu. Kwa sababu kama tunai-*classify* kama kodi halafu tunakuja kuiangalia kama madai tu na kwa kauli aliyosema Mheshimiwa Andrew Chenge hakuna atakayelipa *CESS*, watakuambia tutakutana Mahakamani.

Mimi labda ninakubaliana na wale wazungu wanasema *to abolish*, maana yake hakuna atakayelipa, ni kama silipi tutakutana Mahakamani. Sasa na Halmashauri zetu hizi hazina fedha, Halmashauri zetu hizi hazina mawakili ambao ni wazuri, hazina fedha za kuweka na huyu ni tajiri. Sisi tutakuwa hatuna hela, ndiyo nilikuwa nasema, *I think* kama vile ni *criminal case* kutolipa, ku-*evade tax* sioni kwa nini hii isiwe *classified as a tax* ambayo imeandikwa kwenye Sheria, Sheria ya jambo hili tunapitisha *A Finance Act* na pia imetajwa kama mapato ya Serikali ndani ya Bajeti ya Serikali, *why should criminalized*.

MWENYEKITI: *Actually* hii *institution of memory*, kabla ya kuweka kifungu kama hiki Halmashauri zilikuwa zinatoza kiwango chochote kile, ikawa ugomvi mkubwa kati ya Halmashauri na wananchi, wakulima. Kwa sababu kwa kuweka zile *CESS*

wanavyotaka Halmashauri ilikuwa tunawanyima bei nzuri wakulima. Nakumbuka wakati huo nadhani alikuwa Waziri Basil Mramba ndiyo tukaanzia *CESS* ama asilimia tatu na tano tukafika pale. Sasa *modality* za kukusanya bado *by-laws* za kule zinatakiwa zifanyike. Hii iliwekwa kwa sababu ilikuwa tunachaji mpaka *twenty* ngapi *percent* ikaonekana sasa tunakula, mwananchi ndiye anayepata matatizo kupata bei ndogo. Ndiyo ilikuwa hasa *principal* maana yake na mimi nilikuwa Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, tulikuwa tunachaji *CESS* kwenye tumbaku, *the way we wanted*. Ikabidi sasa tuambiwe aaaah, mnarudi mpaka asilimia tatu au tano. Hii *was a spirit* ya hii. (*Makofi*)

Kwa hiyo, hizi Halmashauri zitakapokuwa zinaweka kodi zao haziwezi kuzidi asilimia tano na kama wewe unatunga Sheria ya kuweka kodi kwenye Halmashauri yako ni lazima ufanye *bye-law* huwezi kufanya peke yako na *by-law* ni Sheria katika eneo linalohusika.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake*)

Kifungu cha 24

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu cha 25

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati natoa mchango wangu nilisema kwenye Kifungu kipya cha 25, kile kifungu kidogo cha (a) ambacho kinaelezea kwamba kinafutwa. Ie sentensi ya *one hundred thousand shillings*. Nilikuwa nasema zile tarakimu pale haziwiani na hilo neno *one hundred thousand shillings*. Sasa kwa kuwa hata kama inafutwa lakini kwenye kitabu hiki lazima ibadilike kama ni *one hundred and twenty thousand* au *one hundred thousand*, basi hiyo iwiane na hiyo *figure* iwekwe hapo tu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, ingawa ulisema wakati unajibu, sasa tunataka useme tena.

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tumelikubali hilo kwamba hili ni kosa la wazi kwamba badala ya *a hundred and twenty* kwenye maneno kumewekwa *hundred thousand*. Kwa hiyo, hii itabadilishwa.

MWENYEKITI: Kwa hiyo inasomekaje?

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: *One hundred and twenty thousand*.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake*)

Kifungu cha 26

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)

Kifungu cha 27

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 28

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri na alileta orodha mpya ya *amendment*, nimeiona nakubaliana nayo lakini nitakwenda kwenye hicho kingine kinachofuata.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)

Kifungu cha 29

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Katika huu Muswada wenyewe nitatumia hizi namba kwa sababu hayo mabadiliko sikuyapata vizuri. Hiyo ya 37 tumeshaimaliza. Sasa hii ya 38 ule ukurasa wa 13.

MWENYEKITI: Hapana tuko ukurasa 16, Kifungu cha 28 cha zamani, sasa kimekuwa Kifungu cha 29. Halafu iko 29 ya zamani tumeipa 30. Labda hatujafikia au?

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Sasa mimi nitumie hii ya kitabu kwa sababu hiyo nyingine sina.

MWENYEKITI: Ya kitabu ni namba gani soma.

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: 38 ya zamani.

MWENYEKITI: Basi hatujafikia huko.

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Ohooo, *okay*.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 30

Kifungu cha 31

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zimabila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 32

MHE. ANDREW J. CHENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa madhumuni ya uandishi tu Kifungu kipya hiki cha tatu, huo mstari wa pili na wa tatu, *before importation for clearance by the Tanzania Revenue Authority*. Mimi nadhani ni Kiswahili, mimi nilikuwa nashauri kwa sababu tunatunga Sheria tuseme *before importation for clearance through customs ukisema for clearance by TRA, TRA inasimamia Sheria na kukusanya mapato*. Sasa tunacholenga hapa ni *clearance through customs by Tanzania Revenue Authority*.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa nafikiria kwamba mchango wa Mheshimiwa Andrew Chenge unakubalika. Lakini hapa tungeishia labda kwenye neno *importation* kwamba *the relief granted under sub-section one, shall not apply to motor vehicles manufactured 10 years or more before importation*. Sasa *importation* hapa ni *jurisdiction* tunayoizungumzia ni *jurisdiction* ya *United Republic of Tanzania*. Kwa hiyo, tungeishia tu pale kwenye *importation* maneno mengine yale tuyafute.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tuondoe *for clearance by the Tanzania Revenue Authority*. Nadhani *more reasonable*.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)

Kifungu cha 33

MHE. WILSON M. MASILINGI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti. Kwanza nianza kwa kuomba radhi, nina makaratasi mengi hapa. Kwanza ule Muswada wenyewe, marekebisho yaliyotangulia.

MWENYEKITI: Mheshimiwa ngoja kwanza. Kitabu chako una-*refer* namba gani? Kifungu gani unacho-*refer* kwenye...

MHE. WILSON M. MASILINGI: Kifungu cha 33.

MWENYEKITI: 33 ya zamani au ya sasa?

MHE. WILSON M. MASILINGI: Ndiyo maana nimeanza kwa kuomba radhi ili uniruhusu nizungumze.

MWENYEKITI: Tunaomba tuwe pamoja, sasa wewe soma kilicho hapo kwenye kitabu chako ni kifungu gani?

MHE. WILSON M. MASILINGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa, ninakushukuru kwa kunielewa. Kwanza nianze kwa kupongeza...

MWENYEKITI: Ni Kifungu gani Mheshimiwa? Hatupongezani hapa.

MHE. WILSON M. MASILINGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Kifungu cha 33, ndio ninachozungumzia.

MWENYEKITI: Inayoonekana kwenye kitabu chako?

MHE. WILSON M. MASILINGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kitabu changu?

MWENYEKITI: Basi hatujafika.

MHE. WILSON M. MASILINGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mko wapi?

MWENYEKITI: Tuko kifungu cha 32 cha zamani, tumeipa namba 33. Kifungu cha 33 kipya kinaafikiwa? (*Kicheko*)

(*Kifungu Kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya BungeZima bila ya mabadiliko yoyote*)

Kifungu cha 34

MHE. WILSON M. MASILINGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na ndio maana nilianza kwa kuomba radhi na hali hii inaeleweka, Serikali mnaleta makaratasi kila baada ya dakika. Baada ya kuchangia imeleta marekebisho, ambalo ni jambo jema, inaonesha kazi ya Serikali inafanyika saa 24, ni jambo jema na huu sio wakati wa kulala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilieleza kwamba tumepokea mapendekezo ya Serikali mazuri sana ambayo nayaunga mkono na yanalenga kuwasaidia wazee wa miaka 60 na kuendelea pamoja na watu wasio na uwezo kutokana na hali yao ya kimaisha, ndio wanaisha *persons' living with disabilities. Amendment* au marekebisho yaliyoletwa nikiwa nimeshachangia yamefanya vizuri, badala ya kuita *levy*, yamekiri kwamba hii ni kodi, kazi ya Bunge, nampongeza Waziri wa Fedha, ni kodi.

Lakini marekebisho yake bado hayakukidhi ninachoomba tufanye, mimi nashauri tufute Kifungu kidogo cha nne inayopendekezwa, inayopeleka jukumu hili kwenye Mamlaka ya Mitaa, kujenga tena mfumo wa kutoa haki hii au niite inakuwa haki kwa sababu tumeshasema ni *mandatory, shall be exempted from paying property tax*. Sasa tusiachie mamlaka za mitaa kuweka mfumo wa kutekeleza hili ambalo ni la heshima kwetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili linavunjwa tarehe 16 Julai, 2010 na Madiwani wanakwenda. Sasa tunawasaidia nini kuanzia tarehe 01 Julai, 2010 hawa

wazee wetu? Tarehe 01 Julai, wazee wa miaka 60 na kuendelea, walemavu, ana jengo moja analoishi, lakini ambalo linaweza likalipa kodi. Mnajua majengo yetu ya Ilala, Temeke na kwingineko, vyumba sita, analala kimoja anakodisha vinne au vitatu, asilipe kodi. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Unasemaje humu, mwenye sheria? Huu utekelezaji, hapa sasa unasemaje kwenye sheria? Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu?

MHE. MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Wilson Masilingi, kwanza kwa maneno yake mazuri aliyoyasema juu yangu mimi na pia kumtakia heri ya yanayofanyika huko Muleba. Basi Mwenyezi Mungu amsaidie arudi hapa Bungeni na wote wanaomsumbua wawe kama malaria haikubaliki. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mamlaka ya kutunga sheria za kodi yaliwekwa kwenye Bunge hili mwaka 1984, kabla ya hapo hayakuwepo na mamlaka hayo ndio haya ambayo yameliwezesha Bunge hili kutunga kifungu ambacho tunakizungumzia. Sasa kinachozungumziwa hapa, sio Halmashauri kuweka mfumo, kinachozungumziwa hapa ni Halmashauri kuweka utaratibu wa utambuzi kwanza; utambue kwamba kweli huyu ana nyumba hii, ni yake na kwamba nyumba hii kuna kodi fulani na kwamba huyu mtu ana matatizo haya tunayoyazungumza; utambuzi huo hauwezi kufanywa na Bunge, utambuzi huo utafanywa na zile Halmashauri ambako hawa wazee wetu na kila mtu ni mzee mtarajiwa, wanaishi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiri kwamba ilivyo sasa, kifungu kile kidogo cha (4), kinawezesha mamlaka hizo kuwatambua hao na kufanya lile ambalo tumesema wafanye. Kwa hiyo, Mheshimiwa rafiki yangu Masilingi, nafikiri kama kutakuwa na tatizo basi tutakapokuja mwezi wa Novemba, tutakuwa tumepata ujuzi zaidi na wewe utakuwepo, basi tutaona kama tunaweza kubadilisha. Lakini kwa sasa hivi hiyo ndio maana yake hasa. (*Makofi*)

MHE. WILSON M. MASILINGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana kwa maneno mazuri aliyoyasema ya kunitakia heri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mimi kama tunavyofahamu, sisi ndio tunatunga hii sheria; na nimewatolea mfano na wewe umethibitisha na mimi nikakupongeza uki-*site institutional memory*. Tulipofuta kodi za kero, ile magulio, sijui kwato, ng'ombe, ni kutokana na hizi Halmashauri kushindwa kufikia azma ya Bunge hili kukusanya kodi, tena hizo ni za ngazi ya *local government*. Sasa tumefika hatua ambapo tukasema wazee watibiwe bure, bado ni taabu sana, Wabunge tunajua. Lakini akina mama wajawazito, watoto wa miaka sifuri, miaka mitano, tuliposema watibiwe bure, inatekelezwa vizuri. Ukishaachia *local government*, madaraka ambayo tunawajibu wa Kikatiba kuweka utaratibu nasema tunakwepa wajibu wetu, Mwanasheria Mkuu atuelewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema ni hivi, mwenye dhamana ya kutekeleza sheria hii sio *local government* ni Waziri wa Fedha. Sisi tunayemtuma hapa kwenda

kutekeleza Sheria hii sio *local government*, ni Mkulo kwamba kuanzia Julai wazee wa miaka 60 na kuendelea, walemavu, ana nyumba moja analala mle, asilipe kodi. Sasa kama kuna *local government* wanakuja kujibu, waje hapa. Sasa hili sio suala la kusema utambuzi mpaka uende *local government*. Hivi kuna TRA, kuna polisi, sisi tumesema wenye mali ni sisi, halafu *local government* wafanye yao na tumeshawapangia viwango. Nakushukuru Mheshimiwa. (Makofi)

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kuonekana nabishana, lakini sheria hii ni sheria ya *local government* na ndio wanaoisimamia sheria hii na tusije tukafika mahali ambapo kila mamlaka inayotakiwa kutekeleza wajibu wake inashindwa kutekeleza halafu Bunge ndio linachukua mamlaka hayo, utali-*overload* Bunge. Nafikiri ni lazima, na Waheshimiwa Wabunge ni Wajumbe wa Mabaraza hayo, ni Madiwani, kwa hiyo tukafikiri kwamba hivi ilivyo hasa kwa utambuzi, kwa sababu kwanza kusema huyu ana nyumba hiyo, Bunge hili haliwezi kufanya hivyo ni Halmashauri. Kwa hiyo, naelewa mantiki ya sheria hii na nafikiri kwamba kilivyo kifungu cha (4) ndivyo hivyo kinavyotakiwa kiwe.

MWENYEKITI: Sawa Waheshimiwa, angekuwa ameleta *amendment* tungepiga kura, lakini kwa kuwa hakuleta, kifungu kinaafikiwa?

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 35

Kifungu cha 36

Kifungu cha 37

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 38

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)

Kifungu cha 39

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshaelewa ni nini kimefanyika. Kwa hiyo, sina hoja tena.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 40

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)

Kifungu cha 41

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 42

MHE. ANDREW J. CHENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nisaidiwe kiingereza changu mimi labda sio kile ambacho wengine wanakitumia. *Any person who is involved in fraud*, sina tatizo na hilo, *or who takes an action or omission*, sasa hapa nina tatizo ningependa tu nisaidiwe, *how does one take an omission?* Ndio maana nilikuwa nasema nadhani tuna tatizo la msingi la lugha hapa. Kwa hiyo, mimi ningeshauri ni afadhali tukawa *repetitive* kuliko kuacha ilivyokaa. *Who takes an action or who omit to take an action*, ndio ina-flow vizuri na inakuwa na mantiki iliyokusudiwa na sio kama ilivyokaa hivi sasa. Nakushukuru sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Halafu na ile *rewording* ile ya 19(3), natumaini inakaribia kumalizika, kwa sababu tumekaribia huko. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo la uandishi hapo, *any person who is involved in fraud or takes an action or omission towards fraudulent avoiding tax*; nafikiri kuna mchanganyiko, naomba waandishi wa-draft upya na wanilettee hapa, nitatoa maelezo baadaye. Tuendelee kwanza.

MWENYEKITI: Ninasubiri, hiyo ni kazi ya pili, ninamatumaini ile nyingine wameshaileta.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu ilisubiri marekebisho ya kiuandishi)

Kifungu cha 43

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)

Kifungu cha 44

MHE. SIRAJU J. KABOYONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hiki Kifungu katika mchango wangu nilikuwa nimependekeza kwamba yale marekebisho ukienda ukurasa wa tatu wa marekebisho, kwenye eneo la *packaging materials*, imewekwa tu *fruit juice* na *dairy products*. Sasa *packaging materials* kwa tafsiri pana ni pamoja na magunia, ni kwa nini magunia hayawekwi? Nataka ufafanuzi.

MWENYEKITI: Ni nani anayetakiwa afafanue sasa? Mheshimiwa Waziri?

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunazungumzia *packaging materials* ambazo zinatumiwa karatasi, plastiki, kwa hivyo magunia ni kitu tofauti kabisa na hata kwenye kodi inatozwa *under different item*.

MHE. ZAYNAB M. VULU: Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na Mheshimiwa Kaboyonga kwenye suala la vifungashio; kwa kuwa Mheshimiwa Waziri, amezungumzia suala la vifungashio vya karatasi na plastiki, nilikuwa naomba suala langu nililomba la vifungashio vya dawa za binadamu na lenyewe lipatiwe ufafanuzi.

MWENYEKITI: Uliomba nini? Hebu sema vizuri.

MHE. ZAYNAB M. VULU: Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ninachangia nilisema vifungashio vya dawa vitolewe kodi iwe kwenye *zero rate* na wakati anatoa majibu yake ya hoja za msingi, hakulijibu.

MWENYEKITI: Kwani wanachaji kodi? Wanatoza kodi?

MHE. ZAYNAB M. VULU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio wanatoza.

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majibu yangu nilisema dawa za binadamu hazitozwi kodi kwa kiwango cha sifuri, ni *zero rated*. Vifungashio vya dawa havitozwi kodi ni *zero rated*.

MHE. DR. ZAINAB A. GAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na hilo lakini nilikuwa nataka kujua iko kwenye maandishi? Kwa sababu, tunazungumzia sheria.

MWENYEKITI: Kwani vifungashio vya dawa, si ni makaratasi? Mheshimiwa, hebu soma ulipoandika.

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: (*Hapa sauti haikusikika*).

MWENYEKITI: Tunaendelea Mheshimiwa Dr. Zainab Gama?

MHE. DR. ZAINAB A. GAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi niko hapo hapo kwenye vifungashio vya dawa, ninaomba a-specify kama ni *zero rating*, nitampa mfano, uchukue dawa inaitwa *carbomazapen*, ambayo inachukuliwa na kutiwa ndani ya mfuko, imetoka tu ndani ya mfuko, inauzwa rahisi. Lakini uchukue *carbomazapen* iliyowekwa katika vifungashio vingine *special*, inauzwa *very expensive* na hata hawa watu wa *epilaptic cases* wanashindwa kununua. Kwa hiyo, mimi naomba a-specify truly vifungashio vyote, *zero rating*.

MWENYEKITI: Kwanza majina yenyewe hayo ya dawa, unamtegemea Waziri wa Fedha ayajue? (*Kicheko*)

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli haya yote yaliyotajwa siyafahamu, kwa sababu sina utaalamu huo. Lakini tulichojibu sisi ni kwamba dawa za binadamu zinazotengenezwa hapa nchini, zinatozwa VAT katika kiwango cha sifuri. Kodi ya Ongezeko la Thamani wanayolipa kwenye vifungashio, yote hurejeshwa kwa watengenezaji wa dawa hizi na kwa hivyo hakuna kodi inayokwenda kwa mlaji. Mahitaji mengine yatafanyiwa kazi katika mwaka ujao. Sasa labda tatizo liwe ni maana ya kutoza kodi kwa kiwango cha sifuri. Labda sasa hilo litakuwa ni tatizo tofauti. Lakini ukweli ni kwamba hayatozwi kodi. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Sasa Mheshimiwa Zaynab Vulu, huruhusiwi kwa sababu umepewa nafasi mara mbili. Anayepewa nafasi ya pili ni Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, wewe umeshapewa nafasi mara mbili. Mheshimiwa Dr. Zainab Gama?

MHE. DR. ZAINAB A. GAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemwambia *carbomazapen*, akaona hiyo ni dawa *complected*, nampa mfano wa *paracetamol*. *Paracetamol* ambayo ipo tu ndani ya chupa na kutiwa ndani ya karatasi ni *cheaper* kuliko *paracetamol* ile iliyofungwa katika *blisters*, ni *very expensive*. Nampa ile dawa ambayo yeye anaweza kuijua. (*Makofi*)

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunachanganya mambo kwamba ile karatasi anayoizungumza yeye, karatasi yenyewe ni ghali, sio kile kifungashio. Sasa kwa hiyo, kuna tofauti kati ya kutoza kodi, kuna dawa za kawaida hizi unaweza kuzinunua kwa kifungashio tofauti, *paracetamol* hii au *panadol* ukainunua kwa shilingi 100, na kuna karatasi nyingine ambazo zimetoka Kenya au sijuu zimetoka wapi, zinafungwa kwenye karatasi tofauti, ukanunua kwa shilingi 1,000. Sasa hiyo sio kodi, tatizo ni kile kifungashio kilichotumika ambacho ni tofauti na kutoza kodi. Lakini kwa ujumla wake kama ni kifungashio, tunatoza sifuri. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Tumemuelewa, sasa yeye anazungumzia kodi. Hizo gharama hizo sio kodi? Mheshimiwa Cheyo, ni suala hilo hilo au?

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwenye hicho Kifungu cha 40, fasili ya pili yaani kifungu kidogo cha pili, *the supply of intra-transport services from the farm to the processing plant of sugarcane, sisal or tea*. Sasa wakati nachangia nilimwambia Mheshimiwa Waziri kwamba mojawapo ya vitu vinavyofanya bei ya pamba ishuke ushuru kwenye *transportation* ni VAT kwenye *transport* kwa mfano ya beli kutoka kwenye kiwanda kwenda kwenye *export point*. Sasa pia nilitaka kujua kama tumeona umuhimu wa chai ni kwa nini tusione umuhimu wa pamba ambao labda kama hiyo itaondoka, bei yetu ya pamba kwa wakulima inaweza labda kuwa shilingi 700/= au shilingi 800/= kwa sababu hii ni sehemu kubwa sana na hii ni mambo ya kilimo kwanza.

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachozungumza sisi hapa ni *organise farming* na maana ya *organise farming* ni *small holder* yaani kwenye miwa, chai na hilo ambalo anazungumza tumetaja kuna *small holders* ambao kile kiwanda chenye kinalima miwa lakini wananchi wanaozunguka

kile kiwanda wanalima pia miwa wale wanakiuzia kile kiwanda. Sasa *process* ni kwamba *within a certain number of hours* lile zao lazima liwe limefika kwenye kiwanda.

Sasa wale ndiyo waliomba hiyo na tukasema kama kuna mazao mengine ambako na kwenyewe kuna *organization* ya namna hiyo tuletewe tutayazungumza na tutaangalia ndiyo tulichosema sisi hapa. Lakini tulichosema sisi hapa ni kwamba kule kuna *small holder farming system* na hii iko kwenye mazao hayo matatu kwa sasa. Sasa kusema kwamba unachukua kahawa kutoka Kagera na kuipeleka Dar es Salaam *for export* hai-*qualify* ile *concept* ya *small holder*.

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, labda kwa sababu ndugu yangu anatoka Morogoro, lakini anajua wazi kabisa kwamba kuna kiwanda cha kusindika pamba na hicho kiwanda cha kusindika pamba kinapata pamba hiyo kutoka kwa *small holders* mbalimbali wa heka mbili, tatu, nne na pamba hiyo yote inapelekwa pale sasa hawa wanakuta *charged VAT if they have to buy services za transportation*, wasipofanya wataingia matatizo na TRA. Kwa sababu umeingiza hapa *physical receipt*, sasa unapotoa *physical receipt* kwa mtu amekusafirishia hiyo pamba ni lazima itaongeza gharama kwa hiyo ni *concept* hiyo hiyo huko ni chai, huku ni pamba pawepo na ubaguzi.

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, sentensi yangu ya mwisho ni kwamba kama kuna mazao mengine wanayofikiria kwamba yana-*qualify* katika hii *concept* ya *out growers* tulate, hatujafunga *chapter*, tuletewe yatatazamwa na yatashughulikiwa.

MHE. JOHN M. CHEYO: Nimekubali. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Lakini sasa kama hivyo ndivyo maana yametajwa wala hukusema ama mazao mengine yatakayo-*qualify* hakuna kitu cha namna hiyo hapa umetaja *specifically rate* ile, hayo mengine yanaingiaje, hayawezi kuingia *unless* umefanya *amendment* ya aina fulani hapa.

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, *for this financial year* haya tuliyoyataja ndiyo yaliyo-*qualify*, sasa kama yatapatikana mengine ambayo yataletwa tuna *task force* ambayo yanatazamwa tutaangalia huko mbele ya safari.

MWENYEKITI: Kwa hiyo hapo Mheshimiwa Cheyo unabidi ukazane urudi. (*Makofi/Kicheko*)

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake*)

Kifungu cha 45

MHE. SIRAJU J. KABOYONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa mimi naomba ufafanuzi ili niweze kuona kama uelewa wangu ni sahihi, katika michango iliyotolewa wakati tunajadili Muswada tulisema pamoja na mambo mengine kwamba

unafuu wa kodi yanayopewa makampuni ya kuchimba madini upelekwe mpaka kwa wakandarasi wa hapa nchini kama watafanya kazi za uchimbaji. Nataka ufafanuzi tu kama je, kifungu hiki ndiyo kinajibu hoja hiyo kwa jinsi kilivyokaa?

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kwenye sekta hiyo kinachozungumzwa ni sheria ni *sub-contractor*, hatuzungumzii *local contractor* kwa hiyo ndiyo kule kwenye madini kuna *sub-contractor* kwa hiyo kuna *main contractor* halafu na *sub-contractor*. Sasa *sub-contractor* amekuwa *taken care off* lakini ukisema tu kwamba ni *local contractor* maana yake ni kwamba hata kama mtu hana *qualification* yoyote ili mradi ni *local* basi tusifanye hivyo lakini *sub-contractor* ambaye ameingiliana mkataba na yule *contractor* yule ana *qualify as if he was the contractor*.

MWENYEKITI: Kwa hiyo umejibiwa.

MHE. SIRAJU J. KABOYONGA: Sijaridhika vizuri hasa hasa nataka Mheshimiwa Waziri kama alivyokuwa ananielekeza asisitize juu ya *sub-contractor* ambaye ni *local* sio *sub-contractor* wa nje mimi nataka *sub-contractor* ambaye ni *local* kwa maana ya kufungamanisha uchumi wetu na haya makampuni yanayokuja kuchimba ndiyo niko hapo. Kwa hiyo, naomba ufafanuzi huo. Je, kipengele hiki kinatoa unafuu huu kwa *sub-contractors* ambao ni *local company's*?

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, *agenda* kubwa hapa ni kwamba tunakwenda kujadiliana na zile kampuni za madini (*Mineral agreements*). Sasa *details* za namna hiyo zitajitokeza wakati wa majadiliano lakini mimi ni vigumu sana kwa sababu sio mtaalam wa sekta ya madini kuweka *specifically* kwamba *local contractor* lazima awe *sub-contractor* nitakuwa naingilia mambo ambayo hata kuzungumza kwenyewe hatujazungumza.

MWENYEKITI: Kwa sababu hii haisemi *foreign* wala *local* inasema *sub-contractor*.

MHE. ISMAIL JUSSA LADHU: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina mawili katika kifungu hiki moja ni hilo ambalo amekuwa analifafanua Mheshimiwa Waziri, mimi nadhani suala hapa analolizungumza sio *MDAs* kwamba itawafunga kwamba lazima wachukue *locally sub-contractor* ninachozungumzia ni huu unafuu kwamba utolewe kwa wote ili iwe ni *incentive* kwao kuweza kuwatumia *locally sub-contractors*.

Kwa hiyo, hiyo haihusiani na suala la kwamba *MDAs* zitakuwa zinawafunga kwa sababu hapa hatuingilii *MDAs*, tunachosema hili ambalo ni jukumu la Wizara ya Fedha na Serikali kutoa unafuu huu kwamba sasa tunatunga sheria kwamba unafuu huu utolewe pia kwa *locally sub-contractors* ili sasa iwe ni *incentive* pia kwa hawa *mining company* na hao *contractors* waweze kuwatumia hawa *locally sub-contractors* na hivyo kulipata fungamanisho tunalolizungumzia ambalo Mheshimiwa Kaboyonga amelizungumzia na pia katika mapendekezo ya Kamati yaliyozungumziwa ya Fedha na Uchumi na pia katika mapendekezo ya Kambi ya Upinzani na pia Wabunge wengi ambao walikuwa

wamechangia hoja hii. Kwa hiyo, kwa hili nilikuwa nataka nipate ufafanuzi na hili la pili nitaelieleza baadaye. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ufafanuzi umetolewa endelea la pili.

MHE. ISMAIL JUSSA LADHU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante twende tu la pili, nilikuwa nasema katika mapendekezo mengine ambayo yametolewa vilevile na Kamati na pia Kambi ya Upinzani lilikuwa ni suala la kuongezea *incentive* ili kutumika *local sub-contractors* na kwa hivyo kuchangia katika uchumi wetu ilikuwa ni suala la ku-*introduce 50% with holding tax* kwa hizi *foreign contractors* ili kuwa-*discourage* na kukubali ku-*encourage* kutumia wandama hili halikugusiwa kabisa katika maelezo ya Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachozungumza ni kwamba kuna mkataba kati ya Serikali labda na Barrick, sasa hakuna kifungu kama hicho kwa hiyo, ni kipya kabisa. Kwa hiyo katika majadiliano tuliyokuwa tunazungumza ndiyo tunaweza kama Serikali kusema kwamba *suppose you do this or you do that* lakini mimi siwezi kujibu hapa kwamba yaingie kwenye sheria kwamba kweli tukitoka hapa kuanzia Julai, tutakuwa tunawa-charge wale watu asilimia 15 kwa sababu haikuwemo kwenye mikataba ile na wala haipo. Kwa hiyo, ni kitu kipya ambacho kimesemwa tumeyachukua, tutakapokuwa tunazungumza na wenzetu tutangalia kwa hiyo hatuwezi kusema kwamba Serikali kwamba kweli kuanzia kesho sisi tutaanza kuwa-charge wale watu asilimia tano, tano.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)

MWENYEKITI: Tunarudi kule tulikoacha, kazi kifungu cha 19(3) maneno yakoje Mheshimiwa Mwansheria Mkuu.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza kuwakumbusha kwamba tunachofanya tunabadilisha sheria ya kodi na kifungu hicho kinachozungumzia kinahusika pia na kifungu cha 109 cha sheria ya kodi. Maneno ambayo napendekeza yawepo kwenye kifungu hicho ni kama ifuatavyo; *“An approved tax consultant who knowingly or recklessly aids, abets, conceals or induces a taxpayer to file a misleading or fraudulent statement commits an offence under this Act.”*

Sasa ukishafanya hayo yanatosha kwa sababu *offence* hiyo matokeo yake yako kwenye kifungu cha 109 na adhabu imetamkwa pale, imetamkwa kwenye 109(a)(b). Ahsante.

MHE. ANDREW J. CHENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu kwa marekebisho anayopendekeza ya kwenye kifungu hicho hasa kwa yale niliyoanza nayo niliposema *aids, abets* niliendelea nikasema *counsel* mimi kidogo hapo nina tatizo huyu ni mtu anayeshauri kwa hiyo lazima *counsel* sio *conceal* tukielewana hapo mimi sina tatizo na AG ku- *counsel* ni kuficha lakini hapa

anashauri, anamashauri mtu afanye vituko ndiyo hiyo nilikuwa nasema *aids, abets, conceals or induces* ndiyo nilivyosema mwanzoni ikienda namna hiyo wala mimi sina tatizo.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mimi nakubaliana lakini huwezi kum-*punish* mtu kwa kushauri utam-*punish* kama ameficha kushauri kama inavyotakiwa. Kwa hiyo neno lile *conceals* halina maana ya *counsel* kwa sababu *issue* ya *counsel you can not punish for counselling* utam-*punish* tu, utamuadhibu kama ame-*conceal* katika *concealing*. Na katika *counseling* pia anaweza pia kumfanya yule a-*counsel* tunafahamu kwamba tatizo tulilonalo ni *a evading tax* lakini *avoiding tax* inaruhusiwa *you can avoid tax for is your concern* lakini unapo-*evade* ndiyo *problem*. Kwa hiyo, hapa sio *counseling* hapa ni *conceal* Mheshimiwa Chenge kubaliana na mimi tu yaishe. (*Kicheko*)

MWENYEKITI: Kwa hiyo tunashukuru sana kwa utalam uliouleta kwa haraka kifungu hiki kinaafikiwa.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Kifungu cha 42

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa naomba tusikilizane halafu tusaidiane, ninapendekeza kwamba hapa sasa ndiyo kuna suala *evasion of tax* ambayo yule anayekushauri u-*avoid tax* lakini anakosea mpaka anakushauri ku-*evade*, ninapendekeza maneno yasomeke kama ifuatavyo; “*Any person who willfully or fraudulently commits or omits to do any action which has the effect of evading tax or recovering tax, commits an offence and upon conviction shall be liable to a fine of twice the amount of tax involved in the commission the offence or to pay five million shillings, whichever amount is higher, or to imprisonment for a term of two years or to both.*”

MWENYEKITI: Naomba turudie kidogo, maana...

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, *any person* naingiza maneno mapya *willfully or fraudulently commits or omits to do any action which has the effect of evading tax or recovering tax and then* mengine yale yanaendelea kama kawaida.

MWENYEKITI: Kuna mtu anafikiria nadhani inasomeka vizuri zaidi.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bunge Zima imemaliza kazi yake.

(*Bunge ilirudia*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa mtoa hoja taarifa.

Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2010 (*The Finance Bill, 2010*)

(*Kusomwa kwa Mara ya Tatu*)

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imepitia Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2010 yaani *The Finance Act, 2010* kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisha yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba taarifa hiyo sasa ikubaliwe rasmi, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

NAIBU SPIKA: Hoja imeungwa mkono sasa nitawahoji, nafikiri walioafiki wameshinda. (*Makofi*)

ND. NENELWA M. WANKANGA – KATIBU MEZANI: Muswada wa Sheria kwa ajili ya kutoza na kubadili viwango vya Kodi, Matozo, Ada na ushuru na kufanya mabadiliko katika Sheria mbalimbali zinazohusu ukusanyaji na uratibu wa mapato ya umma (*A bill for An Act to Impose and alter Certain taxes, duties, fees and to amend Certain written laws relating to the Collection and Management of Public revenues*).

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa na Bunge*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, huu Muswada wa Fedha umepita na katika mzunguko wetu wa kusoma hotuba ya Bajeti hii miaka miwili tumebadili utaratibu kwamba baada ya hotuba ya Bajeti kujadiliwa tunaingia moja kwa moja kwenye *Finance Bill*.

Zamani ilikuwa tunaendelea mpaka tumalize Wizara zote halafu tunaingia *Appropriation Bill* halafu ndiyo tunaingia *Finance Bill* kwa hiyo, Serikali ilikuwa haiwezi kufanya jambo lolote mpaka tumalize sisi. Lakini kwa sasa Serikali inaweza kuendelea kabisa na matumizi yake kwa sababu tumeshayapitisha mfumo wa kukusanya mapato kwa kupitisha sheria hii. Kwa hiyo, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha kama walivyosema Wabunge katika mijadala yote suala la matumizi itabidi muangalie

kwa undani sana na vyanzo vingine vya kodi viendeleo kubuniwa na vile vilivyoko vifanyiwe kazi kimakini zaidi ili tuweze kuongeza mapato kuliko haya tuliyonayo sasa. Vinginevyo tunakupongeza wewe na wataalam wako wote kwa kazi nzuri mliyofanya, ahsante. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hatuna shughuli zingine kwa ajili ya leo na saa nadhani karibia imefika nina kazi, nina tabia ya kufanya kazi mpaka usiku huwa siangalii saa. Kwa hiyo, kesho tunaingia na hotuba ya Waziri Mkuu nayo ina siku tatu tofauti na ile ya Wizara ya Fedha hatukuwa na mafungu, ofisi ya Waziri Mkuu kutakuwa na mafungu, maana yake siku za mjadala zinaweza kuishia mbili tu, kwa sababu tunaingia mafungu yote ya mikoa na mengine, kwa hiyo kama nilivyokuwa nawashawishi kwamba mjiunge kule kwingine ilikuwa hivyo, tuna muda mfupi sana.

Kwa hiyo, nawatakia jioni njema, mkaangalie mpira wa saa tatu ya usiku, huu mwingine mmeukosa lakini nawashukuru sana, nawatakia jioni njema ahsante kwa shughuli nzima. Naahirisha kikao mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 12.40 jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatano, Tarehe 16 Juni, 2010 saa tutu asubuhi)